## KUHUSU LAANA

Katika waraka huu wa pili (ambapo wa kwanza wake ulihusu kutubu kwa ajili ya dhambi za Taifa) tunataka kuangalia juu ya wazo hili la "laana" itokanayo na mambo yaliyopita. *Tunataka kuangalia, iwapo laana ya mtu binafsi au itokanayo na vizazi vilivyopita, inaweza kuwafungia wakristo ndani ya vifungo na kuwazuia kutokana na kupokea baraka za Mungu na Urithi wao katika Kristo*. Kuanzia hapa mwanzoni mwa makala hii, hebu tuweke wazi kabisa kuwa hapa tunaongelea kuhusu mtu ambaye amehukumiwa kwa tendo la dhambi zake, akatubu na kugeuka kutoka katika dhambi zake, na akamwamini Bwana na Mwokozi Yesu Kristo kwa ajili ya wokovu wake, amezaliwa mara ya pili na kujazwa Roho wa Mungu, ameingizwa katika Agano Jipya ndani na kupitia Yesu Kristo. Hapa, kwa mtu huyo, hakuna zaidi! Hakuna kitu kilicho pungua na kwa wakristo kama ilivyoelezwa katika Agano Jipya, kuwa wakristo wa aina hiyo kama mitume walivyokuwa wakiwaandikia.

### Ushahidi wa Agano Jipya

Ni kitu gani basi ambacho mitume wamewaandikia wakristo katika Agano Jipya? Wanayashughulikiaje mambo yanayojitokeza katika makanisa na watu wa Mungu? Wanayatambuaje matatizo hayo na wanatoa ushauri gani na maelekezo yapi kwao? Kwa mafundisho yoyote yale mapya, ambayo yanatoa ushauri na maelekezo yanayohusiana na wakristo, ni lazima mafundisho haya yasimamie katika misingi au yapate kuungwa mkono na maandiko ya mitume au kutoka katika mafundisho ya Yesu mwenyewe.

Kwa hiyo basi, ***mitume wanasemaje*** juu ya mafundisho yahusuyo wazo hili la "laana" zilizopita, kwamba zinaweza kuzuia maisha ya wakristo, au ya kanisa au nchi isipate kuendelea! Kwa kweli ***mitume hawasemi chochote kile***, hakuna chochote wasemacho. Hakuna; na halikadhalika, ***hakuna hata mstari mmoja wa Neno la Mungu unaosema chochote kile***! Wala mitume hawajaribu angalao kutamka au kugusia juu ya jambo hilo. Akili zao haziwapi kufikiria kabisa juu ya jambo hili. Yako wapi basi mausia yao wanayoyatoa kwa wakristo katika kuchunguza maisha yao ili kuhakikisha na kuwa makini sana, kwamba laana haitendi kazi yake wakati wanapokuwa katika shida ndani ya mienendo yao binafsi na kiroho? Mausio ya aina hiyo hayapo kabisa. Ni kweli kwamba Mtume Paulo anazungumza kuhusu laana, lakini anaizungumzia katika mtindo wa tofauti kabisa - yaani, anazungumzia kuhusu Kristo "***akitukomboa kutoka katika LAANA ya sheria***". Tunakuja kuangalia kwa makini kuhusu jambo hili baadaye kidogo, lakini, hakuna sehemu yoyote ile ndani ya Agano Jipya lote, ambayo hata kutajwa tu kwamba laana kutoka katika mambo yaliyopita au kwamba inaweza kuzuia mwenendo wa kiroho wa mkristo au kanisa au Taifa.

Lakini sasa, sisi tutoe sababu gani tunapoona jambo hili liko kimya katika Biblia? Mafundisho hayo ya kisasa au mapya yako wazi sana na yametiririka kwa undani sana na kwa kuwa ni hivyo, basi bila shaka yangepasa kuwakilisha sehemu muhimu sana na ya lazima katika ukombozi wetu katika huyo Kristo Yesu; ikiwa jambo hili kama lingekuwa lina ukweli wowote ule.

Vitabu vingi sana vimewahi kuandika kuhusiana na jambo hili la laana, basi bila shaka, kwa hakika tungetegemea kupata misingi fulani ya mitume na ya kibiblia ndani ya mafundisho yao hayo mapya. Lakini basi, ***kwa nini hakuna hata mtume mmoja ndani ya Biblia anayejaribu kulitaja jambo hili katika nyaraka zake wanapoyaandikia makanisa***? Je, wao walikuwa ni wajinga kiasi kwamba wameshindwa kuelewa umuhimu wa ukweli huu? Ikiwa ni hivyo basi, wao wanahusika katika kuwaacha ndani ya ujinga huo, sio tu wakristo wa vizazi vingi vijavyo, na kwa hiyo kuwazuilia uhuru wao katika Kristo. Kama ni hiyo, basi mitume wamewaachia umati mkubwa wa watu katika vifungo na giza kupitia katika karne nyingi kwa sababu ya kushindwa kwao kupokea na kufundisha mapokeo haya? Bila shaka yoyote ile, kulikuwepo na uzinzi na mila mbaya nyingi nyakati za Agano Jipya. Kwa hiyo, kwa nini basi, hawa mitume hawakuwaonya watu wa Mungu, ili wafahamu kwamba tatizo lolote lile mnalopata linatokana na laana iliyowatangulia? Kwa nini basi hawakusihi ili kuchunguza maisha yao ili waone iwapo wao wenyewe au mababu zao kama watakuwa wamehusika katika matendo ya kishetani ambapo wengi wao wangeweza kuwa hivyo, na hivyo wangefanya hima kutubu na kuungama mambo hayo na kisha kutangaza uhuru wao katika Kirsto? Ni wapi ambapo wanashauri kufananishwa na mtu binafsi, kanisa au nchi? Ikiwa mambo hayo ni ya ukweli, basi, hilo sasa ni tatizo kubwa sana.

Hatuwezi kuachwa katika ujinga wetu, wala hatuwezi kuachwa katika vifungo! Lakini cha ajabu ni kwamba, jambo hili la laana ya mababu halitajwi mahala popote pale wachilia mbali kufundishwa pia. Elimu hiyo wanayoitoa kwa watu sio sehemu ya mafundisho ya mitume, ya Yesu Kristo wala Biblia kwa makanisa halikadhalika Agano Jipya halijafundisha hiyo kwa makanisa pia. Hakuna sehemu yoyote ile ya Agano Jipya ambapo Yesu Kristo au hata mitume wanapojaribu kutia laana ya Agano la Kale lililofanywa kati ya Mungu na

Waisraeli kuitii kwa wale walioingizwa katika ufalme wa Mungu kwa kupitia uzao mpya wanavyofanya nyakati hizi.

Haya, au pengine labda wakristo wa nyakati za Agano Jipya, wao walikuwa na "usafisho" na zaidi ya yote "kupitia" kuhukumiwa na labda mara tu baada ya kuokolewa, wakristo hao hawakuwa na matatizo, na kwa hiyo wao hawakuhitaji aina hii ya mafundisho? Lakini kwa hakika mawazo hayo sio ya kweli kulingana na Neno la Mungu linavyotuonyesha. Watu walipata kuokolewa au kupokea ujumbe wa Injili kama mtu binafsi au maelfu ya watu kwa wakati mmoja. Na yawezekana pia kuwa hali ya mioyo ya wengine wao haikuwa safi au walianza vema, lakini hawakuendelea kutembea katika utiifu wa Imani na Upendo. Kama ilivyokuwa nyakati hizo halikadhalika nyakati hizi. Kimsingi, watu ni wa aina ile ile katika kila kizazi na huyapokea mambo kwa njia ya tofauti katika wokovu ambao Mungu amewapa. Na kama vile ilivyo nyakati hizi za leo, kama tusomavyo katika Agano Jipya ndivyo ilivyo kuwa pia nyakati za Agano Jipya – yaani, watu makanisani walikuwa na aina zote za matatizo yanayotofautiana: dhambi, tabia za kimwili, matendo ya uongo, uchungu, mivutano n.k. Jaribu tu kujisomea mwenyewe Wakorintho au Wagalatia, kwa mfano – utagundua haya!

Haya, iwapo wokovu wa Mungu ni ule ule leo kama vile ulivyo kuwa nyakati hizo, na iwapo mwitikio wa watu na matatizo yao ni ule ule leo, kama vile ilivyo kuwa nyakati zile za Agano Jipya; basi sasa ni kwa nini! Oho, jamani! ***Ni kwa nini basi Yesu Kristo mwenyewe pamoja na mitume wake hawakuwafundisha watakatifu au hata makanisa juu ya mambo hayo*** (au hata wale wasioamini) kwamba laana zilizopita zinaweza kuwaathiri watu wa Mungu na kuwaweka katika vifungo au giza – kama tunavyoelezwa leo na hao walimu wa kisasa? Kwa nini hawakuweza kabisa kuonyesha kwamba matatizo yetu tunayoyapata sasa tukiwa kama ni watu wa Mungu, yanatokana na laana kutoka mambo yaliyopita? Jambo hili halipaswi liwe kama vile jambo la kudhanidhani au kubuni, au kama kazi ya ubunifu ya mwanadamu. Ni jambo la hatari sana katika utata wake, kwamba ni lazima tuwe makini sana hapo katika kuyagundua mafundisho kutoka katika Agano Jipya; kwa sababu humo katika Biblia mumejazwa taarifa zote zihusuzo ukombozi wetu na wokovu katika Kristo. Lakini hata hivyo hakuna popote pale ndani yake unapoweza kuyaona mafundisho yao hayo!

Kutokana na hilo, basi hii pekee ingetosha kabisa kutuonya sisi leo, kuwa kuna kitu ambacho si cha kweli ndani ya mafundisho yao hayo na kwamba hatupaswi kuyapokea ndani ya mioyo yetu. Hii ni nyongeza yao kwenye Injili. Hii ni sumu ndani ya mioyo yetu iliyokwisha kombolewa na Kristo. Hata kama itatokea baadhi ya watu kuamini kuwa wanaweza kuipata mistari katika Agano la Kale inayounga mkono mawazo yao, bado ni lazima tutambue kuwa, kitu chochote kile kinachotakiwa kwa ajili ya wokovu na ukombozi wetu na maisha ya Ki-Mungu, kimeunganishwa na kufunuliwa hivyo pia ndani ya Agano Jipya. Kazi ya Agano la Kale ni kuonya mbele juu ya wokovu na ukombozi kwa njia mbalimbali na hii inasaidia zaidi na kufafanua na kukielezea vizuri kile kinachofundishwa ndani ya Agano Jipya. Lakini kama tunafundisha kama kwa kulazimisha kwa wokovu wetu au ukombozi kama wakristo na tunajaribu tu kupata maelezo mengine kutoka Agano la Kale kwa ajili ya kukidhi dhamira yetu ya kutaka kuungwa mkono katika jambo hilo, pasipo hata kuliona kwanza jambo hilo likifundishwa pia au kutajwa ndani ya Agano Jipya; basi ikiwa ni hivyo, hapo mafundisho yetu yatakuwa yanapingana na ukweli wa Injili.

Na hiyo sio sawa hata kidogo: hiyo ni hila, nasi tutakuwa tukiwadanganya wengine katika kufundisha hilo. Elimu yao hiyo, inapinga kabisa mafundisho ya Yesu Kirsto na ya kwamba yeye Yesu ndiye aliyesulibiwa. Hiyo ni nyongeza ya kibinadamu katika waraka wa Wagalatia. Bila shaka hakuna kupishana kabisa kati ya Agano la Kale na Agano Jipya, lakini yapo maendeleo na mabadiliko ya kimsingi. Yamechukua sehemu yake kwa sababu ya yale yaliyofanywa pale Kalvari. Kama vile ilivyo kwa makosa mengine mengi, hasa yale ya nyakati hizi za leo; mafundisho hayo hayakutokana na Biblia, bali watu wameyaanzisha au kuyabuni kutokana na mawazo yao au mtindo wao wa kufikiri, kisha wakayafasiri maandiko kulingana na matakwa ya muundo wao. *Na wanapindisha na kubadilisha maana halisi ya maandiko, wakayatumia mpaka yakubaliane na muundo wa mawazo yao*. Hivyo ndivyo wanavyofanya katika wanachoweza kukitumia katika Agano Jipya ili kuunga mkono mafundisho (mapokeo) yao.
Lakini hebu tutazame jinsi ambavyo watu hao wangejaribu kutafsiri baadhi ya maandiko kutoka katika Agano Jipya, ambayo ndiyo mistari wanayoitumia kunukuu. Yak.3: 7-10 na Ufu. 22:3. Hayo ni baadhi ya maandiko yanayotumiwa kunukuliwa ili kuonyesha watu kuwa laana na kulaaniwa ni vitu vinavyoendelea kuwepo leo. Kwa kadri ilivyo siyo mbaya, lakini pia wao *wanaendelea* kusema kuwa, kwa sababu laana inaendelea kuwepo, kwa hiyo wakristo wenyewe wanahitajika kutambua kuwa wanapaswa kuwa na hakika wameshawishiwa na kuzuiwa katika maisha yao kwa laana. Lakini maandiko haya "rukii" kwenye ufahamu wa hatua hiyo wanayodai wao. Kwa kweli maandiko hayo mawili hapo juu wala hayafundishi hivyo; badala yake ingalipo inaendelea siku za leo, na watu wanafanya mambo ambayo hawapaswi kuyafanya, kwa mfano, kuwalaani wengine, na kwamba katika mbingu mpya na nchi mpya hakutakuwepo tena na laana, au tungeweza kusema kuwa, hakutakuwepo tena na hukumu - kwa ajili ya dhambi na uasi. *Hata hivyo mistari*

*hiyo hapo juu haileti uhusiano wowote kati ya matatizo ya maisha ya wakristo na laana ambayo ingeweza kuwekwa kwao au kwa mababu zao, kana kwamba hayo ndiyo iwe ni sababu ya mataizo katika maisha yao!* Hakuna mahali popote pale katika nyaraka zote za Agano Jipya, ambapo hata kwa umbali tu inahesabiwa au hata kutajwa tu kwamba ndiyo sababu inayosababisha matatizo au mateso katika maisha ya wakristo, (au katika maisha ya mji au taifa). Yakobo hasemi hapo kuwa, "Tazameni, watu wanalaani, kwa hiyo mnajua laana bado inaendelea kuwepo, na kwa hiyo maisha yenu yatazuiwa kwa laana. Na kama mnalo tatizo linaloendelea katika maisha yenu, basi hilo linaweza kuwa limesababishwa na laana zilizopita. Kwa hiyo mnapaswa kuchunguza miienendo ya mababu zenu kwa makini sana ili kugundua kuwa uwezekano wa mizizi ya aina hii ya laana katika maisha yenu, na hivyo kuomba ukombozi kutokana na hilo." Huu ni upumbavu mkubwa sana kutafsiri maandiko hayo ya Yakobo kwa jinsi hiyo. Anachokifanya Yakobo hapo katika mistari hiyo, ni kutufundisha tu kwa uwazi kwamba maneno yetu tunaposema yasiwe matamu na machungu, uchafu na usafi, baraka na laana. Jambo hilo liko wazi tu hapo, hayo ni mafundisho yenye afya nzuri tu hapo; ni mausia na kukemea kuhusiana na kuokolewa kwetu! Lakini kama nilivyotaja hapo juu, waalimu hao wanajaribu kutumia sura yoyote ile ya maandiko wanayoweza kuitumia, kisha kuipindisha na kuibadilisha, kisha kupanua maana yake halisi.

Yawezakana pia mahala pengine baadhi ya waandishi hawa wanaweza kumnukuu hata Yesu, pale anaposema, "…***Wabarikini wale wanaowalaani ninyi***" (Luka 6:28). Lakini katika mambo ambayo nimepata kusoma, sijaigundua hata sehemu moja ambapo waandishi hawa wanapelekea kutaja mistari hiyo pale wanapojaribu kuunga mkono mawazo yao kuhusiana na laana. Na yawezekana kuona kuwa ndiyo maana haishangazi, mafundisho hayo ya Yesu "hayapindi" kwa urahisi ili yafananishwe na mtindo wa mawazo yao. Yakobo anatueleza kuwa, anaona watu wanaendelea kulaani, wakati hawapaswi kufanya hivyo. Mafundisho hayo mapya yanasema kuwa eti ikiwa mtu bado anaendelea kulaani, kama vile Yakobo alivyosema, basi maisha ya wakristo yatadhurika kwa laana hiyo ya watu wengine. Lakini ***Yesu mwenyewe hasemi*** kuwa kama mtu atakulaani, basi *"uwe mwangalifu sana, yawezekana laana hiyo ikakupata. Unauhakika kuwa hujafanya dhambi? Maana unaweza ukawa tayari uko chini ya nguvu za laana katika maisha yako, na lazima uhakikishe kwamba unataka kutoka katika laana hiyo."* Hapana. Haiwi hivyo hata kidogo; kwa sababu hata kabla ya pale Kalvari, Yesu Kristo aliwaambia watu maana halisi ya kuishi kulingana na mapenzi ya Mungu na tabia yake. Yesu alisema, ***Ikiwa yeyote yule atawalaani, ninyi mbarikini***! – Amen! Kwisha! Hakuna zaidi ya hapo. Uwabariki tu! Hayo ndiyo mafundisho yake Yesu Kristo.

Yesu hawezi kutujaza akili zetu na mawazo ya kiushirikina na udanganyifu kuhusu mambo ya uovu yanayoweza kutujia ikiwa watu watatulaani. Hakuna lolote linaloweza kutudhuru iwapo tunafuata yaliyo mema (1 Petro 3:13). Hayo ni marejeo yaliyo adimu kuhusu laana katika Agano Jipya ambamo Yesu Kristo mwenyewe aliyatoa. Kwa hakika Biblia inacho kitu cha tofauti na cha muhimu inachoweza kutufundisha. Ni kumbukumbu za pekee ndani ya Agano Jipya ambazo hutuelekeza cha kufanya na kuelezea pia kwamba tabia zetu zinapaswa kuwaje pale mtu atakapotulaani! ***Sasa kwa nini basi walimu hawa wanayapinga na kuyakataa yale ambayo Yesu mwenyewe anayasema*** kuhusu njia ya kuifuata pale mtu atakapolaaniwa? Kwa nini basi wao hawayafundishi yale ambayo Yesu Kristo anayafundisha?

Hivyo ndivyo ilivyo katika Yakobo 3:7–10, na Ufunuo 22:3. Huo ndio "Ushuhuda" wao wanaoutumia kutoka katika Agano Jipya ili kuonyesha kwamba wakristo leo wanaweza kuwa na wamo katika vifungo, giza au magonjwa - eti hiyo yote ni kwa sababu ya laana zilizopita! Na jinsi gani tunapaswa kufuatilia au kugundua laana hizo zilizopita, ambapo inaweza kwa kufanya hivyo kutupeleka nyuma zaidi ya miaka mia moja iliyopita?

Mpendwa msomaji, unafikiriaje? Je, na wewe unaamini kuwa mistari hii inatufundisha mambo hayo wayasemayo? Je, hayo ndiyo mafundisho ya Yesu au Mitume? Je, unaweza kuyapata mafundisho hayo mahala popote pale katika Agano Jipya? Ni jambo la kufurahisha kuona kuwa, bila shaka kitabu maarufu sana na chenye kuvutia na kinavyoshabikia kasoro hizi hapa ulimwenguni pote, hakijaribu hata kidogo kutoa ushahidi wowote ule katika Agano Jipya ili kuunga mkono mafundisho hayo. Ingawaje yeye ananukuu mistari ile katika Yakobo ili kuonyesha uwezo uliomo katika maneno hayo, bado mwandishi hanukuu chochote kutoka Agano Jipya ili kuthibitisha mawazo hayo kwamba laana zilizopita zinaweza na zinafanya maumivu katika maisha ya watu wa Mungu. Tangu mwanzoni mwa kitabu na sura, anapojaribu kuyathibitisha mawazo yake ananukuu kutoka katika Agano la Kale. Kwa sehemu nyingine hiyo ni hekima kwa upande wake mradi tu kwamba haiungwi mkono na Agano Jipya. Lakini pia kwa upande mwingine inaashiria ukweli kwamba mafundisho hayo kumbe hayana maana yoyote ile katika Agano Jipya wala hayana maana yoyote ile kwa ajili ya kweli ambayo ndiyo Injili ya wokovu wetu; hasa kwa vile hayaungwi mkono na Agano Jipya. Anatumia maandiko ya Agano la Kale na kisha anayaumbia njia yake mwenyewe ili kuleta mafundisho dhaifu kabisa na yasiyo ya kibiblia, bali ni ya kiushirikina yanayoweza tu kupinga na kuidhalilisha Injili ya Kristo na ya kwamba yeye Yesu Kristo ndiye aliyesulubiwa.

Hii sasa inaondoa tatizo letu, tunapaswa na hasa tunatakiwa kuyakataa mafundisho hayo hasa kwa vile hayaungwi mkono kabisa na Agano Jipya. Na Yesu mwenyewe anatushauri kuachana nao walimu hawa wa kisasa, kama vile mtume Paulo anavyofanya katika Galatia 3. Lakini sasa kwa ajili ya faida ya wale walioshawishika na kunaswa katika mitego ya mafundisho pamoja na mivutano mingine ya waandishi hao, napenda niendelee hapa kuangalia mabishano hayo yao na madhara ya mafundisho ya aina hiyo. Lakini ni tumaini langu kuwa tutanufaika zaidi tunapopata msaada wa maelezo ya kibiblia kadiri tunavyoweza kuendelea kuainisha ukweli huu.

**Baadhi ya Madhara ya Mafundisho Hayo**

Ninawafahamu na kuwakumbuka marafiki zangu wa Kikristo huko Tanzania ambao kwa wakati fulani habari za laana kutoka kwa waganga wa kienyeji na hirizi za uovu zimewahi kuwekwa ndani au nyumbani mwao. Lakini, bila shaka yoyote ile, hilo halikuwa na uwezo wowote ule juu yao, haikuweza kuwagusa wao wala kuwaumiza na wao wameendelea kufurahia ndani ya Yesu Kristo Mwokozi wao na katika Ushindi wake na Amani ambayo Kristo amewapatia! Ni kweli kabisa! Ndiyo, tunaelewa kwamba yupo shetani na kuwa roho za uovu zinaweza kuwashawishi na kuumiza maisha ya hao wasioamini. Lakini kwa wale waliomo ndani ya Kristo, wao wamekombolewa kutokana na nguvu zote za giza, na wale wenye uovu hawawezi kuwagusa (Kol.1:22; 1Yoh.5:18) - wamekombolewa kwa damu ya Mwanakondoo! Bwana asifiwe! Ni ushirikina wa jinsi gani huo, na kuikataa Injili kwa namna gani huko, pale tunapoiweka kuwa, wale waliomo katika Kristo wanaweza kuumizwa kwa laana itokayo kwa watu wengine!

Lakini sasa hivi nimewahi kusikia toka kwa marafiki zangu toka katika nchi ile ile kwamba, eti kama utakuwa umejiumiza wakati unapolima shambani eti hiyo inaweza ikawa ni kwa sababu ya laana! Mafundisho ya jinsi hii yanapokelewa na kutumiwa bure tu pasipo hata kuyachunguza kwanza kulingana na maandiko ya Neno la Mungu. Kwa hiyo hupokelewa tu kutokana na sababu na maelekezo wanayopewa yatokanayo na aina zote za makosa na matatizo mabaya yanayojitokeza. Lakini sasa, mafundisho hayo hutoka kwa waandishi mashuhuri wanaojulikana sana kutoka huko magharibi. Kwa hiyo huwa ni rahisi sana kupokelewa na yeyote yule kisha kuyatumia katika kila hali iwayo kwa njia ambayo *inaweza kusababisha kuchanganya watu, kuwaletea hofu ya bure na maumivu ya moyo yasiyo ya lazima, na kisha kuwawekea watu mizigo mibaya migongoni mwao, ambayo wao hawawezi kuibeba*. Na hii haitokani kwamba watu wanakosea tu katika kuyatumia mafundisho mapya, kama tutakavyoona baadaye, njia zake halisi ambazo mafundisho hayo hufundishwa ndani ya vitabu vyao; *huwasababishia watu kujisikia kuwa ipo laana karibu katika kila jambo lao*.

Namfahamu mkristo mwingine ambaye alipata kuumwa, na Mchungaji wake akamwambia kuwa “Anaumwa kutokana na laana iliyopo juu yao”. Mchungaji huyo aliyajuaje hayo. Aliyajua hayo kwa sababu yeye aliwahi kuhudhuria katika moja ya semina maarufu siku hizi na ambazo watu hudhani kuwa ndiyo semina “zinazoweza kuleta mafundisho mazuri” na mafunzo kwa Mchungaji wa Afrika kutoka huko magharibi. Huko ndiko Mchungaji yule aliko yachukua mawazo yale, na ndivyo alivyoweza “kujua”. Hiyo ni elimu aliyoipata toka kwenye semina moja wapo kubwa, na yeye pasipo kuichunguza na kuichuja kulingana na maandiko kwanza yeye ameitumbukiza moja kwa moja katika matumizi kanisani mwake! Na kwa hiyo sasa, masikini mgonjwa huyo alipaswa sasa aishi akiwa na mawazo hayo ya kuwa alikuwa chini ya laana. Alizidi kutafunwa na hofu hiyo ya fikra za laana kwa muda mwingi. Aliombewa kwa muda usiopungua mwezi mzima ili kumwondoa kutoka katika laana hiyo, lakini pasipo mafanikio yoyote yale. Alipoanza kutibiwa kwa daktari huko hospitalini alipata nafuu. Hapa sisemi kuwa hatutakiwi kuombea wagonjwa kwa Bwana, la hasha; isipokuwa nasema tukio hili ambalo ni kati ya matukio mengi yanayodhihirisha uharibifu unaowaumiza watu kimwili, kiakili na kimawazo – ambako kunaweza kusababishwa na mafundisho hayo tusipoyaangalia vema.

Ni jambo la kushitua moyo wangu ninapoona kuwa watakatifu ambao wamekwishawekwa huru kutokana na nguvu za shetani na vishawishi vyake vya uchawi, waliofurahia uhuru na Kristo, kuona kuwa mpaka sasa, jinsi ambavyo *wamepata shaka na woga uliopandwa kwa upya ndani yao, wakibatizwa kama ilivyokuwa hapo nyuma ndani ya njia zao zile zile za kizamani za ushirikina*, *wakifikiria kuhusika na mila za kiuchawi, wakiwazia kwamba walikuwa katika vifungo vyao vilevile ambavyo walikuwa navyo hata kabla hawajaokolewa.* Na hayo yote yanawajia katika jina la mafunuo mapya ya “ukristo”! Mtume Paulo anaelezea katika hali ile ile ya kushangaza, anasema “Ninawaonea wivu kuwa mnamwacha haraka hivi yeye aliyewaiteni katika neema ya Kristo na kuikimbilia Injili nyingine; siyo tu kwamba ni nyingine, isipokuwa *wanajitokeza watu wengine ambao wanawatabisheni, na kuzuia Injili ya Kristo*”. Ni hali ya kutisha kwa jinsi gani huko kuwaingiza watu wa Mungu ili waone kwamba jambo lolote linapowaendea vibaya kwa njia yoyote ile katika maisha yao wafikirie na waone kuwa yawezekana ni nguvu fulani za giza za kutisha kutoka huko kale, ndizo zinazosababisha na kwamba zina nguvu juu yao! Mafundisho ya jinsi hiyo yanasababisha hasara

kwa maelfu na kuwaingiza watu katika vifungo na wala mafundisho hayo hayatokani na neema ya Injili ya Kristo au ukombozi wa ajabu ule unaopatikana ndani yake.

Nilikuwa nikihubiri sehemu fulani na baadaye mtu mmoja alinijia na kuniambia kuwa, huduma hiyo imegusa tatizo kubwa ambalo alikuwa nalo mtu huyu katika mwendo wa maisha yake ya kikristo. Kisha, mtu huyo akaniambia kuwa hakufahamu kama angeweza kufanya jambo lolote lile kuhusiana na tatizo lile, kwa sababu ni miezi michache tu iliyopita mtu mmoja aliwahi kumwambia kuwa tatizo lake hilo ***linaweza*** kuwa limetokana na laana iliyopita! Nilimfahamu mtu huyo, na palepale nikagundua jinsi gani mafundisho hayo ya kisasa yalivyomtafuna na kumdanganya kisha kumchanganya mtu huyu. Na kwa hakika kuwaacha watu wengi nje ya urithi wao wa ajabu katika huyo Kristo Yesu. Kwa vile hasa kasoro kubwa ya mafundisho hayo, hayashughulikii mizizi ya tatizo lenyewe; badala yake yanaendelea kuwaweka watu katika hali ya utumwa na pasipo ufumbuzi wa kudumu katika maisha yao. Kwa sababu katika maisha yake yote mtu huyu, anaendelea kutafuta na kubuni ili kujua ***ni aina gani*** za laana zinazotenda kazi kwake, ***ziko ngapi***, na zipo kutokana na historia ***ya muda gani*** mpaka sasa imekuwa ikitenda kazi ndani yake, na kujua ***iwapo kama*** tatizo lake hilo linatokana na laana hiyo – au sivyo! Hii sio kuwa naweka chumvi mambo, kama tutakavyoweza kuona hapo baadaye. Isipokuwa ni kutaka kuwaonyesha watu aina hii ya mduara kwa sababu mafundisho hayo yao, yenyewe tu huwasababishia watu kufikiri hivyo!

Ninaye rafiki mwingine aliyewahi kuyapokea mafundisho ya aina hiyo moyoni mwake, katika yeye huyo ni mkristo ambaye ana juhudi sana katika kumpendeza Bwana, na anapendelea kuishi maisha ambayo yatamshuhudia Yesu kwa watu wengine. Kwa hiyo kwa kawaida huwa anaumia sana anapoona kuwa anashindwa kumwakilisha Yesu ndani yake ipasavyo. Anapenda kuwa huru kutokana na tamaa zote za kimwili pamoja na tabia zake. Lakini ukamilifu wa mafanikio yake humpinga (pengine wengine wanaweza wakamtambua mtu huyo)! Ufumbuzi wake ni nini? Yeye alifuatilia vizazi vyake ili aone pengine kuna historia ya laana kwao katika miaka iliyopita? Kwa nini alifanya hivyo? Je, ni kwa sababu biblia inamwelekeza sehemu fulani kufanya hivyo? Kuna mahala popote pale katika biblia panapo mwelekeza afanye hivyo? Jibu ni Hapana. Kama ni hapana, Je labda Roho Mtakatifu anamhukumu kufanya hivyo au amemwonyesha kwamba lipo tatizo la huko nyuma linalomzuia? Jibu ni Hapana; isipokuwa yeye alikuwa akifanya hivyo kwa sababu aliwahi kuhudhuria moja ya mikutano ya walimu hawa wa kisasa, ambao wao kazi yao ni kuyaendeleza na kuyakuza mafundisho haya ya laana. Nao wao wananukuu kutoka katika kitabu cha Kutoka 20:5 sehemu ile ambayo Mungu anaelezea kuwa, “Anawapatiliza wana uovu wa baba zao hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao.” Na katika mafundisho hayo wanatuambia kuwa jambo hilo ni kubwa kiasi kwamba inawahusisha jamii kubwa ya watu, yaani baba yako na mama yako. Kila mmoja wao alikuwa na kipande chake cha wazazi wake na kila mmoja wa hao naye alikuwa na wazazi wake mwenyewe; na iwapo utafuatilia hilo hadi kufikia kizazi cha nne ndipo utapata matokeo ya watu 32 kuanzia pale kwenye uzao wa ukoo wako ulipotokea. Sasa, mwandishi moja anauliza katika kitabu chake ambacho ni maarufu sana kuwa, iwapo unaweza kweli kupata uhakika kama hakuna hata mmoja wao (wa 32) ambaye alipata kuhusika na aina yoyote ile ya uzinzi au ulozi; uhusiano wowote ule wa utambuzi katika maisha yao? Hivyo alikuwa anategemea labda agundue baadhi ya laana kutoka kwa mmoja wa baba zake waliokufa. Na hali hiyo ndiyo hasa ilikuwa inamkawiza na kumzuia kuingia katika haki ya urithi wake katika Kristo! Baada ya kusoma naye mtu huyo maandiko ya Neno la Mungu, ndipo alipata uwezo wa kufahamu kuwa mafundisho hayo aliyofundishwa hayakuwa na msingi wowote wa kibiblia. Baada ya kusoma mafundisho hayo ninaweza kuona jinsi mtu mmoja anavyoweza, sio tu kufanya yale yale ambayo yule rafiki yangu aliyafanya, bali hata namna ambavyo vitabu hivyo vyao kwa hakika vinavyoweza kukuongoza kuelekea katika aina hii ya mawazo na matendo.

Hebu sasa tuangalie mafundisho ya kisasa yanasemaje juu ya mambo ambayo yanapelekea watu kufikiri na kutenda kwa jinsi hiyo. Kwa nini basi hata tufanye utafiti wote huu kwa mambo ambayo hayana uhakika na yanayochanganya na kuleta woga tu na vifungo?

***Kwanza*** kabisa, *kwa mujibu wa mafundisho hayo*, ni nini dalili zake zinazoweza kuonesha kuwa laana inatenda kazi ndani ya maisha ya mtu?
***Pili***, tutawezaje kujua kwa uhakika kabisa kuwa laana imo kazini na kuitambua kwamba hiyo ni aina fulani ya laana.
***Tatu***, ni kwa jinsi gani laana inaweza kumdhuru mkirsto?

**1. Wanasemaje juu ya dalili kuonyesha kwamba laana inatenda kazi katika maisha ya mtu?**

Haya, wanashikilia *karibu kila tatizo* analoweza kuwa nalo mtu, kwamba linatokana na laana. Baadhi ya mambo muhimu ambayo huyataja katika orodha kama ifuatavyo: Kushindwa kwa akili na fikra, kuvunjika kwa

ndoa na matatizo mengineyo ya kifamilia; kurudiarudia mara kwa mara kwa magonjwa ya hatari; kuwa na uhitaji wa fedha, n.k.

Sasa, ijapokuwa imesemwa kuwa moja au mawili ya matatizo yanapotokea, sio lazima imaanishe kuwa hiyo ni laana inatenda kazi, lakini jinsi unavyopata matatizo zaidi, ndivyo ***uwezekano*** wa kuona kuwa laana inatenda kazi unaweza kuwa mkubwa - labda. *Hata hivyo, kama vile mtu mmoja asomapo vitabu hivyo, mara moja inamjia akilini mwake wazi kabisa kwamba aina yoyote ile ya matatizo au maradhi inaweza ikawa inatokana na laana.* Kukosekana kwa mafanikio katika biashara au katika maeneo yoyote yale ya maisha, hudhaniwa kuwa inaweza ikatokana na laana; halikadhalika ufukara katika jamii; ugumba, kuteswa, udhalimu na majonzi; kuhisi kushindwa, uasi wa watoto, kule kujisikia vizuri siku moja kisha siku nyingine kujiona taabuni, kukosa mafanikio halisi, kujihisi kuvurugwa, kukosa kwa uhakika kupata kile unachokitaka, … n.k, n.k. *Hayo yote hapo juu ni dalili za laana ambazo wao huzipata kutoka katika Kumb. ya torati sura ile ya 28, kisha huzitumia kwa wakristo leo*! Haya, kwao sio rahisi kulipata jambo ambalo hawajalijumuisha humo! Na wanaliandika kiasi kwamba linamfanya mtu asomaye ajisikie mara moja kwamba jambo lolote linalomtokea adhanie kuwa hiyo inatokana na laana iliyotangulia, ijapokuwa wao wanakubali kuwa sio kila jambo linaloweza kusababishwa na laana, lakini sio rahisi kwa msomaji wa vitabu vyao kuupata ufahamu huu. Mwandishi wao mmoja amewahi kuandika kuwa, Ijapokuwa sio kila tatizo linalompata mtu husababishwa na laana, hata hivyo,“ukweli” ni kwamba, *mara nyingi mkristo anahitaji ukombozi kutoka kwenye laana. Na anaisisitiza kauli yake hiyo kuwa ni ya kweli kwa mkristo yoyote yule hata yule aliyekua*, (kwamba anahitajika kupata ukombozi kutoka katika laana)! Hayo ni mawazo ya kiudanganyifu na hila kubwa, hasa pale tunapozingatia jinsi Yesu Kristo alivyoteseka na kufa kwa ajili ya hayo. Ndipo tunagundua kuwa kumbe basi huo ni uwongo mkubwa. ***Yapo mapungufu makubwa ya ulinganifu ndani ya mafundisho hayo, ambayo hayajaribu hata kidogo kutaja sababu zingine ambazo zinaweza kusababisha tatizo hilo***. Na hivyo ndiyo ilivyoandikwa ndani ya hivyo vitabu vyao maarufu sana. Havitoi hata maelezo yoyote kwa mfano: watueleze wazi basi ni jambo gani jingine linaloweza kusababishia shida katika ndoa, mbali na lile la laana!

**2. Lakini sasa tutajuaje “kwa hakika” kwamba ni laana inayotenda kazi ndani ya maisha yetu kulingana na mafundisho hayo?**

Ni maandiko gani katika Agano Jipya wanayorejeshea ili tupate kusaidiwa kujua kwa hakika kuwa laana inatenda kazi. Kwa hakika jambo muhimu kama hili linalohusu maisha ya watu mbalimbali lisielezwe kwa mtindo wa kubuni au la kutokuwa na uhakika. Ni muhimu sana jambo lihusikalo lisiachwe gizani – liwe wazi, na lazima tusimame juu ya misingi iliyo imara - kama vile ilivyo kwamba tunapenda kuomba kwa uhakika iwapo tunapenda kuona mafanikio.

***Haya hawatupeleki kwenye mistari yoyote ile ya Agano Jipya ili itusadie kutambua kwamba laana inatenda kazi katika maisha ya watu.*** Lakini sasa nitajuaje kwa uhakika kabisa wa kibiblia kwamba tatizo nililonalo linatokana na laana? Na kama sifahamu hivyo kwa hakika nitawezaje basi kuomba kwa nguvu na ujasiri kuipinga laana hiyo? Kwa misingi hiyo, kwa nini basi hawatupatii mifano yoyote ya Agano Jipya ya wakristo waliopata matatizo yao kutokana na laana. Au hata Yesu mwenyewe haelezi mfano wowote wa mtu aliyepata matatizo katika maisha yake kutokana na laana! ***Haipo kabisa mifano ya jinsi hiyo ndani ya Agano Jipya na hiyo ndiyo sababu wao hawawezi kutupatia.*** Kadhalika Yesu pamoja na mitume hawakueleza ndani ya Agano Jipya juu ya laana ya aina hiyo, bila shaka hawakufanya hivyo kwa sababu jambo lenyewe na muundo wa mawazo yake hautokani na mpango wa Mungu kwa wanadamu nyakati za leo. Vipi basi washindwe kuturudisha kwenye maandiko ya Agano Jipya yanayopaswa kutuelezea, namna ya kutambua kuwa laana sasa inatenda kazi katika maisha ya watu? ***Hawawezi kufanya hivyo kwa sababu mistari kama hiyo haipo kabisa.***

Kwa nini hawatupatii mifano yoyote ile kutoka katika nyaraka za mitume kwa watu wa Mungu, inaonyesha kwa jinsi gani laana ilivyokuwa ikisababisha matatizo katika maisha ya watu jinsi ilivyovunjwa. Hawawezi kufanya hivyo, kwa sababu hakuna hata mistari ya jinsi hiyo inayoendelea kuwepo, (bila shaka maeneo kama Efeso watu walikombolewa kutoka kwenye ushiriki wao wa mambo ya kishirikina na uchawi, Mtd. 19:9 na 8:9, lakini mifano hiyo inahusu watu kusikiliza Injili. Lakini katika sasa makala hii tunatilia maanani ile huduma ***kwa watu wa Mungu***). Walipokuwa wakiyaandikia makanisa na kuwaelezea matatizo mbalimbali katika makanisa au katika maisha ya mkristo mmoja mmoja, mitume hawakutaja au kuonyesha, ukiachilia mbali tu kule kufundisha kuwa matatizo yanaweza kutujia yakisababishwa na laana zilizotangulia; *jambo kama hili haliwaingii mitume akilini mwao*! Lakini kwao, kama inavyopaswa kuwa kwetu sisi kama watakatifu wa Mungu, wanaliona tatizo likiwalipo mahali pengine.

Mambo yote niliyoyasema hapo juu, yanahusu pia laana juu ya Taifa ambayo nayo imekwishaelezwa kwa undani sana katika makala yangu iliyotangulia. Lakini hebu nirudie kueleza tena hapa, kwamba hatupati hata

mstari mmoja ndani ya Agano Jipya, wala hakuna mafundisho au maandiko yoyote yale. Hakuna hata mstari mmoja unaoelekeza kuwa aina yoyote ya laana inazuia kazi za Mungu katika mji wowote ule, mkoa au hata nchi. Wala hakuna tatizo lolote lile linaloweza kuwa ni la kimkoa au kienyeji ambalo laweza kusemwa kuwa linatokana na laana. ***Wala Yesu au mitume hawakufundisha popote pale wala kuomba dhidi ya aina yoyote ile ya laana juu ya mji, mkoa au nchi.*** Kwa ujumla haijafundishwa hivyo wala kufanywa hivyo. Hawatusihi eti tuanze kuzitafuta laana za kitaifa au mkoa ili kuombea kufunguliwa dhidi yake. (Yalikuwepo mambo yaliyokuwa yanawahusisha Waisraeli katika Agano la Kale, lakini bado hiyo ni tofauti kabisa na inahusiana tu na Agano ambalo walikuwa nalo kati ya Mungu na Waisraeli katika Agano la Kale.)

Ni kwa jinsi gani vitabu hivyo vya kisasa vinaweza kutusaidia ili kupata uhakika wa kujua iwapo laana inafanya kazi katika maisha yetu? Hawajui, na wala Hawawezi! Kutokana na uzito wa tatizo mara zote wao hutumia lugha hii: "…Hii *inafanana* na…", "*Inaweza* kuwa ni….", "*Yawezekana* kuwa ni…", "*Kama unaamini* kuwa laana inakudhuru wewe…", "*Labda*…", "Unahitajika kwa makini sana kuzingatia kuwa….", "Lazima *uchunguze*…", "Unahitajika *ugundue*…". Na hata inatisha zaidi ya kumaanisha wanapotuambia kuwa eti Mungu hatuhukumu kwa ajili ya "ukweli" (kama walivyosema) kwamba mababu zetu walituletea laana juu yetu, isipokuwa badala yake Mungu atatutia hukumuni iwapo hatutayatumia yale ambayo ametupatia ili kuondoa kutoka katika laana. Je, hiyo ni sheria ya vifungo na udanganyifu wa jinsi gani ambao unawekwa juu ya watu wa Mungu!

Katika baadhi ya mistari mmojawapo wanaopendelea sana kuunukuu ni ule wa Mith.26: 2 ambao unatuelezea kwamba, "Laana haitokei pasipo sababu". Lakini hata hivyo, hilo ni wazi na ni rahisi tu, kwamba, kama ipo laana mahala fulani, basi ipo sababu ya kuwepo kwake. Lakini sasa, wao huutumia mstari huo vibaya ili kutufanya tufikirie kuwa mara zote linapotokea tatizo basi hiyo "*yaweza* kuwa ni laana". Na *kama wewe unaamini* kuwa hiyo ni "laana" basi hapo unalazimika kuitafuta kuona kama imetokea wapi hiyo laana. Hii ina maana kuwa utafute sababu zilizosababisha laana kuwepo! Mafundisho yao hayo hayatupatii chochote kile ili kutusaidia angalau kutambua kuona kama laana inatenda kazi katika maisha yetu; hii inawahimiza watu kuanza kufikiria labda yawezekana kuna laana inayotufuatia nyuma yetu na ya kila tukio baya! Jambo fulani linapoharibika, wao wanakutaka ufikiri kuwa, useme,"Oho! Mama yangu wee! Sijui hii inatokana na nini? Hakuna chochote kinachoweza kutokea pasipo sababu. Je, chanzo cha tatizo langu ni laana?" Kwa hiyo wanahimiza hiyo ya watu wa Mungu ijengeke na kutoamini na ushirikina mtupu.

Lakini tunaweza kuuliza tena, kuwa tunawezaje kujua kwa usahihi kabisa iwapo laana inatenda kazi katika maisha yetu? Na jibu lao kwa swali hilo ni kuwa, pale mwishoni, baada ya kuweka maanani yote, Roho Mtakatifu pekee ndiye anayeweza kutupatia ushahidi mtimilifu na dalili zake! Roho mwenyewe, eti lazima atatuonyesha! Hayo ndiyo majibu yao ya jumla. Hivyo ndivyo itupasavyo kufahamu kwa uhakika kwamba Roho Mtakatifu ndiye atakayetuonyesha, lakini hili linaweza likawa ni jambo linalonenwa tu. Aina zote za kutilia maanani pamoja na kweli yake yote inaweza ikashawishi kuona kwangu na hitimisho langu. Na kama ninalo tatizo binafsi ambalo ni la hatari sana, Je nitakuwa katika nafasi nzuri ya kumwezesha kupokea kutoka ufahamu wa kimbinguni kutoka kwa Roho Mtakatifu huyo? Je, hainibidi hapo kuanza kumtafuta mtu mwingine aliye na "karama" za Rohoni ili kuitambua laana (kama walivyosema)? Hii kwa hakika inashangaza sana! Kwa maana haiwezekani kuwa Roho wa Mungu anaweza kutuonyesha, ***kwanza, kwa sababu hakuna chochote cha jinsi hiyo kinachofundishwa ndani ya Agano Jipya.*** Pili, ni kwa sababu pia kwamba yeye anayeteseka kwa madhara hayo, amekwisha jenga moyoni mwake misingi ya kuamini kuwa hiyo ni laana inatenda kazi, hata inakuwa vigumu kumpa nafasi ya kusikiliza ushauri wa huyo Roho wa Mungu. Kwa hiyo, wewe au pengine mtu mwingine yeyote yule anakuonyesha hilo kwa dhahili kuwa laana ipo katika maisha yako, hapo ndipo unapohitajika kujaribu kugundua pia sababu ya kuwepo kwa laana hiyo, kwa kuwa pale unapogundua sababu ya kuwepo kwa laana, ndipo hapo utakapokuwa na haki ya kuchukua hatua sahihi dhidi ya laana hiyo!

***Ni ujinga ulioje wa makosa na kuchanganyikiwa, ambapo kunaweza tu kuwaingiza watu katika udanganyifu.*** Inaonyesha kuwa, hatuwezi kuishughulikia laana kwa usahihi zaidi pasipo ufahamu wa Roho Mtakatifu kutoka juu; ili kujua chanzo na sababu za laana hiyo kuwepo kwa mtu au jamii, kujua ilikotokea na ni aina gani ya laana hiyo itusumbuayo. Je, huo sio ukatili? Kuwaambia watu kuwa matatizo yenu yanayowapata yanatokana na laana, na hivyo ni juu yenu kugundua kwa njia ya maombi pamoja na vipawa vya mbinguni ili kuijua ilikotokea laana hiyo na nini hasa?

Wapendwa wasomaji wangu, hivyo ni vifungo vya ukatili mtupu na ni upuuzi. Haishangazi kuona kuwa watu niliowataja hapo juu ambao walijaribu kujishughulisha na laana zinazohusika, walitumbukia katika maumivu makali ya moyo na kuchanganyikiwa, wakizidi kutafuta, lakini hata hivyo kwa kweli wasifikie katika jambo lolote lile la Mungu; wakiomba, wakitafiti, wakichungulia ndani, wakitazama nyuma kwa vizazi vilivyopita, wakishangaa, wakijiuliza maswali mengi; wakiwataka wengine kuomba; wakiwaomba wengine kupokea

wakionacho wao, au kuzionyesha karama zao maalum za kutambua, wakijisikia kwa wakati fulani kama wanaondelea mbele, wakipata unafuu lakini hata hivyo hayo yote hayawi katika ule uhuru wa Kristo Yesu.

Sasa, ijapokuwa hivyo vitabu vyao vinatoa maombi ya kisasa ya kujiondoa kutoka katika laana, lakini papo hapo bado wanaendelea kuwafundisha watu jinsi ambavyo wanapaswa kuitambua laana na vyanzo vyake kwanza. Sasa, nasemea nini hasa hapa, siweki chumvi zaidi ya yoyote ile. Kwa kweli tunaweza kupata mfano halisi wa moja ya maisha kutoka kwa moja ya vitabu vyao wenyewe vinavyoelezea habari za laana; inatupatia moja ya maelezo hayo pia yanatupatia moja ya mifano mizuri sana hata kupelekea makala hii kuandikwa. Hebu basi sasa niitaje iwapo nitaweza kuilezea ipasavyo ushuhuda wa mtu mmoja ambaye kwa miaka mingi amekuwa na kuheshimiwa sana kuwa ni mtu ambaye amekomaa katika Bwana na anahusika katika huduma, yeye huyo zaidi ya miaka 20 amekuwa akisema kuwa anaona maumivu makali katika sehemu fulani ya mwili wake, mume wake na mama huyu ambaye alikuwa akijishughulisha na huduma ya Mungu kimataifa kwa miaka mingi, na ndiye ambaye amekiandika kitabu kile kinachonunuliwa sana siku hizi kihusucho laana. Yeye mara moja *aliamini* kuwa maumivu ya mkewe yalitokana na laana; akaomba naye na maumivu yake yakapata kupungua na mkewe *alifikiri* kuwa *yawezekana* huo ukawa ndio mwisho wa tukio hilo la ugonjwa wake. Lakini baadaye baada ya miaka kadhaa, mama huyo alipata tatizo zaidi katika eneo lile lile la maumivu ya kwanza, hapo sasa akahitaji msaada wa kidaktari. Mama huyo sasa, anaandika katika kitabu hicho kuwa, *ilionekana* kuwa kulikuwa bado kuna laana katika mwili wake na inawezekana kuwa hata katika maisha yake. Anazidi kutuambia kuwa kwa muda wa kuandika kitabu chao hicho, yeye alikuwa bado anasumbuliwa na afya yake. Tunaambiwa kuwa katika muda huo, Roho Mtakatifu alifunua aina nyingi sana za laana kutoka katika maisha yake yeye mwenyewe na maisha ya mababu zake. Yeye pamoja na mumewe walifanikiwa kuwapata wakristo wengi sana ili kuomba kwa ajili ya jambo hili, hapo pia walipata kupewa "maelekezo" ya ki-mungu kupitia neno la maarifa. Hata hivyo yeye mwenyewe anakiri kwamba kuzikataa laana hizo zote imemchukua muda mwingi, na kisha baadaye katika kitabu hicho chao, tunaambiwa kuwa vita kuhusu laana bado inaendelea kadiri anavyoendelea kuomba ili kufunguliwa akiwa pamoja na mumewe wakiyatumia maandiko mara nyingi kwa siku ili kutangaza uhuru wao kutokana na laana!

Hatupaswi kushangazwa kuona baadhi ya ndugu zetu wa kiafrika wanaotuhusu wakififikiria kwamba wanarudishwa nyuma kwenye mila na desturi za kiuchawi, za woga, za kutokuwa na uhakika wa hirizi na hiyo inaloga dhidi ya laana! Ni huzuni iliyoje hii wapendwa wangu! Hasa tuonapo kuwa watu waliokomaa kiroho wakidanganywa hivyo na yule shetani na wakitumbukizwa ndani ya vifungo vya aina hii ya mawazo ya ushirikina na maombezi yasiyo na maana. ***Hapa tunaona wazi kuwa, hata mafundisho yao wao wenyewe yanashindwa kuwaleta watu katika baraka za Mungu na Uhuru wakati ambapo tatizo lao bado linaendelea kuwepo ndani ya maisha yao***, hapo kwa haraka tu wanaamini kuwa laana bado inaendelea kuwepo na kuwakalia, pia wanaachwa wakiwa wamejazwa mawazo hayo ambayo hayana misingi ya kibiblia na yasiyotambulikana kwamba ***eti "laana" inaendelea kuwakalia juu yao kwa miaka mingi***.

Mambo hayo yananihuzunisha na kuniumiza sana. Hivi mtu ataaminije mambo ya jinsi hiyo? Siziandiki habari hizi ili tu kuwalaumu wengine, hapana; au kwa sababu ninahusika kwa kiasi kwa mafundisho yaliyo sahihi, hapana - hata kidogo. Isipokuwa mimi ninayaandika haya yote kwa sababu, nawaona watu ninaowajua na kuwapenda wameathirika kwa mawazo hayo yao, na zaidi ya yote imewasababishia kuchanganyikiwa, kudanganywa na kupata maumivu ya moyo. Watu wa Mungu wanatumbukizwa katika utata usioisha na kuchanganyikiwa na udanganyifu mkubwa kama tulivyo soma habari zake hapo juu. Na sasa baadhi yao wameniomba niweke katika maandishi mambo haya ambayo nimekuwa nikihudumia kwao. Ni kweli kuwa inaumiza sana, kuona watu wakiporwa ile kweli yao kama ilivyo ndani ya Kristo; Inaumiza pia kuona Injili ikishambuliwa na kuchafuliwa namna hiyo, Kristo amefanya mambo mengi, na ametuleta katika mambo mema zaidi ya hayo yanayotambuliwa na mafundisho yao ya kisasa; mbaya zaidi walimu hawa wa kisasa wanatutumbukiza katika giza nene na vifungo ambavyo havikupangwa na Mungu vitujie.

***Kwa hiyo, habari hii inaelezea maeneo ya makosa ambayo mafundisho hayo yamewatumbukiza watu ndani yake.***

***Kwanza kabisa***, tunaona kuwa tatizo lolote lile liwe baya au siyo baya wao hulitafsiri ***kiurahisi*** kuwa linatokana na laana. Kwa maneno mengine, wale watu ambao tayari huyapokea mafundisho hayo ndani ya mioyo yao, wapo tayari kabisa kuona na kusadiki kuwa laana ndiyo inayosukuma matatizo nyuma yao ndani ya maisha yao. Kama uonavyo mwandishi wao mwenyewe akifanya pale anapolijadili suala la mkewe ndani ya kitabu chao. Na kwa hakika, kadiri tukio linavyochukuliwa kwa hatari zaidi kwamba linatokana na laana nyingi isiyo na mwisho. Kadiri watu wanavyoendelea kuteremka chini huku wakififikiria, hawatoi nafasi ya kufikiri kuwa labda tatizo lao linatokana na jambo lingine ambalo sio laana. Hawana nafasi ya kufikiri hivyo, na kama tatizo lile linaendelea kudumu kwa miaka mingi ndipo hapo wanapoamini kuwa hayo yote yanatokea hivyo kwa vile bado hawajazigundua laana zote zinazofanya kazi ndani ya maisha yao. Hivyo

wanaendelea kutafuta zaidi kutoka kwenye mambo yaliyopita ili kuona kama wanaweza kuona, wanaweza kugundua uwezekano wa kuwepo kwa laana.

*Jambo hili linafungulia hofu na kuwakusanyia watu mawazo ya kiushirikina katika mioyo yao na maisha yao*; matendo ambayo yanapishana sana na tumaini tuliloitiwa katika Yesu la Amani na furaha ambayo ndiyo urithi wetu katika Kristo, ambaye yeye ametukomboa kutokana na nguvu zote za shetani za kutoka katika roho za vifungo ambazo ndizo zinazoleta hofu. Haya ni maisha ya jinsi gani ambayo tunayachagua kuishi? Ya kwamba kila mara mtu awe na habari mbaya tu na matatizo ambayo yanakupelekea kuwazia kuwa yawezekana kuna nguvu za giza au hukumu fulani, zilizopita zinazoshambulia maisha yako. Kwa nini mtu uliyekombolewa ubakie katika hali ya woga, mashaka, hofu na vifananavyo na hayo?

***Jambo la pili ni hili***: kwa kuwa ukweli wa Biblia pamoja na maelekezo yake na miongozo yake *inakataliwa kuaminika* katika mioyo yao; basi sasa roho ya mtu huyu inatumbukia pasipo kuepukika katika hali ya kazi za ubunifu na kukisiakisia kusikoisha kadiri anavyoendelea kugundua tabia au chanzo cha laana hiyo. Kwa sababu haupo mfano wowote ule wa kiroho au mafundisho kwa ajili ya hali hii ya kuendelea, hapo sasa ndipo mtu huyo anajifanya mateka ya Shetani. Katika dhana na mafunuo yake binafsi tu kuhusiana na Roho; hapo haijalishi hayo ni yake yeye mwenyewe au kutoka kwa mtu mwingine. Hatari kubwa inayoweza kutokea hapo ni hii, kwa kuwa wanalikataa Neno lake Mungu juu ya jambo hili, na kwa sababu sasa wanachagua kuyaamini mawazo yasiyolingana na Injili, ***kwa hiyo basi wanajikuta wametumbukizwa wao wenyewe kwenye maroho ya udanganyifu pale*** wanapozidi kutafuta na kuyasubiria majibu kupitia dhana zao wenyewe na "karama za Roho", kama wanavyoamini. Mambo yao hawayajengi juu ya msingi wa Neno la Mungu, bali wao huamini uongo na hivyo matokeo yake hujikuta kuwa wao wamekuwa ni mateka ya maroho yadanganyayo. Roho hizo huweza tu kuimarisha na kuwathibitisha katika udanganyifu wao, hila yao, hatimaye zikiwaachia kila aina ya "kujisikia dhana na mafunuo" na mishituko ya mwili. Ndipo hapo mmoja ananaswa katika mzunguko huu wa kutisha wa "baraka" na "laana" kama vile katika habari ya kuhuzunisha ya hapo juu. Zaidi ya yote, katika habari hii tumeambiwa kuwa katika kipindi hiki kirefu, Roho Mtakatifu, yeye kwa kutumia uvumilivu mkubwa na ukamilifu wake, alijifunua kwake ili kuona chanzo cha laana hizo hatua kwa hatua na inaonekana wazi kuwa bado mwendo huo ulikuwa unaendelea.

Ndivyo; mambo haya ni ya hatari sana ndiyo sababu na mimi sipendi kuyaelezea kijujuu tu, kwa kuwa kile kilicho kuwa kinatokea hapa, kinapatikana pia katika 2Kor 11: Ni hila za shetani tu. Watu wa Mungu wanauacha ule wepesi wenye nguvu za ajabu uliomo ndani ya Kristo; wanaliacha Neno lake na kuyafuata mambo mengine yasiyo na uhai wowote, ambayo mwisho wake watu hao huangukia katika shida ya kumpokea Yesu mwingine; Injili nyingine na roho nyingine; na hayo yanatokea leo kwa watu wengi wa Mungu, vilevile kama ilivyokuwa nyakati zile za Agano Jipya. Ndiyo, ni sawa kuwa wao ni watu wa Mungu, lakini hila imewaingilia na kuwakalia.

***Jambo la tatu*** nalo ni hili kwamba; habari inaelezea kwa uwazi kabisa kuwa, mafundisho hayo hayawahusu tu watu wasiookolewa, au hata kwa wale wanaotaka kupokea msaada wa wokovu au kwa wale ambao kwa hakika hawajawahi kuelewa kwa uhakika utata wa Injili, au kwa wale wakristo wanaoishi pasipo kujijali na ambao pengine wanahusika na mambo yasiyo ya ukweli. Hapana; kwa vyovyote vile haijaweka mipaka kwa watu wa aina hiyo pekee; kinyume chake, habari hii inaweka uwazi usio na ukomo, wanataka ufahamu kuwa kwamba *kila mkristo* anaweza akawa na yawezekana ameathirika kwa aina fulani ya laana iliyopita; hapo unaweza ukawa wewe ni mtu uliyekua kiroho, mwenye miaka mingi, unaweza ukawa ni mkristo uliyekuwa mwenye uzoefu mkubwa wa maisha ya kiroho, hata ukawa unatumika katika huduma kubwa ya Mungu kimataifa na mwenye juhudi ya kuishi maisha matakatifu na mwisho wake pamoja na hayo yote eti wao wanadai kuwa bado laana za kale zinaweza kukuletea huzunimwilini mwako, inaweza kukuletea matatizo na vifungo ndani ya maisha yako kiroho na shida katika mazingira yako! Aha! ni ushirikina uliokithiri huo. Hiyo ni kuukana uwezo wa Injili katika maisha ya watakatifu kwa jinsi gani huko? Ni kujirudisha nyuma katika fikra za kiuchawi kwa jinsi gani huko? Kule tu kuyaamini mafundisho hayo yao ni tendo la zaidi ya laana kuliko kitu kingine chochote kile. Kwa maana ya kwamba, mafundisho hayo yanawabana watakatifu na kisha kuwatumbukiza katika giza nene na vifungo. Hii sasa inakuleta kwenye mtazamo wetu wa tatu.

**3. Je, dhambi au laana kutoka kwa mababu zetu inaweza ikawadhuru watu wa Mungu, yaani, wale waliomo ndani ya Kristo?**

Hivyo ndivyo kwa hakika wanavyofikiri hao waandishi wa kisasa. Ndani ya moja ya vitabu vyao vya hivi karibuni, kinaeleza kwamba, shetani anatumia dhambi za vizazi vilivyopita zaidi kuliko hata kitu kingine chochote kile katika kuwatesa wakristo na kanisa pamoja na kuitesa miji na nchi. Huo ni upotoshaji wa fikra za kiroho na siasa tupu za kidini. Ijapokuwa haupo hata mstari mmoja wa Agano Jipya unaounga mkono hoja hiyo, bado mafundisho hayo ya udanganyifu yanazidi kusambaa na kuhofisha umati mkubwa wa watu wa

Mungu. (Lakini kwa vyovyote vile mafundisho hayo yanawezesha kumfanya mtu aone kuwa laana ndiyo isumbuayo karibu kila nyuma ya tatizo linapomjia au shida inapomjia, katika maisha yake). Yawezekanaje kuwa hivyo? Haya, bado hicho kitabu chao kinazidi kusema kuwa, eti dhambi ambazo mababu zetu hawakusamehewa (ambazo walikufa nazo) *zinazo uhalali wa kisheria leo kuwadhuru na kuwatesa wakristo*, eti bado sisi leo tunaendea kuvuna madhara ya dhambi za mababu zetu ambazo wao hawakuzitubia! Huo ni uwongo mweusi, ni sumu ya fikra kwa wakristo ikiwa wataamini hivyo. Watu hao wananukuu maandiko ya Agano la Kale, *kujaribu* kuunga mkono na kuyajengea hoja mafundisho yao na mawazo yao yanayoipinga Injili ya Yesu Kristo wanaupenda ule mstari unaotumiwa katika Kut. 20:5 pamoja na habari nyingine zinazofanana na hapo ambazo tutaziangalia hapo baadaye.

Inaendelea kusema kuwa, pana tofauti kati ya (msamaha na ghofira au uradhi) kwa hiyo wanaendelea kudai kuwa, Mungu anapotusamehe anakuwa anatuosha kutokana na hatia ya dhambi, lakini dhambi zile ambazo mababu zetu hawakuzitubia au kusamehewa, ambazo hazikuoshwa katika damu, hizo hazina uradhi wa Mungu kwetu sisi. Ina maana watu hawa *wanataka kutueleza kuwa, adhabu ya dhambi hizo za mababu bado ina nguvu na inaweza kutuletea magonjwa sisi leo au kutudhuru na kutuharibu hata kizazi cha nne*! Inaniumiza sana, hata kutamkia udanganyifu huo wa kutisha na wenye kutuletea madhara na hila ambayo inalenga kuangamiza ukweli wa Injili. Lakini, tazama sasa; tumo katika Agano Jipya, tumezaliwa katika Roho wa Mungu, na tumeoshwa kwa damu ya Mwanakondoo wa Mungu. Hivyo basi, hayo wanayotuelezea yatawezekanaje! Dhambi za vizazi vilivyopita zawezaje leo kumdhuru mkristo? Kitabu kimoja cha kisasa kinauliza swali hili kuwa, “Dhambi za vizazi vilivyopita (za mababu) zawezaje leo kumdhuru Mkristo?” Na wao (waalimu hawa wa kisasa) wanatupatia jibu gani kwa swali hilo hapo juu? Haya, wao wanajibu kwa kusema kuwa eti hilo ni *fumbo*!! Wanasema kuwa ***hawawezi kulielezea*** kwa ufasaha, kwa nini wakristo leo - hata wale watakatifu na waliojitoa kwa Mungu - wanaweza kuteseka kwa madhara na adhabu zitokanazo na dhambi hizo za mababu!
Hapa, kwa ujumla wanataka kusema kuwa hawawezi kusimulia kwa makini kwa nini msalaba wa Kristo Yesu hauwezi kukatilia mbali madhara yote ya laana hizo, pale mtu anapotubu na kuwa amezaliwa upya. Hivyo ndivyo wanavyokusudia kutuambia! Mafundisho yao hayo yenye kuogofya na kutisha yamekaa kwenye misingi ya “fumbo”, kwa maneno mengine yamekaa katika jambo lingine ambalo Mungu hajalifunua na juu ya kitu ambacho hakielezeki!
Wanasema kwamba *inaonekana* kwa sababu ya sheria za Mungu, basi baadhi ya dhambi za mababu zinaweza kuharibu maisha ya wakirsto - haijalishi kama wewe unaweza kuishi maisha ya utakatifu kiasi gani - mpaka pale tu dhambi hizo au laana hizo zitakapogundulika na kuombewa maombi maalum. Na kwa jinsi gani basi laana hizo zitaweza kutambulika na, unajuaje basi kama ni laana itendayo kazi na tena inatoka wapi? Haya, wanasema eti kwa njia ya Roho watatambua. Nilivyokwisha sema hapo nyuma kuwa mambo hayo yao yote yanahusika sana na aina ya ushirikina na matendo ya kimafumbo ya kiunajimu, kuliko ukombozi wetu katika Kristo. Hii inaharibu ufahamu wa Mungu ndani ya watu ambao Yesu aliwafia ili kuwapa (2 Kor.4:6). Ijapokuwa kwa makosa na udanganyifu, lakini mwandishi wa kitabu hicho chao cha hivi karibuni, angalau ni mwaminifu kidogo, zaidi kuliko vitabu vile vingine vinavyojaribu kuonyesha misingi ya kibiblia kwa mafundisho hayo yaliyokosewa.

**Wagalatia sura ya tatu (3)**

Sasa tunafikia katika sura ya muhimu katika waraka kwa Wagalatia – ile sura ya tatu. Mstari wa 13 unatufundisha kwamba “tumekombolewa kutoka katika laana ya sheria”. Je, tuuonapo mstari huu wa Biblia, tunahaja ya kusema zaidi juu ya laana? Je, hawa walimu wa kisasa wanautafsirije mstari huu? Sawa, wao wanakubali kwa maelezo yao ya wazi kwamba, kazi ya Kristo pale Kalvari, imekamilika, naye Yesu amesababisha msamaha wa dhambi zetu zote na kwamba ametukomboa kutoka katika nguvu za shetani. Ni ukombozi kamili, nasi tunaweza kuwa huru kutokana na makosa na uweza wa dhambi ikichanganywa na laana. Hivyo ndiyo ajabu. Lakini pia wao *wanaendelea* kueleza kwamba eti hayo yote hayawezi kumtokea mtu wakati wa kuokolewa kwake. Ni sawa, ikiwa umeokoka ya kwamba Mungu anakusamehe dhambi na wewe mwenyewe pia, kisha anakukomboa kutokana na nguvu za shetani pale unapokuwa umeokolewa kwa neema yake – lakini eti wanadai kuwa - ile laana itokanayo na kutosamehewa kwa dhambi za mababu zetu, hudhuru, huzuia na kuharibu maisha yako! Inaweza eti ikasababisha kuvunjika kwa ndoa, ajali na kifo katika maisha yako!!Ni udanganyifu na uongo mwingine mno. Ni siasa tupu za kidini ambazo hazina nafasi ya kuokoa mtu! Wanasema, wokovu wako haujakamilika pale katika kuokolewa kwako, yaani siku ile ulipotubu dhambi zako na ukamrudia Mungu, eti kwa sababu tendo hilo la kutubu tu, haliwezi kusimamisha madhara ya dhambi za mababu zetu ili yasikuharibu wewe! Wala eti kifo cha Kristo pale Kalvari hakiwezi kusababisha ukombozi wako kutokana na adhabu au madhara ya dhambi iwapo wewe umeokolewa na kuzaliwa upya! Hayo ni mafundisho yenye ndimi zenye sumu ya fira kwa watu wa Mungu. Hayo ni mafundisho na mafunuo ya shetani yakilenga kuwarudisha watu wa Mungu utumwani upya! Jihadhari nayo! Hivyo ndivyo wanavyopita huko na huko, wakikusanya umati wa watu wengi na kutufundisha hayo! Hivyo ndivyo wanavyotutaka

tuwaamini! Na kwa hakika hivyo ndivyo vitu walivyonavyo mioyoni mwao wakilenga kuhalalisha madanganyo yao kwetu. Sasa, tunapataje basi kukombolewa kutoka katika laana? Haya, baada ya mtu kuokolewa na kadiri matatizo yanavyozidi kutusonga na ugumu kutokea kwa miaka mingi, tunaweza tukagundua ni aina gani ya laana iliyopo, ili kwamba tuweze kuishughulikia ipasavyo kwa njia ya msalaba.

Kwa hiyo ujumbe kwamba "Kristo ndiye yeye pekee aliyesulubiwa" hautoshi kuishughulikia dhambi na hukumu siku ile tunapotubu na kumgeukia Mungu kwa imani na kwa kazi yake timilifu pale Kalvari. Njia mpya iliyo katika uhuru kamili, wanasema kuwa ni Kristo ***pamoja na*** kutambua na kugundua hali halisi ya laana iliyopita kupitia karama za kiroho! Hivyo ndiyo ni aina halisi ya kasoro ambayo Mtume Paulo alikuwa akishindana nayo dhidi ya makanisa ya kule Galatia; ili kuleta wokovu kamili. "Kristo na kuwa yeye ndiye aliyesulubiwa" eti hiyo haitoshi; unahitaji kupata kitu kingine tena cha zaidi, na hicho kitu kingine chenyewe kimekaa katika misingi ya Agano la Kale! Katika Galatia watu wengine walifundisha kwamba, kutahiriwa ni *nyongeza ya lazima* sana katika kumwamini Kristo kwa ajili ya kupata wokovu halisi. Na leo, hawa waandishi wa kisasa wanawaandikia watu kuwa, haja ya kutambua na kugundua laana zilizopita kupitia karama za rohoni na utambuzi hivyo ni vitu vya *nyongeza ya lazima* katika kumwamini Yesu – iwapo utahitaji kuanza kuingia katika uhusiano wako kama mwana wa Mungu. Wanafundisha kuwa, wewe hutahukumiwa kwa ajili ya dhambi za mababu, ***isipokuwa utahukumiwa pale unaposhindwa kuzitambua na kuzishughulikia laana zile*** ambazo ni matokeo ya dhambi zao! Huu ni udanganyifu wenye ukatili wa hali ya juu wanafanya hivyo ili kutafuta kuhalalisha wingi wa kasoro zao hizo kwa kutumia Kut. 20:5 na Kumb.28: 48. Kwa hiyo sasa mtu atalazimika kuyapokea na kuyaamini mafundisho yao hayo mapya, ambayo hayamo kabisa katika Agano Jipya – isipokuwa kimsingi mafundisho yenyewe yamesimama sehemu hizo mbili tu za Agano la Kale ambayo inahusisha hukumu ya Mungu chini ya Agano la Kale.

Hebu niseme tena hapa kwamba iwapo itatokea mtu yeyote yule, akajihusisha mwenyewe katika mambo haya ya fumbo za kiunajimu, uchawi au vyovyote vile wote hao wanakuwa wanatenda dhambi na kumpa shetani uwezo mkubwa dhidi ya maisha yao hata kama wao sio waamini au ni wakristo. Hatutakiwi kufanya chochote kile katika mambo hayo. Mungu ametuita ili tuachane na mambo hayo tuishi katika utakatifu. Hali kadhalika iwapo mtu mmoja kwa namna fulani amempokea Yesu Kristo, naye akaona mambo haya hayamwathiri chochote kile, naye amejihusisha nayo au anaendelea kujihusisha nayo, ndipo kwa vyovyote vile kwa mtu kama huyo yatahitajika maelekezo zaidi na ushauri, bila shaka hawajaisikia Injili kwa hakika au kuielewa ipasavyo, na hivyo itawawia vigumu wao kunufaika kutokana na nguvu zake ndani ya maisha. Watu wote wa aina hiyo wanahitajika kupata ushauri na huduma ya ukombozi kutokana na aina yoyote ile ya ubaya waliohusika nao. Lakini katika hali ya makosa hayo yote, njia sahihi ya uhuru wetu ni kupitia toba ya kweli na imani ya kweli katika kazi ya Kristo pale Kalvari. Njia hii ndiyo ivunjayo nguvu za kila laana! Haleluya!

Lakini tunachokitilia maanani ndani ya makala hii hapa ni ushauri na mafundisho ambayo wanapaswa kupewa wale ambao wanayaelewa mambo hayo na kisha wanapenda kuishi katika hayo. Wakiwa ni watu waliozaliwa upya, siyo kwa mbegu iharibikayo bali isiyoharibika, lakini sasa, waandishi hao wanayafanya mafundisho haya yawahusu wakristo wote pasipo kujali kukua kwao au utakatifu wao. Ni jambo moja tu ambalo linapaswa kusema kuwa, watu wengine wanahitaji ukombozi kutokana na ushawishi wa laana pale wanapomrudia Bwana, jambo ambalo kwa ujumla wake ninalikubali. Lakini ni jambo la tofauti sana kufundisha watu kwamba, wale ambao sasa wamo ndani ya Kristo wanaathirika na kuzuiwa katika maisha yao kwa laana iliyopita tangu miaka mia moja iliyopita! Na moja ya kasoro yao kubwa ni kwamba wanaifanya laana kuwa ndiyo chanzo cha kiroho pamoja na matatizo mengineyo, au wanaiona ndiyo kizuizi cha kupokea urithi wetu katika Kristo - inatuweka nje ya uhuru na wokovu wetu uliomo ndani yake Yesu Kristo. Wakati ambapo Agano Jipya lenyewe linazitambua sababu zinavyoonekana katika sehemu fulani humo kwa mfano: kuwa katika tabia ya kimwili, au ya dhambi, katika kukosa toba au kukosa imani katika Kristo pamoja na kazi yake iliyofanyika pale Kalvari. Hayo ndiyo mambo yanayoweza kuleta vizuizi kwa mtu.

**Ni Laana ya Mungu**

Hebu sasa tutazame vema, ni laana *ipi* inayoongelewa katika Galatia sura ile ya tatu (3). Ni wazi kuwa hiyo ni laana ambayo Mungu aliiweka kupitia sheria, na hii inakubalika na waandishi hao. *Siyo* kwamba hiyo ni laana ya shetani au mtu, aliyeiweka. Hilo pia wanalikubali kwa sababu ya Kalvari, Mungu anatusamehe dhambi zetu zote tunapotubu na kuamini, na kwamba sasa, kwa kupitia Kalvari tumekombolewa ipasavyo; kutoka katika nguvu ya dhambi, nguvu ya shetani na tumewekwa huru kutokana na kulaumiwa. Lakini hata hivyo, ijapokuwa Mungu hutusafisha dhambi zetu zote na hukumu iliyotupasa huiondoa, wao bado wanafundisha kwamba, Kalvari haishughulikii hukumu inayotokana na kutosamehewa dhambi zisizosamehewa au kuungama mababu zetu kama tulivyo ona hapo juu, eti hilo halifanywi pale Kalvari wakati tunapookolewa! Hukumu tuliyokuwa tunastahili kupewa inaondolewa pale tulipo mwamini Kristo. Hata hivyo ile hukumu

ambayo ilikuwa inapaswa kutokana na dhambi za mababu zetu inaendelea kuwepo hata baada ya wokovu wetu na Kalvari haiwezi au haishughulikii jambo hilo hadi pale utakapo litambua tatizo katika maisha yako na kuamua kuwa hiyo inatokana na laana ile itokanayo na yote mawili, kwamba ile itokanayo na madhara ya dhambi za mababu au ile isababishwayo na tatizo lako. Hapo ndipo mtu anaweza kuitumia faida itokanayo na msalaba. Watu hawa wanazidi kufundisha kwamba eti, *laana hizo zinazidi kutufuatilia hata baada ya wokovu wetu*, *kwa sababu eti kifo cha Yesu pale msalabani hakikutosha kushughulikia tatizo la dhambi za mababu zetu*, pale tunapotubu na kumgeukia Bwana. Na kwa sababu ya hilo, kadhalika wala halikuweza kutosha kuzishughulikia hukumu zitokanazo na dhambi hizo – sio tu kwamba mpaka mtu awe amekwisha kuzitambua na kuungama katika maisha yake, ha kuutumia msalaba katika dhambi hizo! Wanasema kuwa dhambi hizi za mababu pamoja na madhara yake yanaweza tu mwishowe kushughulikiwa ipasavyo (kwa toleo lihusulo) kwa uwezo wako kuzigundua na kuzitambua katika maisha yako. Ndivyo wasemavyo watu hawa. *Na hilo ni kosa la kutisha na upotoshaji uliokomaa*! Ijapokuwa inaeleweka wazi kabisa kuwa hiyo ni laana *ya Mungu mwenyewe* kupitia *sheria*, na ijapokuwa Mungu huyo alimtuma mwanae ili aweze *kutukomboa kutoka katika laana ya sheria*, lakini sasa bado waandishi hawa wanang'ang'ania kuwa kifo cha mwanaye Mungu kinamruhusu Mungu kukusamehe dhambi zako binafsi, lakini eti Mungu ***anaruhusu*** (?) madhara ya dhambi za mababu kukutesa wewe kwa vile hazijaungamwa! Au kusameheka! Kwa kweli wanafundisha kwamba, laana ya Mungu mwenyewe haikuinuliwa pale Kalvari na yeye mwenyewe! Kwa maneno mengine wanataka kusema kwamba Mungu atatusamehe kwa ajili ya dhambi zetu tu, *lakini bado laana ya Mungu inakukalia eti kwa sababu ya dhambi zisizotubiwa za mababu zetu*! Yawezekana hivyo kuwa ni kweli? Lakini sasa, kama ni hivyo, kwa nini basi Yesu Kristo alikufa msalabani kuzichukua dhambi za ulimwengu pamoja na madhara yake. Kwa hiyo hayo mafundisho yao, ***yanatufanya tubebe madhara ya dhambi za mababu zetu***. Mafundisho hayo yanapingana kabisa na Neno la Mungu katika Ezekiel 18:20, Jeremia 31: 29,30, halikadhalika yanapingana na moyo halisi wa Injili yetu. Na ni kuwapa watu mzigo usiobebeka, yanapingana kabisa na kile alichokifanya Yesu Kalvari kwa ajili yetu.

Mungu alisema, atafanya Agano ***Jipya*** na chini ya Agano hilo, atatangaza kuwa, dhambi zetu na uchafu wetu *hatazikumbuka tena*! Yeremia 31:34; Heb. 8:12; 10:7; lakini sasa hawa waandishi wa kisasa wanalibadili Agano la Mungu kwa kusema kuwa "… Aha, sawa; Mungu hazikumbuki tena dhambi *zako* unapokuwa unatubu na pale unapomgeukia Mungu, lakini hapo hapo, *kwa hakika* eti angali *akizikumbuka* dhambi za zinaa na tabia ya dhambi za mababu. Na sio hivyo tu, bali ataendelea kukutesa na kukulaani kwa sababu ya dhambi zao (kwa sababu tu ya pale kutoka 20:5 na Kumb.28: 45) hadi pale utakapoweza kutambua kuwa tatizo lolote linaloweza kumjia linatokana na dhambi ambazo itakupasa kuziungama kabla ya ukombozi halisi haujakujia! Ni kweli kwamba watu hawa hawaandiki kwa maneno haya haya na lugha hii niliyoiandika hapa, lakini huo ndio ukweli wa matokeo ya mafundisho yao wao wenyewe. Lakini hata hivyo kile wanachokifundisha nacho ***hakina ukweli wowote hata ule ndani ya Agano la Kale*** kama tutakavyoweza kuona baadaye, kwa vile wao wanatafsiri vibaya na kulitumia vibaya wazo zima la "laana ya sheria".

Kama tulivyokwisha sema hapo juu, kuwa hiyo ni laana *yake Mungu* ambayo aliitangaza na kuianzisha kupitia *sheria*. Laana hiyo wala sio jambo lenye nguvu za giza ya kutisha iliyo nje ya uwezo wa udhibiti wa kwake Mungu; laana ya Mungu sio kitu kingine chochote kile zaidi ya hukumu ya Mungu dhidi ya dhambi na kutokuwa mtiifu. Ni jambo alilolianzisha yeye mwenyewe kulingana na kusudi lake kupitia sheria na hii ni kutokana na hekima yake yeye mwenyewe, neema, haki na dhabihu kupitia kifo cha mwanae Yesu Kristo, na ya kwamba, *yeye mwenyewe ameipata njia ya kutukomboa kutoka katika laana ya sheria na hukumu yake*! Sifa kwa jina lake takatifu! Mungu alimfanya awe dhambi yeye asiyezijua dhambi ili tufanywe wenye haki wa Mungu katika yeye (2Kor. 5:21). ***Sasa basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu*** (Rumi 8:1). ***Tutawezaje*** basi sasa kulaumiwa au kuhukumiwa kwa sababu ya dhambi za mababu zetu? Yesu Kristo mwana wa Mungu, yeye alifanywa kuwa laana…kwa ajili yetu sisi …(Galatia 3:13). ***Yesu Kristo hakufanyika kuwa laana kwa ajili yetu bure tu, wala hakuteseka kwa dhambi hizo zote juu yake ili kwamba sisi tuendelee kuzichukua hukumu za dhambi za mababu zetu***. Yeye mwenyewe alishinda zote hizo, yaani dhambi, giza na nguvu za shetani. Nami nabarikiwa sana na faida zitokanazo na kifo chake na ufufuo wake mara ninapotubu na kumrudia Bwana na kuiamini Injili. Na pia sasa tunajua kwamba, Mungu, Baba wetu "alitubariki kwa baraka zote za kiroho katika Kristo!" Efeso 1:3. Kwa upande mwingine, tukiamini mafundisho mapya ya siku hizi, lazima tuseme, "tumelaaniwa kwa laana zote za mababu zetu!" Lakini imekwisha, na wala hiyo haitegemei uwezo wa elimu yangu kiroho, wa kutambua dhambi za mababu toka historia ya nyuma! ***Tutawezaje basi sasa kuibeba laana tena baada ya kutakaswa, kuoshwa, kupewa haki ya kufanywa kuwa wana wa Mungu? "Mungu akiwepo upande wetu ni nani aliye juu yetu? Ni nani atakayewashitaki wateule wa Mungu? Mungu ndiye mwenye kuwahesabia haki. Ni nani atakaye wahukumia adhabu? Kristo Yesu ndiye aliyekufa tena ndiye anayetuombea (Rumi 8: 31, 33-34). Mungu yupo kwa ajili yetu, ametupa haki kupitia damu ya mwana wake, yeye hatuhukumu kwa ajili ya dhambi za mababu zetu, isipokuwa hutuombea, akisha kutukomboa kutokana na laana ya torati***.

Kutokana na hayo yote, Mungu atawezaje sasa kuweka laana yake juu yetu, kwa sababu tu ya dhambi za mababu? Je, hawa waandishi ni kweli kuwa hawatudhihaki kwa hayo mafundisho yao? Kama tulivyokwisha kuona kuwa waandishi hao wanaamini pia kuwa mambo hayo ni ya kweli kwa mfano: msalaba wa Kristo umeshughulikia mambo yote, dhambi pamoja na madhara yake ambayo imejumlishwa na laana. Wao wenyewe wanafundisha hivyo; lakini jambo linalohusika hapa ni lipi? Ni kule kusema kwamba mtu hanufaiki na kifo cha Yesu kutokana na habari ya laana pale mtu anapotubu na kurejea kwa Bwana wakati wa kuokolewa - ni pale tu ambapo matatizo yanapomjia mtu katika maisha yake na unayatambua kuwa hayo yanatokana na laana (lakini vipi) ndipo hapo mtu anaweza kutumia faida zitokanazo na kifo cha Yesu. Lakini tatizo la mafundisho hayo, haifundishwi hivyo katika Agano Jipya na kama tutakavyoona hayawakilishi pia mafundisho ya Agano la Kale. Pili, unawezaje kutambua kuwa jambo fulani linatokana na laana; tatu, kama tulivyoona katika shauri la hapo juu, hata kama inatokea mmoja wapo akaitambua laana ndani ya maisha yake, inawachukua miaka mingi sana ya kuomba na bado uponyaji usipatikane kutokana na laana hizo! Lakini sasa, kwa nini basi ichukue miaka mingi namna hiyo kupata uponyaji kutokana na laana hata baada ya mtu kutubu na kuombewa maombi ya kuachiliwa kutokana na laana ambazo hawa walimu wa kisasa wanawafundisheni? Na kwa nini hasa uendelee kuteseka kwa ajili ya dhambi za mababu *hata kama baada ya kuzitambua laana hizo na kuzikataa*. Laana hizo ni laana za sheria ambazo ziliwekwa na Mungu; sasa *inakuwaje basi Mungu huyo huyo achague kukuacha wewe katika laana hizo kwa muda wa miaka mingi hata baada ya kuwa umekwishazitubia*? Na hasa hata baada ya Yesu kufa na kufufuka ili kukukomboa kutokana na laana ya sheria? Tunaweza kusema wazi kabisa kuwa mafundisho hayo hayaleti maana yoyote? Hayana msingi wowote wa kibiblia wala kithiologia.

Ni kifo kile kile kilichotokea pale Kalvari ambacho kinatupatia msamaha wa dhambi zetu, kile kinachotuweka huru kutokana na dhambi, kile kinachotupatia uhuru kutokana na nguvu za shetani, na kile kinachotuweka huru kutokana na kuhukumiwa; kifo hicho ndicho kinachotukomboa pia leo kutokana na laana ya sheria pale tunapoiamini Injili ya wokovu wetu kwa mioyo yetu yote. Dhambi za mababu zetu hazina uwezo wala milki ya kisheria juu yetu, 2Kor 5:17-19; 1Petro 1:18. Laana ya sheria inao uwezo au milki ya kisheria pale tu tunapochagua wenyewe kurudi nyuma, au kuishi chini ya sheria kama walivyokuwa wakifundishwa kufanya hivyo na walimu wa uongo katika makanisa ya Wagalatia, na kadhalika kama vile ilivyo sasa, hawa walimu wa kisasa wanavyotutaka sisi tufanye hivyo! Lakini mpendwa msomaji, ninakusihi, usitumbukizwe katika nira ya vifungo tena; usimame imara katika uhuru ule ambao Kristo amekufanya uwe huru.

Mambo haya yote yameelezwa kwa uwazi kabisa katika Agano la Kale tunapotazama katika kitabu cha Yoshua sura ile ya tatu (3) tunaona jinsi Mungu alivyowaleta Waisrael katika nchi ya ahadi – katika urithi wao. Makuhani walipaswa kulibeba sanduku la agano la Mungu katikati ya mto Yordani. Kwa uweza wa Mungu na upako wake, yale maji ambayo yalikuwa yanatiririka toka juu mara tu miguu yao ilipokanyaga kingo za mto ule yalipaswa kusimama na yakatulia (Mstari wa 16) kama ukuta. Na maji hayo yalikuwa yakitiririka kutokea wapi? Yalikuwa yakitiririka kwenda chini kutokea katika mji wa Adamu, ambao kwetu sisi tuliambiwa kuwa ulikuwa ni mbali sana! Na yakitiririka kuelekea katika bahari ya chumvi (ambayo pia inajulikana kuwa ni bahari ya Araba) ambayo inamaanisha kuwa ni bahari ya waziionyeshayo uwazi wa Yordani, na ilikuwa ni miji ya Sodoma na Gomora ambayo ndiyo ilikuwa ni miji ya uwazi wa Yordani, miji ile ambayo Mungu aliiteketeza kwa moto, kiberiti na chumvi, na inasemekana kwamba hukumu ile ya madini ya chumvi ilisafishiwa na kumiminikia ndani ya bahari hata kuifanya ijae wingi wa chumvi hata hakuna chochote kilicho hai ambacho kingeweza kuishi humo. (Siku za leo inajulikana kama ni Bahari ya Chumvi kwa sababu ya ile chumvi ndiyo maana maji yake yakawa vile – inajulikana pia kama ni Bahari ya Kifo kwa ajili ya hayo.) Hayo maji kwa upande mwingine wa makuhani yalishindwa na yakafutiliwa mbali na hata ule mto ukakauka kabisa (Mstari wa17). Na hao makuhani waliolichukua sanduku la Agano la Bwana wakasimama imara mahala pakavu katikati ya mto Yordani. Israeli wote *wakavuka katika nchi kavu*, hata taifa lile lote likaisha kuvuka Yordani. *Hawakuweza kulowa kabisa kutokana na chochote kile kilichokuwa kikitiririka kutoka katika mji wa Adam. Hata tone moja la maji halikuweza kuwagusa wakati sanduku la Bwana (Agano) lilipoyasimamisha mafuriko ya mkondo wa maji kwa ajili yao.*

Na Israel waliweza kujenga mnara wa ukumbusho kwa tendo hilo kwa milele (Yosh. 14:7); mnara wa mawe 12 ambapo makuhani walisimama katikati ya mto; huku wakibeba sanduku la Bwana. Mnara huo walioujenga ulikuwa ni ukumbusho wao kuonyesha yale ambayo Mungu amewatendea, kule kuyaondosha maji ya mto Yordani *mpaka pale mambo yote **yalipotimizwa***; mambo ambayo Mungu aliongea nao (Yosh14: 10). Je, unaweza kuona hapo ndugu msomaji? Jinsi ambavyo *mto wa dhambi* ukitiririka toka kwa Adam (yule mtu aliyetenda dhambi mwanzoni) kuelekea kwenye vizazi vingi vikileta kifo na hukumu kwa wote; unapaona hapo kuwa *Kristo* naye pale msalabani *aliweza kusimamisha mto wote wa dhambi* ambao Adamu aliuanzisha katika ulimwengu wote kuanzia mwanzoni kabisa ambao ulikuwa unawapelekea kifo na hukumu (Rumi 5:12). Yesu Kristo aliingia katikati ndani ya mto huo wa kutisha (msalabani) kwa ajili yetu. (Heb.2: 9,14). Na

akautundika pale juu kwa muda wa masaa matatu ya kutisha, wakati akizibeba dhambi zetu, akizisafisha kabisa mpaka ilipokuwa ***Imekwisha***. Yesu alikuwa ametengwa kutoka kwa Mungu ili kwamba aweze kuyatenga mafuriko ya mkondo na mtiririko wa dhambi, kifo na hukumu ambazo zilikuwa zikitiririka toka vizazi na vizazi kuanzia nyakati za Adamu *hadi hapo wote watakapovuka salama Yordani*. Yesu kama kuhani mkuu anaendelea kusimama katikati ya Yordani huku mafuriko ya mtiririko wa dhambi toka kwa Adamu yakisimishwa kwanza hadi hapo wote watakapovuka salama, wale wote watakaomwamini. Kwa maana katika Adamu wote hufa, katika Kristo wote hufanywa hai. Alitutenga sote na kutuleta tukiwa safi katika msalaba tukiwa pamoja naye. Rumi 6:3-5; 2Kor 5:14,17,18; Efs1:3; 2:5,6. Tumesulubishwa pamoja na Kristo, tukazikwa pamoja naye tukafufuliwa pamoja naye tukainuliwa pamoja naye na kufanywa tuketi pamoja naye mbinguni sehemu ambayo Mungu anatuleta katika Urithi wetu na akatubariki kwa baraka zote za rohoni. Bwana Asifiwe! Hakuna chochote tena kuhusiana na laana hapa.

Hebu tuwe wazi hapa kwamba Yesu hakuzishughulikia dhambi za watu binafsi tu, isipokuwa yeye amezishughulikia nguvu zote na ile sheria ya dhambi ambayo ndiyo iliyo msababishia kila mtu kutenda dhambi. Yesu ameshughulikia hivyo vyote, mizizi yake pamoja na mashina yake. Wala hakutusamehe dhambi zetu tu, isipokuwa zaidi ya hivyo yeye ametuweka huru kutokana na sheria ya dhambi na mauti ambayo ilitufanya tuwe watumwa wa dhambi, Rumi 8:2, "Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu, umeniacha huru mbali na sheria ya dhambi na mauti".

Lakini sasa, bado huyo mwandishi wa kitabu maarufu kihusuvyo laana, anafundisha kwamba, ni rahisi mtu kukombolewa kutoka katika laana ile itokanayo na dhambi katika maisha yake, kuliko ile inayotokana na laana ya dhambi zilizopita, kile kizazi cha zinaa! Mwandishi huyo anaendelea kushangaza pale anapozidi kusema kuwa, ile laana itokanayo na dhambi zako binafsi inaweza kuwakilishwa kwa upande mmoja au ni kama mizizi ya pembeni tu, mwa mizizi halisi iliyo ni minene, iliyojichimbia kwenda chini sana ardhini. Lakini mizizi hiyo halisi na ambayo ndivyo mikubwa ambayo ni kujitokeza nje, inawakilisha laana za vizazi vilivyopita pamoja na dhambi zake zote kurudi nyuma hadi kufikia miaka mia mingi iliyopita! Mwandishi huyo angekuwa anasema ukweli iwapo kama angekuwa anakubaliana na maandiko ya neno la Mungu kuwa, mizizi ya dhambi inarudi nyuma sio tu kwa vizazi vingi tu, isipokuwa hadi kufikia kwa Adam, na kufikia yale yote ambayo Adam aliyafanya. Yale ambayo Adam aliyafanya yalikidhuru kizazi chote cha binadamu pamoja na nguvu au sheria ya dhambi iliyowaletea kufa. Huo ndio mzizi mkuu wa nguvu ya dhambi ambayo ndiyo iliyomfanya kila mmoja awe mtumwa wa dhambi (Rumi 6:17). *Na kutokana na mzizi huo mkuu, ndipo Yesu akaushughulikia pale msalabani* ambapo ulikiharibu kizazi chote cha binadamu kuanzia kwa Adamu mwenyewe na imemfanya kila mmoja kuwa mwenye dhambi (Rumi5: 12:6:6:8:2). Ikiwa utajisomea mwenyewe ile Rumi sura ya 5 mstari wa 12, utaona pale kuwa ni Adamu ndiye aliyeileta dhambi, kifo na hukumu juu ya mwanadamu. Lakini sasa, ni Yesu ambaye mbali ya kule kutusamehe dhambi, ametuweka huru kutokana na nguvu ya dhambi hizo na kisha kutuokoa dhidi ya hukumu yake! Maandiko ya neno la Mungu yanatufundisha wazi kuwa watu hutenda dhambi na sasa kutokana na msalaba tunao msamaha wa dhambi hizo. Lakini pia, zaidi ya hayo yote bado maandiko ya neno la Mungu yanazidi kutufundisha kwa ufasaha kwamba Kristo ametukomboa kutoka katika milki ya dhambi ambayo ndiyo iliyomfanya kila mmoja atende dhambi. Hayo ndiyo maarifa na wokovu kamili ambao Kristo Yesu ametumwa kwa ajili yetu. Lakini sasa, yapo chini ya mashambulizi makubwa kwa hayo mafundisho yao mapya.

Kama tulivyokwisha kuona katika kitabu cha Yoshua, kadhalika katika kitabu cha Kutoka tunasoma habari za Farao pamoja na jeshi lake wakiwafukuza wana wa Waisraeli ambao walikuwa wakivuka ile bahari ya Shamu. Wao waliokolewa kutokana na hukumu kwa kuwekwa damu ya kondoo katika miimo ya milango yao kama vile Mungu mwenyewe alivyowaamuru kufanya. Farao anamwakilisha shetani na nguvu zake, lakini twaona kuwa ***hakuweza kuwafuatia watu wa Mungu***, kwa maana Mungu alifungua njia katikati yake pale Musa alipoinua fimbo yake. ***Wana wa Israel walipita salama kabisa*** katika bahari ile, lakini ilikuwa ni katikati na jeshi lake waliangamizwa! Heb.2:14, Mtd 26:17,18; Colosai1:13; 1Yoh3: 8. Tukio hili linatuonyesha kuwa jinsi ambavyo Mungu amekomboa watu wake kutoka nguvu za shetani pamoja na vifungo vyake na utumwa - "kwa kuwa hamkupokea tena Roho ya utumwa iletayo hofu, bali mlipokea Roho ya kufanywa kuwa wana ambayo kwa hiyo twalia Aba - yaani Baba" (Rumi8: 15). Lakini mafundisho hayo yanawatumbukiza watu nyuma katika vifungo na hofu! *Nguvu za Farao hakuweza kuwafuatia wana wa Israeli kuvukia bahari ili kuwateka na kuwaingiza katika vifungo na utumwa tena*. Hali kadhalika Farao hakuweza hata kuushikilia ukwato wao (Kutoka10: 26). Kinyume chake, Mungu anawapendelea watu wake kiasi kwamba, waliweza kuwaangamiza watu wa Misri kwa kuchukua fedha na dhahabu zao, Kut.12:35,36. Lakini sasa kwa mafundisho yao walimu hao wapya wanataka kutufanya sisi tuwe angamizo au mateka kwa nguvu za shetani na kwa maingiliano na kwa laana za vizazi vilivyopita, kisha kutunyang'anya urithi wetu katika Kristo. Wakianzia kwa kusema laana katika Biblia ni laana zake Mungu kupitia Torati; hata hivyo, waandishi hao husahau ukweli huu, na wanasema kwamba sio tu kwamba laana inayomiliki katika maisha yetu kwa sababu ya dhambi za mababu, bali eti, *shetani* sasa *anayo haki* ya kutusumbua katika maisha yetu kwa sababu ya

dhambi hizo za mababu zetu! Je, hiyo siyo dhihaka dhidi ya kazi ya Yesu pale msalabani? Mambo kama hayo hayafundishwi wala kutajwa katika Agano Jipya. Na kusema kwa uhakika, mambo ndani ya Agano la Kale pia.

Tafadhali hebu nielezee, kwa jinsi gani mafundisho hayo yanawaingiza watu katika udanganyifu. Katika kitabu kimoja cha kisasa, ambacho kinayakuza mafundisho haya, mwandishi wake anaelezea habari hii kulikuwa na kanisa huko Amerika (USA). Kila mara kanisa hilo lilipopata mchungaji mwingine, mke wake mchungaji huyo alikufa kwa ugonjwa au ameuawa kwa ajali. Ilitokea hivyo kwa vichungaji vinne – wake wane walikufa. Mwandishi huyo pamoja na mkewe walikuwa wanatoa ushauri katika kanisa hilo na "wakagundua" kuwa, mikondo ya kichungaji mitano iliyopita, mke wa mchungaji aliyekuwepo kipindi hicho alikuwa ni mwenye wivu na roho ya kishindani. Na hivyo mwandishi huyo ***akaamua katika ushauri wake kwamba eti wake za wachungaji hao wanne waliopita walikufa kwa ajili ya dhambi za mke wa mchungaji huyo aliyetangulia***! Pia mwandishi huyo anawaonyesha wasomaji wake kwamba hao wake za wachungaji hao wanne waliokufa, ***walikuwa ni wajinga, bila hatia – lakini hata hivyo walikufa kwa sababu ya dhambi za mke huyu wa mchungaji wa kwanza***! Anamalizia hadithi yake kwa kusema kuwa eti hao wake wanne ***wamevuna dhambi*** za vizazi vilivyopita za huyo mwanamke wa mchungaji wa kwanza. Aliomba ili "kufuta" madhara yoyote mengine ya laana ya kizazi kile.

Habari kama hizo hapo juu ni udanganyifu mkubwa, ambao mafundisho hayo ya uongo yanauleta kwa watu. Ni mafundisho ya kiuchawi na wala hayatokani na Injili ya Bwana Yesu. Maandiko hayatufundishi hivyo kwamba, "dhambi" za vizazi au "laana" zake au nguvu za shetani zinaweza kisheria au kiroho kuizidi ile ambayo Yesu Kristo aliifanya pale Kalvari. Hapo inaonyesha wazi kuwa inafundisha kinyume kabisa. ***Laana haiwezi kuuvuka msalaba wa Kristo, wala kuwafuatilia, kuwashikilia au kuwa na milki juu ya hao walio ndani ya Kristo***, na hata wale waishio kwa faida na baraka za kuwa mmoja katika Kristo, katika mauti yake na ufufuo wake! Mwishoni mwa makala hii tutakwenda kuangalia sababu zinazowafanya wakristo wengi kupata matatizo katika maisha yao; hapo hapo tena, tutakwenda kuona kuwa, laana haitajwi kabisa kwamba ndiyo chanzo cha matatizo.

***Ni Laana ya Sheria***

Tumeona kwamba laana iliyotajwa katika Biblia ni laana ***ya Mungu***; pili ni laana ya Mungu ***kupitia sheria***; ni laana ya sheria. Sheria (Torati) ilitolewa kwa wana wa Israel kupitia Musa, kama sehemu iliyo ya muhimu sana ya Agano kati ya Mungu na watu wa Israel. *Sheria (Torati) hiyo ilihusika na Agano*. Wakati ambapo lile Agano lilikuwa likiendelea kudumu, watu wa Mungu walipaswa kuishi katika hilo, kuishi kulingana na kiwango chake na watu watakatifu. Watu ambao hawakuendelea kuitunza sheria yote, walipaswa kuwa chini ya laana ya Mungu. Kumb27:26. Tunajua kuwa, sheria inatuambia nini tunapaswa kukifanya, sheria inatueleza jinsi gani tunatakiwa tuwe. Lakini sheria haikuweza kutujaza nguvu za kufanya au kuwa kama hivyo (Rumi 8:3,4; Heb 7:18,19; 10:1). Kwa hakika tusingeweza kuishi kulingana na haki ya Mungu. Kwa nguvu zetu wenyewe jitihada zote za nguvu zetu zilikuwa ni duni kuweza kujazia haki yake kwa sababu ya ile sheria ya dhambi na mauti ndani yetu. Kuishi chini ya sheria ni kugundua kuwa unapungukiwa na utukufu wa Mungu, mbali kabisa na uwepo wake, na kwamba huwezi kujaziliza haki ya Mungu (Rumi 3:10,23). Kuishi chini ya sheria ni kule kugundua kuwa, ni kwa jinsi gani sheria, dhambi na mauti zilivyo na nguvu katika maisha yako. Na kwa hakika hiyo ndiyo sababu muhimu iliyopelekea kuwepo kwa sheria kuwahukumu watu kutokana na dhambi zao, na kuwafunulia kuwa wakosa mbele za Mungu. (Rumi 3:19,20). Na walitakiwa kujua hivyo, iwapo walipaswa kuongozwa kufikia toba ya kweli na kuokolewa kutokana na hali hiyo yenye kutisha (Gal.3:22-24). Kwa sababu ile dhambi iliyomo ndani yetu ambayo inaifanya sheria ituhukumu, hicho ndicho kitu kinachokutenga na Mungu na kisha inatuweka katika kifo kiroho.

Mungu aliyaeleza hayo kwetu mapema kwa kutomruhusu yeyote yule kuingia katika uwepo wake, katika patakatifu pa patakatifu juu ya maumivu ya mauti isipokuwa yule kuhani mkuu, naye ni mara moja kwa mwaka – pale alipomtabiria Kristo. Na kwa sababu ya dhambi hiyo, hukumu ya Mungu ingali ikikalia kila roho ya mwanadamu "…***amelaaniwa*** kila mtu asiyedumu katika yote yaliyoandikwa katika kitabu ***cha torati*** ayafanye". Mtume Paulo ananukuu mistari kutoka Kumb. 27:26 katika Wagalatia 3:10. Utagundua kuwa katika ule mstari wa 26 wa Kumbukumbu ya Torati, ile hukumu ambayo Mungu anaitamka haihusu dhambi inayofahamika (kama ilivyo katika mistari iliyotangulia), halikadhalika mstari huo hautaji aina fulani maalum ya laana au hukumu, kama vile maradhi au majanga kama ilivyo katika sura ifuatayo. Hapana! Hii ni asili ya ukweli wake ambao Mungu mwenyewe anaulezea hapa; kama vile kuonyesha kuwa wanadamu wana dhambi na kwamba wako chini ya hukumu ya Mungu kwa ajili ya dhambi iwapo hawataweza kuendelea katika kuzitunza amri zake na haki yake. Kama vile Yakobo anavyotuambia, maana mtu awaye yote, atakayeshika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote" (Yak.2:10).

Kiwango cha haki ya Mungu ni timilifu ni jumla, na wala hakuna yeyote yule awezaye kuishi juu yake kwa kujaribu kuzitunza sheria! Kwa hiyo ule mstari ni wa kweli kwa mtu yeyote yule ambaye hajawahi kuishi. Hakuna yeyote yule ambaye kwa uhakika anaweza kuitimiliza haki ya Mungu katika maisha yake nje ya Bwana Yesu Kristo - hata kama walikuwa wanaishi kwa kufuata sheria au la! (Rumi 2:12). Huo ndio ukuu na asili ya kimsingi na maana sana katika mstari huo katika Kumbukumbu la torati. Sio tu kwamba mstari huo utawafunulia watu kujijua kuwa wao ni wenye dhambi, kama ilivyo katika mistari ile ya Warumi hapo juu jinsi inavyoonyesha, lakini pia mistari hiyo inatangaza hukumu ya Mungu kwa dhambi hiyo. Sasa tumeeleza ya kuwa Mungu aliwapa sheria wana wa Israel, ambayo ni ya kweli. Lakini kwa namna ya kuitunza haki ya Mungu na kuwa ni mwenye haki, ule mstari wa 26 katika Kumb.27 unawaonyesha watu wote kuwa ni wenye dhambi na kwamba wako chini ya hukumu ya Mungu. Kama tulivyokwisha sema kuwa sheria ambayo ndiyo amri ya nje ya Mungu - inafunua tu kule kutoweza kwa mwanadamu kuitunza haki yake kwa kutumia nguvu zake mwenyewe. Sheria haiwezi kutupatia haki wala kutufanya tuwe wenye haki (Gal. 3:21,22). Lakini sasa Mungu kwa rehema zake kuu na neema ametutafutia njia ili kutuhalalisha na kutufanya tuwe wenye haki na washiriki wa utakatifu wake, Gal.3:24, 2Kor 5:21, Heb.12:10 - lisifiwe jina lake! Ametupatia roho wake na kutufanya kuwa wana wake ili kwamba sasa katika mwili huu tukaribie katika uwepo wake(Gal. 4:6). Lakini hivyo sasa inafanyikaje na kutimizwaje? Ni kwa njia mpya na kwa njia ya maisha, ni kupitia Kristo, kutokana na kifo chake pale Kalvari, na ni kwa njia ya *imani* ile ipatikanayo kwa *neema* (Rumi 4:16). Ile sheria ambayo ilifanyika kuwa ndiyo njia ya kutufanya tuwe wenye haki haikufaa kitu, hivyo Mungu amempatia mwana wake, ili kutupatia njia iliyo bora zaidi, na Agano lililo bora zaidi. Na kutokana na Agano hili Jipya tunapokea neema isiyo na ukomo pamoja na wokovu, Efs. 2:7,8. Lakini lile la kale pamoja na lile jipya ***hayawezi kufanya kazi pamoja***, bega kwa bega, (Rumi 7:1-4). Hivyo sisi leo hatuwezi kufuata na kumwamini Yesu na kwa wakati huo huo ***tena kuifuata sheria na Agano la Kale*** (Gal.3:3). Huo ni mchanganyiko, huko ni kumfanya Kristo kuwa asiyefaa kitu katika maisha yetu na kuikana imani (Gal.2:21; 3:4; 4:20; 5:2-4). Sasa kwa kupitia Agano Jipya katika huyo Kristo sisi ***tumeifilia sheria*** kama njia ya kutupatia haki yetu. Kwa kuwa sheria ingeweza tu kutushawishi juu ya dhambi zetu na kuziimarisha dhambi hizo ndani yetu kama tulivyojaribu kutafuta kuzishinda. Kristo sasa, ***ametukomboa kutokana na sheria hizo*** (Rumi7:4-6, Gal.2:10), kwamba yatubidi sasa kupokea roho wake kwa imani na kutuweka huru kutokana na sheria ya dhambi na mauti. (Rumi8: 2-4; Gal.3: 14).

Hakuna sehemu yoyote ile ambayo mitume au Kristo ambapo wanapendekeza kuwa sheria iwe kama ndiyo njia ya kupokea msamaha au kutuweka huru kutoka dhambini na hukumu yake au kutufanya tupate haki mbele zake Mungu. Kinyume chake matumizi ya sheria ya Agano la Kale inaleta matokeo ya kushindwa, dhambi na kuhukumiwa (Gal.5: 16-18 Rumi 3:19). Kwa hiyo, katika Kirsto Yesu Mungu ***ameyaondolea yale ya kale*** na kuyaanzisha mapya. Mtume Paulo anawapa changamoto wale wanaopendelea kukaa chini ya sheria (Gal.4: 21) kutokana na matukio ya Agano la Kale yenyewe. Mtume Paulo anawaonyesha kuwa ***Mungu amekwisha kuiondolea mbali ile sheria***, kwa sababu ile sheria haiwezi kabisa kuwa kama njia ya kutupatia baraka na inaweza tu kututumbukiza katika vifungo. Imani katika Kristo ndiyo njia pekee ya kupokea msamaha na uhuru kutokana na dhambi pamoja na hukumu zake. Matumizi yoyote yale ya sheria hayawezi kabisa kufanya hayo. ***Kwa hiyo hatupo tena chini ya sheria,*** kwa sababu Kristo amewakomboa wale wote waliokuwa chini ya sheria ili kuwafanya kuwa wana wa Mungu, (Gal.3:25; 4:5). ***Kristo ametukomboa kutokana na laana ya sheria*** - hii ina maana kwamba, tumekombolewa kutokana na hukumu ya Mungu iliyokuwa ikitusubiria kutokana na kushindwa kwetu kuitunza ile haki yake; sheria ingeweza tu kutuonyesha dhahiri kama wenye dhambi na kutulaumu. Kwa jinsi hiyo Kristo Yesu amezichukua dhambi zetu pale Kalvari kisha kutukomboa kutokana na kule kuhukumiwa. Haleluya!

Hivyo ndivyo tunavyofundishwa katika waraka ule kwa Wagalatia. Zaidi ya hapo, ***ni nani*** aliye chini ya laana ya sheria? Galatia 3 inatuambia ***kwa uwazi*** kwa maana wale wote walio wa matendo ya sheria wako chini ya laana (Galatia3: 10)! ***Wale walio chini ya sheria na ambao wanapenda kuifuata sheria*** na kutafuta haki na ukombozi kwa kupitia sheria, ***hao wanaiacha imani*** na uweza wa wokovu wa Mungu; matokeo yake ni lazima wataishia katika kushindwa na dhambi, mwisho wao ni katika kuhukumiwa na Mungu; hiyo ndiyo chini ya laana yake. Kwa hiyo Mtume Paulo anawaonya kwa nguvu na kuwaomba wasirudie tena kwenye kuifuata sheria au kujiweka wao wenyewe chini ya sheria tena. ***Kuirudia sheria, ni kujiweka mwenyewe chini ya hukumu au laana ya Mungu.*** Hii inakuingiza katika vifungo na kuhukumiwa (Gal. 4:21-31).

***<u>Kwa hiyo, jambo pekee ambalo huleta laana ya Mungu juu yetu, sio dhambi za mababu, isipokuwa ni kule kuishi chini ya sheria ya Agano la Kale!</u>***

Unaweza sasa kuona jinsi waandishi hawa wapya wanavyojifanyia mambo kwa kufuata vichwa vyao tu, na kwa hakika wanafundisha vitu vyao binafsi tu, mambo yaliyo *kinyume kabisa na maandiko*. Hivyo ndivyo haswa, hawa waandishi na walimu wa kisasa wanavyofanya. ***Wanawarudisha watu nyuma na kuwaketisha katika mambo ya kidini na hukumu ya sheria***. Eti kwa sababu tu ya ule mstari mmoja wa

Kut.20:5 pamoja na Kumb.28: 45, wanafundisha kwamba eti laana ya sheria bado ipo na inatumika hata kwa wale waliomo ndani ya Kristo; eti kwa sababu tu ya dhambi za mababu. ***Mtume Paulo anasema, hapana, laana ya sheria inawahusu wale tu wanaotaka kuishi kwa sheria badala ya kuishi kwa imani katika Kristo.***

Wale wanaoishi kwa imani katika Kristo, wamekombolewa kutoka katika laana ya sheria. Hivyo dhambi za mababu haziwezi kuwatesa pale wanapokuwemo ndani ya Kristo! Lakini hawa walimu wanasema kuwa, "Hapana; laana bado inatenda kazi hata kwa wakristo, hata wakristo wale ambao wamekua kiroho na kwamba ***hatukombolewi*** kutokana na laana ya sheria ***mpaka tunapozitambua*** dhambi za mababu ambazo zinatenda kazi kama laana katika maisha yetu na ambazo ndiyo chanzo cha matatizo yetu na kisha kuutumia msalaba kwao!" Wanadai ya kuwa utaratibu huu unaweza kudumu kwa miaka mingi au hata kwa maisha yako yote!

Mafundisho ya jinsi hiyo hayatukomboi kutoka katika laana, isipokuwa yanaweza tu kutuletea laana pale tunapoipinga kweli ya Injili ya Mungu! Hapa moja kwa moja wanayachanganya mafundisho ya kwa Wagalatia. Ule mstari halisi ambao unatuambia kuwa tuko huru kutoka katika laana, wao wanatumia vibaya ili uweze kuunga mkono mawazo yao potofu na wao pasipo hata kujua, wanaileta laana ya sheria chini kabisa hadi kwetu kama madhara yake! Zaidi ya hayo yote, mafundisho hayo yanakusudia kuturudisha nyuma kwenye aina fulani ya ushirikina pamoja na mambo ya unajimu na kati ambapo tutawezeshwa kupata "uwezo wa maroho" wa kugundua nini kilisababisha dhambi pengine miaka mia mingi iliyopita zilizofanywa na mmoja wa mababu zetu?

Lakini jawabu la Mungu katika hayo yote ni kuamini katika wokovu kamili ule anaotupatia kupitia huyo Kristo Yesu. Sasa kama nilivyokwisha kusema kwamba waandishi hawa wanakiri kwa uhuru kabisa kwamba tumehalalishwa kwa imani katika Kristo na wala sio katika matendo ya sheria. *Hata hivyo*, *bado* mafundisho yao yanaendelea kutangaza kuwa, sheria na laana zako zinaendelea kutumika leo kwa wakristo hata kama wamekwisha kutubu dhambi zao kwa ukweli kabisa, na kuokolewa. Wanasema hayo eti kwa sababu tu ya pale katika Kut.20:5, Kumb.28:48 na Mambo ya Walawi.26:40 wanasema ni mpaka pale tunapoweza kuyagundua madhara ya dhambi za mababu zetu katika maisha yetu ndipo tunapoweza *kuanza taratibu za ukombozi* kupitia "karama za roho na utambuzi" (kama wanavyodai) na toba kwa ajili ya dhambi za mababu zetu. Kwa maneno mengine hapo wanamtangaza Kristo ***pamoja na sheria*** kwa wakati mmoja. Kwa upande mwingine, ***Mtume Paulo anasema kuwa huko ni kuikana imani na kumwacha Yesu!***

Hebu niseme hapa kuwa kadiri ilivyokuwa, kwamba sheria ilikuwa ndiyo mwangaza wa haki ya Mungu mwenyewe, wema wake na utakatifu, hapa ipo thamani ya kudumu ihusuyo sheria na wala sio katika maonyesho ya masherehe, matarajio ya ki-inje (kimwili) bali katika hali ya tabia ya haki ya Mungu. Mungu yule anayetaka kututimilishia ndani yetu na kwa ajili yetu ili tuwe washirika wake. Sio sasa kwa kupitia utunzaji wa sheria isipokuwa kupitia imani katika Kristo. Rumi 3:31; 8:3,4; 2Petro1: 4. Hiyo ndiyo sababu inayomfanya Mtume Paulo aseme katika Rumi 3:31, "Basi Je, waibatilisha sheria kwa imani hiyo." Hapa haongelei kuhusu mambo ya kiinje (kimwili) au mambo ya sheria za masherehe, kama vile kutahiriwa (ambazo yeye anaonya kuwa tusiyaendekeze). Yeye hapa anaongelea kuhusu haki ambayo sheria ilipaswa kutuingiza sisi ndani yake lakini haikuweza kufanikiwa (Gal.3:21). Katika nyaraka zake kwa Warumi, halikadhalika kwa Wagalatia, Mtume Paulo anafasiri ambavyo tumehalalishwa na jinsi ambayo haki ipatikanavyo kwa sheria iliyotimilizwa ndani yetu na jinsi ilivyopatikana kwa njia ya imani kwa kadiri tunavyoishi na kutembea katika roho; na wala haipatikani kwa njia yoyote ile nyingineyo kama vile ile ya kutumia sheria!

Lakini hawa waandishi wa kisasa hupenda kuitumia sheria kwa njia isiyo na uhalali wa Agano Jipya wala Agano la Kale lenyewe; kama tutakavyoweza kuona baadaye. Tumekwisha kuona kuwa pale katika Gal.3:10 Mtume Paulo ananukuu Kumb.27:26; pia tumekwishagundua tayari kuwa huo ndio mstari wa kimsingi ikihusisha haki ya Mungu isiyo na mashaka yoyote ile; pamoja na hukumu zake juu ya kushindwa hatamara moja tu katika kuzitunza amri zake (Mungu). Haipo kabisa kumbukumbu yoyote ile hapa kwa dhambi maalum, kama vile ilivyo katika mistari iliotangulia, wala aina yoyote ile ya laana au hukumu, ambavyo imetajwa kwa ajili ya kushindwa huko; kama vile ilivyo katika ile sura ya 28. Mstari huo ni kumbukumbu ya kweli kuonyesha kwamba hukumu ya Mungu iko juu ya yeyote yule atendaye dhambi na kwa sababu hiyo Yesu Kristo alikuja kuishughulikia ile nguvu ya dhambi ndani ya maisha ya watu pamoja na hukumu ya dhambi juu yao. Lakini sasa, hawa waandishi wa kisasa wanaporejea katika Gal.3:10, wanapoteza lengo ambalo Mtume Paulo analijenga hapo ndani ya mafundisho yake; yeye ananukuu Kumb. 27:26, isipokuwa wao sasa wanayeyusha maana halisi ya mstari huo kwa kusema kuwa mstari huo wa Wagalatia 3:10 *unajumlisha laana iliyotajwa katika Kumb.28:45*, na hivyo ndivyo wanavyoendelea kukazia katika mafundisho yao - aina zote za laana katika ile sura ya 28 Kumb. Na wanazidi kutuambia kuwa, hivyo ndivyo Mtume Paulo

anavyorejea pale katika Gal.3:10! Wanatuambia kuwa mkristo anaweza akateswa ***kwa laana yoyote ile iliyopo pale katika Kumb.28 kwa sababu tu ya dhambi zile walizozitenda mababu zao*** - aina zote za magonjwa, majanga, maafa, kushindwa, kuanguka kibiashara, kuvunjika vunjika kwa familia pamoja na ndoa, wenda wazimu; hayo yote eti yanaweza kukushikilia na kukutesa kwa sababu ya dhambi za mababu! Hivyo ndivyo wanavyofundisha sehemu ile ya Gal.3:10!

Mpendwa msomaji wangu, Je, hayo ndiyo Mtume Paulo anavyolifundisha kanisa la Wagalatia? Je, pale anawaandikia Wagalatia kuhusu kuteswa kwa nje pamoja na hukumu inavyoweza kuwajia wakristo kwa sababu ya dhambi za mababu na jinsi unavyopaswa kuwa mwangalifu katika kuzigundua laana hizo pamoja na mateso ndani ya maisha yako? Je, Paulo anawafundisha, "Uzitubie dhambi hizo za mababu kisha, endelea kuitumia ile faida ya msalaba wa Kristo"? Je, anaitumia ile Kumb.27:26 kwa njia ya jinsi hiyo pale anapofundisha mambo hayo? Hapana. Hapana kabisa! Paulo ***hataji*** dhambi za mababa zetu. ***Hataji*** laana ile ya nje iliyotajwa katika sura ya 28 Kumb. ***Hafundishi*** kuwa dhambi za mababu zinaweza kuletea hukumu ya nje juu ya wakristo! ***Hasemi*** kuwa ni lazima tugundue dhambi hizi za mababu zetu ili tuwekwe huru kutokana na hukumu na laana! Kama tulivyokwisha ona isivyo na ukomo ile Galatia sura ya 3, hali kadhalika ule waraka wote wa Wagalatia, unatufundisha kuhusu imani, kuhalalishwa, haki, pamoja na kuishi katika Roho na katika ule uhuru wa mwana wa Mungu. Yeye alizipinga kazi za kimwili na kule kuishi kwa kufuata sheria (kuwa chini ya sheria) *ambako kunaleta hukumu na kushindwa*. Hayo ndiyo mambo makubwa ya msingi kuhusu imani. Lakini kama tulivyoona ndani ya makala iliyopita ihusuyo kutubu kwa ajili ya dhambi za kitaifa, waandishi hawa wa kileo bado wanaitafsiri vibaya Injili na kwa uhakika hawaelewi vizuri Agano Jipya na kwamba linahusika na mambo gani hasa. Wao wanapenda tu kuzingatia ***mambo ya nje***, mambo ***ya kimwili***. Kwa hiyo, kutafsiri ki-Biblia, huitafsiri kimwili na wanalenga zaidi katika mambo ya nje. Maana ufalme wa Mungu haupo katika kula na kunywa (mambo ya nje), bali ni haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu (Rumi14:17). Yesu alikuja kuleta mabadiliko makubwa yenye msingi wa kiroho ndani yetu sisi tuliozaliwa katika ufalme wa Mungu, tumehalalishwa na kuwekwa huru kutoka dhambini na hukumu yake. ***Lakini walimu hawa wao wanazingatia tu mambo ya nje ya sheria***, wakidhania kwamba mambo hayo yanaweza kutuweka huru katika haki ya Mungu. Lakini kama ilivyotokea kwa walimu wa uongo huko kwenye makanisa ya Wagalatia walivyokosea (Gal.3:1-3), halikadhalika walimu hawa wa kisasa kwa masikitiko makubwa na kwa hatari sana wanakosea pia.

Na hizi ni tabia za hila na udanganyifu wa jinsi gani huu? Kama kwamba Mungu anaruhusu au anatuma mateso au masumbufu juu ya watu wake nyakati hizi, kama vile aina ya laana yenye kutisha na isiyojulikana kutoka huko nyuma (Kale) ambayo sasa tunapaswa tuigundue kwanza na kuitambua na ndipo tuitubie na kuutumia msalaba wa Bwana Yesu katika hilo. Lakini hayo mafundisho ya uongo yamo kwenye hatari ya kutisha yenye kulenga kunyang'anya ule mfano wa kweli wa tabia ya Mungu. Wanakaribia kabisa kwenye mtindo wa kiuchawi katika kumwakilisha Mungu na wanamfanya Mungu kuwa ndiye anayeruhusu laana za kutisha ili kututesa, ***kwa sababu eti ya dhambi za mababu zetu zilizojificha***. Na kutokana na hali hiyo hatima yake ***inawaletea watu hofu na woga*** tukifikiria kana kwamba tabia ya tatizo lolote lile linaloweza kututokea ndani ya maisha yetu, inawezekana kuwa imetokana na laana anayostahili kufanyiwa fidia (kafara). Lakini ni kwa ajili ya upotofu huu ndio maana ndugu zangu kaka na dada zangu wa kiafrika wameupokea ukombozi wake. Hiyo ndiyo hali halisi na tabia inayowaingiza watu kwenye hofu na kuyafanya maisha yao yaonekane kuwa yenye huzuni (uduni na umaskini) kabla walipokuwa bado hawajasikia na kuiamini Injili ya wokovu wao. Huo ni ushirikina wa kutisha sana! Na sasa walimu hao hao wa kisasa wanatafuta kuwabatiza tena katika hali hiyo na tabia ya hofu na ushirikina hayo yote yanafanywa kwa jina la mafunuo ya Kikristo!

Hebu sasa tufikirie laana ya sheria ni kitu gani. Kama ilivyotolewa mifano yake katika Agano la Kale, ndipo tutakapoweza kuona jinsi wanavyokosea kuwakilisha hata hiyo sheria ya Agano la Kale.

**Laana ya Sheria katika Agano la Kale**

**Kut. 20:3-5**

Hawa waandishi wa kisasa wanajaribu sana kuunga mkono zile fikra zao kuhusiana na laana. Hapo kimsingi wao wanazingatia katika nyaraka mbili za maandiko ya neno la Mungu; pengine jambo la maana zaidi wao huchukua kutoka kitabu cha Kut.20:3-5 pamoja na nyaraka nyinginezo ambazo zinazokubaliana na hizo katika Kut.34:7, Hesabu 14:18 na Kumb.5:9). Kutokana na nyaraka hizo wao wanataka kutueleza kwamba hukumu au madhara ya dhambi za mzazi mmoja - ambazo wao huziita "laana" - inaendelea kuchukuliwa mpaka vizazi vinachoendelea hadi kile cha nne, pamoja na matokeo ambayo vizazi hivyo vimeteseka na kuumizwa kwa laana hiyo, ukichanganya na watu ambao wameokolewa na kuishi kama wakristo katika Kristo! Wao wanabuni tu wazo la "laana ya vizazi vilivyopita" toka katika sura hiyo. Kwanza kabisa katika

mstari huo unaopatikana katika Kut.20:5, Mungu anasema kuwa,
"dhambi za mababa huzipatiliza *juu yao wao* ***wamchukiao***", kwa hiyo, hapo inaonyesha wazi kuwa wale waliomo katika Kristo leo kwa wazo lao wanahesabiwa pia pamoja na hao wamchukiao Mungu! Hiyo ni kutokana na tafsiri yao wao wenyewe waandishi hao! Tutakwenda kuona kuwa, laana haitajwi kabisa kwamba ndiyo chanzo cha matatizo. ***Kwa kuwa maandiko yanasema kuwa Mungu hupatiliza dhambi za mababa juu ya watoto wao wamchukiao***. Lakini hawa waandishi wao, wanafundisha kwamba; Eti wakristo wanakuwa wakiteseka kwa sababu wanakuwa wametembelewa na dhambi za wazazi wao, hata kama wao wanaishi maisha ya utakatifu! ***Lakini wakristo hao sio wale wamchukiao Mungu! Basi kwa hiyo waandishi hao wa kisasa wanapaswa watueleze wanaitumiaje mistari hiyo kwa wakristo ambao Kristo sasa amewafilia!***

Jambo la pili, kama tulivyokwisha kugundua habari hii haisemi kwamba Mungu *ataadhibu* vizazi vitatu hadi vinne vinavyowafuatia, isipokuwa yeye anasema kuwa *atawapatiliza* kwa dhambi za wazazi. Ezk.18 inaunga mkono jambo hilo na maana yake kwa kueleza kwa uwazi kuwa, ***"mwana hataubeba uovu wa baba, bali atahukumiwa kwa dhambi zake mwenyewe"***; ijapokuwa hapo pana utata pia, kwamba mwana anaweza kutegewa kwa dhambi za babaye na kufuata katika njia za uovu za babaye. Lakini sasa iwapo mwana atamgeukia Bwana na kutubu, ndipo mwana hatateseka kwa sababu ya dhambi za babaye, ile toba yake inamsafisha na kumhalalisha kikamilifu mbele ya Mungu, hivyo kwamba haina ulazima kwake kutubu dhambi za babaye. Hayo ndiyo mafundisho yaliyo wazi kutoka kwa Ezekiel na yanaenda sambamba na habari iliyo katika Kut. 20.

Kwa uhakika, ***Mungu alikuwa anawafokea Waisrael*** pale katika Ezekiel, ***kwa ulalamishi wao na kule kung'ang'ania kwao kuwa watoto wanateseka kwa sababu ya dhambi za wazazi wao***. Wale Wayahudi waliokuwa wapo utumwani ***walikuwa wakisema kuwa wao wanateseka kutokana na dhambi za baba zao***. Lakini sasa ***Mungu akasema "Hapana, kila mmoja atateseka kwa dhambi zake yeye mwenyewe".*** Katika Isaya 65:7 Mungu anaweka wazi pale kuwa, hukumu yake imewajilia juu yao kwa sababu wametenda dhambi ***pamoja na*** baba zao - hawakuzikimbia dhambi za baba zao bali waliendelea katika dhambi zile zile. Na kwa hiyo sasa wanavuna hukumu ya Mungu ambayo ndiyo maana halisi ya Kut.20:5. Lakini sasa hawa waandishi wa kisasa wanampinga Mungu sana hasa nyakati hizi za Agano Jipya na Neema kwa kusema wazi wazi kuwa, "sawa watoto wanateseka na kuyabeba maovu ya baba zao" - hata baada ya watoto hao wao wenyewe watubu na kumgeukia Bwana ipasavyo! Na hayo mafundisho yao yamesimamia katika kasoro kubwa mbili: yanapingana na mafundisho yanayopatikana katika Agano Jipya *na hata Agano la Kale lenyewe*. Katika Agano la Kale wale watoto ambao hawapendi kuziacha njia mbovu za mababa zao, wao wananaswa na dhambi za mababa zao na wanavuna matokeo ya uovu huo. Hata hivyo Biblia yote inaonyesha na kutufundisha kwamba mara tu baada ya toba, mtu huyo au (watu wa Israel katika Agano la Kale) wanakuwa wameondolewa hatia, wanakuwa wamesamehewa, wamewekwa huru kutokana na dhambi za wazazi wao; amesafishwa na kuhalalishwa na Mungu.

Katika kanuni ya mahusiano pamoja na Mungu, mtu hawezi kuzuiliwa kutokana na dhambi au hatia ya wazazi au mababu. Kanuni hii imeonyeshwa ndani ya Biblia mara kwa mara kwa mafundisho pamoja na mifano yake. (Tafadhali hebu rejea pale penye makala ya kwanza ambapo jambo hili limeelezwa kwa kirefu hapo).
***Lile wazo kwamba mtu anaweza akateswa kwa laana ndani ya mwendo wake pamoja na Mungu baada yakuwa amekwisha tubu ipasavyo, halipatikani kabisa ndani ya Biblia wala halifundishwi hivyo hata kidogo au je, wewe waweza kuupata mfano wa fundisho moja huko katika Biblia unaoelezea hivyo?***

Upo ukweli kwamba, kwa namna nyingi, matendo fulani fulani atendayo mtu yanayo madhara yake ambayo hayaepukiki. Kwa mfano, kama mzazi anakataa kumtunza mtoto wake, au kumlisha ipasavyo hivyo basi mtoto huyo bila shaka anaweza akaangukia katika afya mbaya au pengine au mtoto huyo anaweza kuangukia katika mikono ya marafiki wabaya. Na kama tulivyokwisha kuona kuwa, njia za uovu za wazazi hao zinaweza kumnasa mtoto wao pia aingie katika dhambi hiyo hiyo; uovu katika jamii pia unaweza ukawa kama mtego kwa watu wanaoishi humo. Ijapokuwa mambo hayo yapo hivyo, lakini hata hivyo inapotokea mtu yeyote yule anapokuwa katika hali yoyote ile kati ya hayo yaliyotajwa hapo juu, au hali nyingine yoyote ile iwayo, kisha mtu huyo akamgeukia Bwana katika toba ya kweli, basi hapo mtu huyo anakuwa amesafishwa kikamilifu na kuwekwa huru mbele za Mungu ambaye hawezi kuyashikilia matendo yao maovu yaliyopita kinyume nao wala hatazishikilia dhambi za mababu zao zilizopita kwa ajili ya mtu huyo. Kwa sababu mtu huyo anakuwa amehesabiwa haki na kusafishwa kikamilifu na Mungu katika uhusiano wao pamoja naye, pasipo kujali madhara yoyote yale ya matendo yasiyoepukika. Wanaweza wakawa bado wanayachukua kutoka katika matendo yao ya zamani katika maisha yao, lakini katika mwendo wao pamoja na Mungu, hawawezi kuteswa wala kuzuiwa kwa laana itokanayo na mambo yaliyopita baada ya wao kwa hakika sasa wanakuwa wamekwisha kutubu.

***Ndani ya mwenendo wao pamoja na Mungu laana haiwezi kamwe kuwafuatilia zaidi ya ile ya toba ya kweli waliyoitenda. Jina la Bwana lisifiwe!*** Hayo ndiyo mafundisho ya Biblia na hayatofautiani na maandiko yote ambayo ni neno la Mungu. Katika ukweli huu wa kimsingi kwamba toba yenye uhakika humtengeneza au humleta mtu ndani yake ule uhusiano mzuri na Mungu na hivyo dhambi zake hazikumbukwi tena, na hapo sasa yale yote yaliyopita yanakuwa hayana nguvu tena juu yao pale wanapokuwa wanatembelea na Mungu.

Pengine litakuwa ni jambo la maana kuona wafasiri wa Biblia nao wanasemaje juu ya jambo hilo, kwa mfano, katika tamaduni za kale kama vile Israel na kama vile ilivyo katika tamaduni fulani fulani leo. Ni jambo ambalo lilio la kawaida kuona familia wanashikamana, pamoja na kuishi pamoja, au makazi mamoja au jirani, kwa hiyo haitakuwa ni jambo lisilokuwa la kawaida, kuvipata vizazi vitatu hadi vinne kutoka katika familia inayoishi kwa pamoja au wanaoishi jirani sana na mwingine. Hii inaweza kuelezea chanzo cha Mungu hata kuhesabia hadi vizazi vinne kwa ajili ya uovu wa baba. Mtu anaweza akawa anaishi vizuri na ana uhusiano mzuri na watoto wake wote hadi wajukuu zake ambao nao pia wanaweza wakawa bado wanaishi hai. Hebu tafakari juu ya jambo la Kora aliyempinga Mungu na akawa amesimama mlangoni mwa hema lake akiwa pamoja na familia yake yote (Hes.16). Kwa hakika, wale ambao tumewafahamu katika maisha yetu ya utotoni na maishani mwetu, hao ndio waliweza kutushawishi sisi zaidi, na pengine hii inatusaidia sana kuilewa maana halisi ya Kut 20:5.

Jambo lililo wazi na linalokubalika katika yale yote ambayo nimeyaandika juu ambayo yanahusika katika kujishughulisha kwake Mungu pamoja na watu wake wale ambao walichaguliwa katika Agano la Kale. Taifa la Israel lilikuwa ni watu wake aliowachagua nao waliwakilishwa na ***taifa moja*** tu linaloonekana; halikadhalika lilihusika pia na mtu mmoja mmoja binafsi. Mungu pia alijishughulisha nao kama mtu binafsi ambao kwa kushirikishwa alihusika na matendo yao katika Historia. Jambo hili liko tofauti sana ikiwa utalinganisha na kanisa la leo ambalo linajumlisha watu wa kutoka katika ***kila kabila na kila taifa***. Tafadhali rejea makala yangu ya kwanza, sehemu ile ambayo nilifundisha juu ya dhambi ya Akani na Sauli. Pia tungetaja juu ya uasi wa Kora au kule kuhangaika kwa taifa la Israel mle jangwani, ambapo watoto wao walipaswa kusubiri ili wapate kuingia katika nchi ya Ahadi kwa sababu ya dhambi za wazazi wao, kwa sababu ya kutokuamini kwa wazazi wao. Lakini sasa, mifano hiyo yote ilikuwa inamwonyesha Mungu jinsi alivyokuwa akijishughulisha *kwa namna ya pekee* katika kuhukumu *Israel kama taifa*. Hata hivyo, haupo hata mfano mmoja kati ya hiyo yote unaoweza kubadilisha yale yaliyofundishwa ndani ya Biblia; kwa mfano pale inapotokea mtu (au taifa la Israel) akatubu kikweli, kisha mtu huyo (au taifa la Israel) akasamehewa kikamilifu na kuachwa huru ili kwamba yale ya kale yasiwe na nguvu tena dhidi yao, kadiri wanavyozidi kuendelea kutembea na Bwana. Na jambo hili pia limekwisha kuelezwa kwa uwazi katika historia ya wana wa Israel.

Tunaona pia kwamba Daniel naye alichukuliwa utumwani kwa sababu ya uasi wa wana wa Israel dhidi ya Bwana, ijapokuwa yeye binafsi hakuwa na hatia yoyote ile. ***Lakini dhambi na uasi wa kizazi chake na kizazi kile kilichomtangulia, haukuweza kwa namna yoyote ile, kumzuia, kumpinga, kumharibu au kumtesa katika uhusiano wake na Mungu wala mwendo wake kiroho na Mungu***. Kinyume chake yeye ni mfano wa mtu yule aliyebarikiwa, mwenye haki na upendo wa Mungu. Ijapokuwa yeye Daniel alipelekwa Babeli akiwa na wenziwe; mfano huu unahusika tu na Agano la pekee la Mungu na wana wa Israel kama taifa na wala haiendi sambamba na Agano Jipya au Injili.

Ikiwa wewe utapenda kuitumia sheria kwa njia hii, basi kwa kweli basi yale yanayowahusu Wakristo ndiyo yale tunayoyapata kuandikwa katika Kut. 20:6, ambapo ***Mungu anaahidi rehema zake kwa maelfu wampendao***. Hapa tunaupata utofauti kati ya Mungu kuzifuatilia dhambi za wale wamchukiao hadi kufikia *kizazi cha nne*, na pale ambapo Mungu amezidisha rehema zake hadi kufikia *maelfu* wale wampendao! Ni kweli kabisa! Rehema zake zinaishangilia hukumu yake. Hizi namba au hesabu za maelfu zinaonyesha kuwa baraka zake za umilele zi juu ya hao wampendao. Hapo hakuna zaidi ya jingine! Lakini sasa, ***hebu waone hawa walimu wa kisasa wao wanaiweka "laana" ambayo kwa kawaida inawahusu watu wale ambao hawajatubu, ambao wanamchukia Bwana, na kuiweka juu ya wakristo leo***! Lakini sasa maandiko yanasemaje? Mtume Paulo anatuambia kuwa ***"tumebarikiwa"*** (hapa hasemi kuwa tumelaaniwa) kwa ***baraka*** zote za rohoni katika Kristo (Efs.1:3). Mungu akiwa upande wetu, ni nani atakayekuwa juu yetu? Naye ni nani anayetulaumu sasa? ***Je, ni nani atakayewahukumia adhabu wateule wa Mungu?*** (Rumi8:31-34). Pengine haya mafundisho ya kisasa yamo katika hatari ya kuyatenda haya tunayoulizwa hapo juu! Lakini sasa Mungu yupo upande wetu, na ni Kristo ndiye aliyetuhesabia haki na ndiye anayetuombea. Itakuwaje sasa Baba pamoja na mwana, watuletee sisi hukumu ambayo iliwapasa wale waliokufa, pale tunapokuwa tupo ndani yake Kristo?

Tunahitaji kutofautisha haya maagano mawili, na pia inatupasa tujue, maagano hayo yanawaelezea watu

gani, kwa sababu, sasa walimu hawa wa kisasa wanashindwa kutambua sio tu jinsi gani sheria na laana yake inavyotenda kazi ikiwa ni pamoja na kushindwa kutambua mazingira yake; isipokuwa wao pia hawaelewi kuwa yanamhusu mtu gani! Wao, (walimu hawa wa kisasa) huitumia sheria pamoja na laana kwa ajili ya watu wa aina zote - Wayahudi au watu wa mataifa, watakatifu au watu wenye dhambi; wanashindwa kutofautisha wakati wote wao kwao ni sawa tu! Kabla hatujaendelea zaidi sana hebu sasa tuangalie katika jambo hili.

**Agano la Mungu kwa Israel**

Onyo la Mungu katika amri yake ya kwanza katika Kut. 20:3-5 ni dhidi ya wale wanaoabudu masanamu. Lakini hawa walimu wa kisasa wao wanadai kuwa kwa sababu ya dhambi hii maalumu, ndiyo sababu laana inawajia kizazi kinachokuja, pasipo kujali kuwa watu hao ni watu wa namna gani - Wayahudi au wamataifa, watakatifu au wenye dhambi. Bila hata kuridhika na hilo wao wanaendelea kung'ang'ania kufundisha kuwa karibu kila dhambi anayoitenda mtu, inaweza ikamletea laana kwa vizazi vinavyokuja! Lakini sasa, hebu tutazame Mungu mwenyewe anavyosema katika ule mstari wa 5, hapo anawaambia Waisrael "…Bwana Mungu ***wako***.." Mungu hapo anakazia ukweli kuwa yeye ni Mungu ***wao*** na wao ni watu ***wake***. Kupitia lile chaguo lake la neema ya upendo na alikwisha kuwaambia katika Kumb. 2:6-8; 10:15, na tukitilia maanani ule ukweli kwamba yeye aliwakomboa kutoka Misri kwa damu ya mwana kondoo, na hivyo ndivyo Mungu anavyozitambulisha kutolewa kwa amri kumi katika ule mstari wa 2. Anasema kuwa "Mimi ni Bwana Mungu wako niliyekutoa kutoka katika nchi ya Misri kutoka katika nyumba ya utumwa, usiwe na Mungu mwingine isipokuwa mimi."

Hapo ndipo, Mungu anapotoa ule msingi na sababu za toleo la amri kumi ambazo zilikuwa zinawajia. Yeye ndiye Mungu wao kwa nguvu za uchaguzi wake yeye mwenyewe kwa ajili yao na kwa nguvu ya kuwaokoa na kuwakomboa! Amewafanya kuwa ni watu wake; amewanunua na akajifunua kwao, akawaokoa na akawabariki kwa kuwepo kwake pamoja na neno lake; anawaambia kuwa wao (Waisrael) ni watu maalum juu ya watu wote wa nchi. Na *kwa sababu ya hilo*, anawategemea kuwaona kuwa ni *waaminifu kwake*, kwa sababu anawaambia kuwa "..Bwana Mungu wako ni Mungu mwenye wivu" wao ni watu wake yeye naye ana wivu juu yao kwa ajili yake mwenyewe. Wao bado ni watu wake, hivyo yawapasa kumheshimu kama watu wake, ili jina lake lipate kutakaswa na kuabudiwa na sio kufanywa najisi katikati ya mataifa ili kwamba jina lake lipate kuheshimiwa. Mungu hawezi kuruhusu vishawishi ambavyo hatimaye vinaweza vikamfanya mtu binafsi au hata jumuia ya Israel iweze kumuasi Mungu. (Jambo hili linasaidia kueleza baadhi ya hukumu na namna ya pekee iliyowafikia wana wa Israel; kama vile ule uasi wa akina Kora - Kumb.16). Kama tutafuatilia na kuona jinsi Mungu alivyowatendea, kuwafanya wawe watu watakatifu, ***jambo ambalo alikuwa hajawahi kulifanya kwa taifa lingine lolote lile***.

Waisrael pia walihusika na matengenezo ya aina ya pekee kabisa ambayo aliwafanyia, jambo ambalo Mungu hakulifanyia taifa lingine lolote lile liwalo kwa jinsi ile ile aliyoifanya kwa Waisrael. Kwa maneno mengine, ***mambo hayo yote mawili, yaani baraka na hukumu za Mungu zilikuwa ni za aina ya pekee kabisa kwa wana wa Israel***. ***Na Mungu alilianzisha Agano lake pamoja nao, na akawapatia sheria (torati) pale katika mlima wa Sinai ambazo hizo zilithibitisha baraka hizi na laana au hukumu kama sehemu tu ya Agano la Kale na wao***. Tunafahamu ya kuwa Mungu habadiliki, isipokuwa baadhi ya mambo hubadilika - hubadilika sana na kwa kimsingi. Ipo tofauti kubwa kati ya Agano Jipya na Agano la Kale; kulikuwepo pia na tofauti kubwa kati ya wana wa Israel na yale mataifa mengine. Mungu mwenyewe anaweka jambo hili wazi kabisa katika Amosi 3:1,2, "Lisikieni neon hili alilolisema Bwana juu yenu, enyi wana wa Israeli, juu ya jamaa yote niliowapandisha kutoka nchi ya Misri, nikisema, ***Ni ninyi tu niliowajua katika jamaa zote zilizo duniani, <u>kwa sababu hiyo</u> nitawapatiliza ninyi maovu yenu yote***."

Lakini sasa, kosa ambalo wanalifanya hawa waandishi wa kisasa ni kule kuchukua baadhi ya mistari kutoka katika Agano la Kale, mistari ile inayohusiana maalum na wana wa Israel na Agano lao la aina ya pekee lililofanywa kati yao na Mungu, nao hulitumia hilo sasa kwa watu wote na katika nyakati zote. Basi kama mambo yako hivyo kama wafanyavyo hao waandishi wa kisasa, Je Mungu amewaahidi mataifa yote mengine nchi ya kaanani iwe milki yao na urithi wao kama alivyowahi kuwafanyia hao wana wa Israel? Je, mtu yeyote leo, anahitajika kutahiriwa ili aupate wokovu? Kama jibu lako kwa maswali haya ni "sivyo", kwa nini basi mambo hayo yasiwe hivyo hivyo hata leo? Haya basi, ni kwa sababu hizo hata na sisi leo tunapaswa kuyakataa mafundisho hayo za kisasa ili tupate kupona. ***Mafundisho hayo hayawezi hata kupambanua kati ya Agano la Kale na lile jipy, kati ya Israel na mataifa mengine, kati ya mwili na Roho na kati ya kanisa na ulimwengu!*** Mungu hajawahi kujifunua mwenyewe kwa mataifa mengine kama alivyowahi kujifunua kwa wana wa Israel. Na kwake yeye aliyepewa zaidi, yanahitajika mengi zaidi. Kama vile tulivyokwisha kuona kwamba Mtume Paulo akisema kuwa Mungu alijifanya kama haoni wakati wa ujinga kati ya mataifa, lakini alitegemea mengi zaidi kutoka kwa Israel kiasi kwamba hata Yesu akaulilia Yerusalemu

kwa ajili ya ugumu wa mioyo yao. Alikuja kwa walio wake nao walio wake hawakumpokea. Mungu alikuwa na matazamio makubwa kutoka kwao kama watu wake yeye mwenyewe, na kwa kadiri walivyoweza kumkataa basi bila shaka hukumu yao ingepaswa kuwa kubwa zaidi juu yao. *Fursa yao ilikuwa ni ya aina ya pekee kwao na wala haikuwahusu mataifa mengine yoyote yale (isipokuwa wengineo wangeweza kujiunga nao), kwa hiyo hukumu yao pamoja na adhabu yao ingekuwa ni aina ya pekee kwa sababu ya Agano ambalo Mungu alikwisha kufanya nao.*

**Kanuni ya Uhalisi wa Ujinga katika Maandiko**

Unazitegemeaje nchi za wa mataifa ziweze kumwabudu "Bwana Mungu wao" kisha wasiweze kujiingiza katika masanamu yao *wakati tayari wao walikuwa wakiziabudu sanamu zao wakati wa ujinga wao*. Na kwa ujumla walikuwa hawakumjua Mungu wala amri zake, wala sheria zake hazikufunuliwa kwao wala hawajaingia katika Agano pamoja nao! Wangewezaje kulivunja agano ambalo sio lao? Ambalo kwao wao walikuwa ujingani? *Hawakuwa washiriki wa baraka zake zile za aina ya pekee, watawezaje sasa kuishiriki hukumu ya aina ya pekee ambazo zilikusudiwa kwa wana Israel pekee?*

Ukweli wa mambo hayo yote, unatolewa wazi na Mtume Paulo katika zilenyaraka zake kwa Warumi Rumi.3:20; 4:15; 15:13; 7:17. Ijapokuwa yeye alizijua sheria (torati) kama Mfarisayo bado hapo hapo, alikuwa yupo katika hii kanuni ya ujinga halisi. Na kwa mapenzi yake Mungu tu, Mtume Paulo alipokea neema na msamaha wake bure, analieleza jambo hilo yeye mwenyewe katika 1Tim1:13, ambapo anaeleza kuwa "…ingawa hapo kwanza nalikuwa mtukanaji, mwenye kuwaudhi watu, mwenye jeuri; ***lakini nilipata rehema kwa kuwa nalitenda hivyo kwa ujinga*** na kwa kutokuwa na imani." Ndani ya muda huo wa ujinga wake yeye alikuwa hamuasi Mungu kwa makusudi au kwa kudhamiria. Hakujua kuwa kwa kufanya kosa alikuwa akimpinga Bwana, Mtd 9:5. Na mafunuo hayo yaliuhuzunisha sana moyo wake. Hivyo kwa kweli ndivyo ilivyokuwa; ilimjia kwake kwa hofu kubwa na kwa sababu ya hilo aliipokea neema ya Mungu na msamaha bure, na wala hakutendewa kama mmojawapo ambaye kwa makusudi ameyafedhuli mapenzi ya Mungu.

Yesu Kristo analielezea jambo hilo kwa uwazi pia katika Luka12:47-48 "…Na kila aliyepewa vingi kwake huyo vitatakiwa vingi." Na wale wote wanaoyajua mapenzi ya Mungu kisha wasiyafanye watapata hukumu kali zaidi, kuliko wale wanaovunja amri za Mungu katika ujinga wao. Ukweli huo unawekwa wazi zaidi pale Mtume Paulo anapohubiri kwa mataifa katika Mtd 14:15-17, ambapo anaelezea kuhusu Mungu, "…ambaye zamani zilizopita ***aliwaacha mataifa yote waende katika njia zao wenyewe***". Na katika ule mstari wa 17, Mungu ***hasemi*** kwamba, "kwa hiyo wameshikwa na laana yake kwa sababu ya zinaa ya mababu zao." Basi sasa kinyume chake, Mtume Paulo anawawekea wazi juu ya jambo hili kuwa kwa hakika Mungu amebariki kwa mambo ya kimwili (kikawaida), akiwapatia watu mvua, pamoja na chakula. Na katika Mtd 17:30 hapo anawaonya juu ya kuyaabudu masanamu. Angeweza kuwaambia hapo kuhusu kuja kwa laana ya Mungu ni ya watu wote waabuduo sanamu (iwapo hilo lilikuwa ni jambo la ukweli kwao). ***Lakini Mtume Paulo hakuchukua fursa hiyo ili kuyafanya kama hivyo***. Badala yake sasa anasema, ***"...Basi zamani zile za ujinga, Mungu alijifanya kama hazioni, bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu". Hapo, Mtume Paulo hatoi laana ya sheria ya Musa katika mazingira hayo, hafanyi hivyo hapo wala pale anaziandika nyaraka zake kwa watakatifu.*** Hawaonyi wala hawafundishi kuwa laana ya Agano la Kale inawahusu wao pia. Ni tofauti iliyoje katika mafundisho ya Agano Jipya na yale mafundisho yao ya kisasa pamoja na kasoro zake. Kwa hiyo hapa tunaona kutoka katika maandiko hayo yote kwamba pale ambapo watu hawana sheria na wala hawazijui sheria wanatenda katika uhalisi wa ujinga wao wa kutokuyajua mapenzi ya Mungu, hapo Mungu anakuwa hawahesabii hizo dhambi zao walizozitenda katika uhalisi wa ujinga wao wa kutokuijua Rumi 4:15; 5:13 (ijapokuwa dhambi halisi zinatakiwa kufidiwa, lakini hii sasa ilitolewa na Mungu mwenyewe kupitia mwana wake kwa yeyote yule aaminiye). Wala hawawezi (kwa majaliwa ya Mungu) wakapata hukumu yake kwa maana ile ile kama ambavyo ingestahili kuipata watu wale ambao wanayajua mapenzi ya Mungu na wamedumu katika ushirika wa kiagano pamoja naye.

Hebu tukumbuke kwamba ilikuwa ni kule kukataa kwa mara nyingi kwa wana wa Israel kwa lile toleo la namna ya pekee ya Mungu ambalo lilisababisha wokovu wa bure na baraka za ajabu za kuja kwake Mungu kwa mataifa (Rumi11:11,12,15). Kwa hiyo ile hukumu ya wana Israel ya kulikataa lile Agano la pekee maalum la Mungu pamoja nao ilisababisha kutuletea sisi leo baraka zetu. Ndugu msomaji, nadhani unaweza sasa kuona jinsi uhusiano na Mungu ulivyokuwa ni wa tofauti kati ya mataifa ambayo hayakuwa katika maagano na Mungu na ile ya Israel ambao wao walipata fursa hii ya kupokea Agano la kipekee na Mungu? Kwa hiyo ndiyo sababu haishangazi kuona Paulo anasema "***lolote lile ambalo linatajwa na sheria, linasemwa hivyo kwa wao walio chini ya sheria."*** Kwa maneno mengine tungesema kuwa, sheria inawahusu wale tu walio chini ya sheria au kwa wale ambao wanapenda kujiweka wenyewe chini ya sheria, kama ilivyokuwa kwa baadhi yao walivyofanya katika makanisa ya kule Galatia na kama hawa waalimu wa kisasa wanavyotutaka sisi tufanye! Tumeona kuwa mataifa hayakuwa chini ya sheria kwa sababu wao

hawakuwa katika maagano na Mungu wala hawakuzijua sheria zake Mungu. Na sisi leo, tumekwishaona kuwa wakristo hawawi chini ya sheria kwa kuwa sheria inaweza tu kutuhukumu, na Yesu alikufa ili kutukomboa kutoka katika laana ya sheria!

Hao wamataifa hawakuwa chini ya sheria na kwa hiyo hawakuwa na ufahamu huo wa dhambi ambao unaletwa na sheria (Rumi 3:20; 7:7). Hii haimaanishi kwamba wao walikuwa hawana dhambi au hatia. La, hasha! Kwa sababu maandiko yanafundisha kwamba, binadamu wote wametenda dhambi, wanayo makosa na wanahitaji wokovu. (Rumi 3:19; 5:12). Pia mistari hiyo hapo juu inatufundisha kuwa, binadamu hawana udhuru kwa sababu wameumbwa na Mungu ili wamjue na kuzitambua nguvu zake na uungu wake kwa kupitia mambo yale aliyoyaumba Rumi 1:18-25. Tukisha kuwa tumeumbwa na Mungu, na kumjua Mungu, haishangazi kuona kuwa wamataifa wanayo mioyo pamoja na dhamira inayowashuhudia pale matendo yao yanapokuwa ni ya uongo au ya ukweli. Kwa hiyo Mtume Paulo anasema kuwa mataifa ambao hawazijui sheria, wanapoyatenda matendo ya kawaida yaliyomo katika sheria, hii inaonyesha kazi ya sheria iliyoandikwa ndani ya mioyo yao (Rumi 2; 14-16). Lakini bila shaka hapa Mtume Paulo anazungumzia kuhusu dhamira zetu zinazotuhukumu kuhusiana na haki ya kimsingi ambayo hiyo kila mtu amezaliwa nayo; hazungumzii kuhusu ile sheria ya ki-Musa pamoja na zile taratibu zake za kusherehekea kwake. Hivyo kila mtu atahukumiwa kulingana na matendo yake (Rumi 2:6-9); hapo haijalishi kama ni Wayahudi au ni wamataifa. Na wale wote ambao wametenda dhambi nao watahukumiwa.

Kwa hiyo, ili kuponya na kuokoa wote Wayahudi kwa wamataifa kutoka katika dhambi pamoja na hukumu zake hata kama ni chini ya sheria au la, Yesu Kristo akaja! Sheria ni takatifu, njema na ni yenye haki (Rumi 7:12), lakini matumizi yake ndani ya maisha yetu isingeweza kutufanya tuwe watakatifu, watu wenye haki na wema. Njia pekee ambayo kila mmoja wetu anaweza kuitimiza ile haki inayotakiwa na sheria – haijalishi kama ni ile haki inayoshuhudiwa na dhamira yako au ile haki iliyotakiwa na sheria za Mungu za Agano la Kale; isipokuwa ni katika imani ndani ya Bwana Yesu Kristo!

**Kumb. 28**

Kama tulivyokwisha kuangalia, sura nyingine ambayo hawa waandishi na wahubiri wa kisasa wanayoipendelea sana kuitumia, na ambayo ndiyo jiwe la msingi la mafundisho yao ni Kumbukumbu ya Torati sura ya 28:(45). Kutokana na sura hiyo, ambayo hupatikana katika Agano la Kale, wao wanataka kutuambia kuwa sisi kama wakristo leo, tunaweza kuteswa na kubanwa na laana yoyote kati ya laana hizo zilizotajwa katika sura hiyo hapo juu kwa sababu ya dhambi za mababu zetu. Wanaendelea kufundisha kwamba sio tu kwamba tunaweza kuendelea kuteswa kwa dhambi za mababu zetu hadi kufikia kizazi cha nne kurudi nyuma yetu, bali zaidi ya hapo – nyuma zaidi kufikia miaka mia au hadi elfu. Habari hii kwa ujumla wake ni udanganyifu wa hali ya juu na uliokithiri. Hata tukilinganisha na maandiko wanayoyatumia katika kitabu cha Kut. 20:5, Mungu alitaja kwamba, hadi kizazi cha nne. Lakini wao hata hawafikirii jinsi wanavyolichafua neno la Mungu na kuzitumia hoja zao binafsi wao wenyewe. Wanasema kuwa, ikiwa kila kizazi hakitatubu na ikiwa vizazi vingi vitaendelea na zinaa kinyume na Bwana, ndipo, eti hiyo idadi ya vizazi vinne vilivyotajwa na biblia vinajizidisha vyenyewe mara idadi nyingi zaidi, ili kwamba wewe uweze kudhurika kwa dhambi zilizotendwa miaka elfu kurudi nyuma!

Ni upuuzi gani huu! Huo ni ushirikina ambao umewaganda kiasi kwamba sasa wanalikataa neno la Mungu na badala yake wao wanajitungia mtindo wao wa mafundisho! ***Kadhalika kwa kufanya hivyo wanakuwa wakiitukuza sheria kinyume na neema na wanaitukuza hukumu ya Mungu dhidi ya rehema. Haitushangazi, kwa sababu tumekwisha kuona kuwa mafundisho hayo yanalenga kutuweka chini ya sheria; maana yake ni kutuweka chini ya hukumu.***

Lakini sasa, hata hiyo sheria yenyewe tu inasemaje? Mbali ya mipaka wanayoiwekea kwamba hadi kizazi cha nne, lakini pale katika ule mstari unaofuatia tu wa Kut. 20:5 unatuambia wazi kuwa, "***nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao*** na kuzishika amri zangu"? Na katika Yakobo 2:13 tunaelezwa kwamba, "Huruma hujitukuza juu ya hukumu na baraka zake zimemwagwa kwa wingi na zaidi kuliko hata laana zake" Unaona! Huo ndio ufunuo unaopatikana kutoka sehemu zote mbili - Agano la Kale na lile Agano Jipya. Sasa tunapoitazama Kumb.28 tunakuta kwamba *laana inajihusisha na Agano ambalo lilifanywa kati ya Mungu pamoja na watu wake Israel*. Sasa walimu hawa wanaichukua sheria kwa namna ya pekee ambayo ilisimikwa kwenye agano la aina ya pekee kati ya Mungu na watu wake ambao ni wa aina ya pekee Israel, na ***wao huitumia kwa watu wote na wakati wote. Huitumia hiyo kwa waaminio na kwa wale wasioamini pia.***

Lakini katika Mtd. Sura ya 14 na ile sura ya 17 kama tulivyokwisha kuiona, Mtume ***Paulo*** anapohubiri Injili kwa mataifa, ***hafanyi tamko la aina hiyo***, wala haja hiyo au matumizi ya sheria. ***Kinyume chake*** kama

tulivyokwisha eleza, Mtume Paulo anatangaza kuwa “Mungu alijifanya haoni wakati wa ujinga” naye amewabariki badala ya kuwahukumu kwa ajili ya dhambi zao kama walivyostahili kwa wakati ule. Kwa sababu yeye alitambua kuwa, wao walikuwa hawana habari juu ya sheria zake Mungu na tabia yake kama vile ilivyo kwa wana wa Israel wenyewe, ambao kwao Mungu amejifunua kwa neno lake na mafunuo mengine ya aina mbalimbali pamoja na madhihirisho. Kut 20:5 unatueleza kuwa mtu asiyetubu, yule mtu mwovu (mtu yule ambaye humchukia Mungu) wasipotubu, watavuna na watapatilizwa kwa dhambi za uasi wa mababu zao hadi kufikia kizazi cha nne. Lakini hapo hapo tena, kwenye ule mstari wa 6 unatuambia kuwa, ikiwa mtu atamgeukia Mungu na kumpenda ndipo Mungu atazionyesha rehema zake zenye kuzidi kusiko na ukomo.
Hatulioni dokezo lolote pale la mpango wa Mungu wa kuwafuatilia watu kwa laana kana kwamba Mungu ni adui, iwapo tu mtu huyo mara moja atatubu na kumgeukia Bwana kwa moyo wake wote. Kwa sababu, kama tulivyokwisha sema kwamba, Rehema hushangilia juu ya hukumu na zaidi ya yote huo ni ufunuo wa aina ya pekee kabisa ambao Musa aliupokea kwa tabia ya Mungu pale mlimani Sinai. Na jambo hilo hilo limefunuliwa pia katika Agano Jipya kwa mfano, kwamba Mungu ni “mwingi wa huruma ni mwenye fadhili si mwepesi wa hasira mwingi wa rehema na kweli”, Kut. 34-6-7. Na kutokana na mstari huo hapo juu, haileti ugumu wowote ule kunukuu mistari mingine mingi kutoka katika Agano Jipya ambayo ndiyo inatangaza ukweli unaofanana na hiyo hapo juu na ule ujumbe wake, kama vile Yoh. 1:17; Rumi 2:4; 15:5; 2Kor 1:3; Efs 1:6,7; 2:4:7. Kama vile ilivyo, ni jambo la kutisha sana kwa hakika kuona watu hao wanayatumia kwa makosa hizo laana pamoja na hukumu zake zote zilizotajwa katika Kumb.28. Wanawatumbukiza wakristo katika matumizi ya laana hizo, ijapokuwa nao wanakuwa wamekwisha tubu, wamemgeukia Bwana na ni watu wanaompenda Kristo.

Lakini katika hiyo Kumb.28 hizo laana zilizoandikwa humu zinawahusu Waisrael wale ambao hawajatubu dhambi zao, na hii ina maana kwamba ikiwa kizazi kimoja *kitaendelea kudumu katika uasi* na *wao wanakataa kuzikiri dhambi zao* na kumgeukia Bwana kwa toba, ndipo na hizi hukumu pamoja na laana zinazidi kulundikana kwa kadiri kizazi kimoja kinavyoendelea katika uasi na dhambi za kizazi kilichopita. Katika ule mstari wa 20,45 na 62 kwa mfano, tunaendelezwa kwamba, laana hizo zitawajilia Waisrael iwapo watakuwa wamefanya uovu na ikiwa hawatazitunza amri zake na iwapo watakuwa wanamkataa Bwana Mungu.
Laana hizo zitawajilia wana wa Israel kwa sababu ya kiburi cha kutokutii kwao. Laana haiwezi kufanya kazi yake ikiwa Israel anatembea katika utii kwa Mungu! Hivyo ndivyo tunavyoambiwa na kuona ilivyo pale katika Kumb.28. Tunaona pia kuwa sura hiyo inaenda sambamba na mambo ya Walawi sura 26 ambapo hapo panajaribu kuweka jambo hilo wazi zaidi. (Tafadhali utazame makala ya kwanza, utaona jinsi jambo hili ililivyofafanuliwa).

Hukumu ya Mungu (laana) sio majanga yanayojiachia tu pasipo kusudi kana kwamba ni adhabu isiyo na mwisho juu ya vizazi zinavyoendelea kuja kwa sababu ya kutokutii kwa kizazi kimoja. Hapana. Hapana kabisa, na wala haiwi hivyo hata kidogo! Hebu jisomee ile Walawi 26 yote, na utaona kuwa kwa kadiri kizazi kimoja cha Israel kilivyoasi dhidi ya Bwana na kwenda kinyume na neno lake Mungu, ndipo Mungu alisema atatuma hukumu juu ya Waisrael ***ili kwamba Waisrael hao wapate kutambua ujinga wao ili wakatubu dhambi zao kumrudia Bwana Mungu. Ikiwa wataendelea kukaidi na kuasi atatuma hukumu nyingine ili kuwaleta kwenye ufahamu wao na toba. Hukumu ya Mungu kwa Waisraeli ilikuwa katika muundo wa rehema, na katika hilo, mradi tu Waisrael hawakusikiliza neno lake, Mungu alituma hukumu ya nje ili apate kuwa rejesha kwake. Na kama wataweza kumrudia Mungu ndipo watasamehewa, watasafishwa na kisha kuletwa katika ushirika wa wazi pamoja naye; pasipo hata haja ya kutafuta ukombozi kwanza toka kwa laana za mababu.*** Jambo hili limeelezwa kwa undani zaidi katika makala yangu iliyotangulia ambamo tulitaja mashauri ya Mfalme Hezekia na Yosia ambao walipogeuka kutoka katika dhambi za baba zao na kumgeukia Mungu. Wao hawakuhitaji kuachiliwa kwanza kutoka kwenye aina yoyote ya laana. Kutubu dhambi kunashughulikia pia madhara yote ya dhambi hizo, hiyo haijalishi kama laana hiyo ilianzia kwako au kwa wazazi wako. Toba mbele za Mungu ndiyo ukomo wa dhambi, laana pamoja na maumivu yake.

Hakuna salio au masazo yoyote yale ya dhambi au laana zinazoweza kubakia baada ya mtu kutubu. Katika lile Agano ambalo Mungu alilifanya na Waisrael laana iliwajia watoto wale tu ambao hawakutubu au taifa ambalo halikutubu, ***waliokuwa wanaendelea*** katika njia za uovu wa mababa zao. ***Lakini laana haikuweza kuendelea kuwafuatilia au kuwahimiza baada ya kuzikiri dhambi zao na wakatubu!*** Yale yote yaliyoandikwa katika Kumb.28 yapo wazi kabisa, kwa sababu kule *kuendelea kutokutii* kinyume na Mungu, Mungu angetuma hukumu maalum iliyo kali, lakini anafanya hivyo *akiwa na nia ya kuwarejesha Waisrael* walipofanya dhambi. Mungu aliwatumia manabii akiwaamsha mapema kabisa ili kuwatangazia dhambi zao na kuwaonya juu ya hukumu itakayowajia iwapo hawatatubu. Manabii wale waliwataka watu watubu na wamrudie Mungu ambaye atawapa msamaha usio na ukomo. (Isaya1: 18,19). ***Waisrael hawakuachwa tu katika hali ya kutokujua matokeo ya kutotubia dhambi zao na kwa nini Mungu alikuwa akituma hukumu ya namna hii juu yao***. ***Halikadhalika hawakuachwa katika hali ya mashaka yoyote juu ya nini***

***wanachopaswa kukifanya ili wapate kusamehewa kikamilifu*** na kwamba, ili wapate kutembea tena kwa upya katika baraka zake Mungu na kupendelewa naye. Walielezwa mambo hayo yote mara nyingi na manabii wale. *Sasa ni jambo la tofauti kabisa iliyoje kwa mafundisho hayo ya kisasa ambayo yanasema, eti laana kutoka mbali kitambo kilichopita, inaweza kutokea kwa ghafula bila kujua sababu yake na kwa vitisho vikubwa na ikitesa hata kama tutakuwa tumekwisha tubu na kumrudia Mungu.* Hali ya jinsi hiyo wanayotuelezea hawa waandishi pamoja na wahubiri wa kisasa kwanza haipo katika Biblia na wala hata haikujulikana katika Historia ya Israel! (Isipokuwa ikiwa unapenda, basi ni pale ambapo Mungu alipoendesha hukumu zake za mwisho za kuwatapanya Waisrael katika mataifa mengine). Walimu hao wa kisasa wanaendelea kutufundisha kuwa, eti tunapaswa kuangalia nyuma katika mambo yetu yaliyopita, pengine tutazame nyuma zaidi ya miaka hata mia moja, ili kukijua chanzo cha laana, eti hata hivyo inaweza kutuchukua miaka mingi ya "utambuzi" huo pamoja na maombi kabla mtu hajaachiliwa kutoka katika laana fulani!

Ni mafundisho ya upuuzi wa jinsi gani huu juu ya neno la Mungu! *Ni kweli kwamba Waisrael walipata hali nzuri zaidi chini ya Agano la Kale, kuliko hali yale ambayo sasa hawa walimu pamoja wahubiri wa kisasa, wanatafuta kutuweka sisi chini yake.* ***Katika Agano la Kale, sababu au kiini cha kutolewa hukumu au laana kilikuwa ni wazi kabisa***. Na watu wale ambao walitaka kutubu kwa kweli na kumgeukia Mungu, haikuwa ni kazi ya kubahatisha ikimhusisha kwanza ajue eti kama kwa nini laana, yaani, hukumu hiyo imemjia! Badala yake ***wao walielewa kikamilifu kile wanachopaswa kukitubia***. Manabii pamoja na torati iliiweka hilo wazi kabisa. ***Matengenezo yake yalikuwa wazi pia na kwa haraka mara tu baada ya toba***; walipokea msamaha na walirejeshwa kwenye upendeleo wa Mungu kama watu wake mwenyewe walio wa thamani. Mungu asifiwe!

Kristo leo, amekuhifadhia ule uhuru wako! Kwa mara nyingine tena tunaona hapa kuwa hawa waandishi wa kisasa pamoja na wahubiri wao wanafanya makosa mawili yenye misingi ya hatari sana. Kwanza kabisa, wao hawajatambua kuwa laana au hukumu zimefutiliwa mbali kabisa au zimefikia mwisho wake pale wakati wa kutubu. Hii ina maana kwamba ukomo wa laana au hukumu ni pale mtu anapotubu dhambi zake kidhati mbele za Mungu. Pili, halikadhalika watu hao hawatambui kuwa zile laana zote zilizomo katika Kumb.28 zinahusika na Agano ambalo Mungu alilifanya na Waisrael na kwamba laana hizo ni namna ya pekee kwa Waisrael, halikadhalika na baraka pamoja na ahadi zote zilikuwa ni namna ya pekee kwa Waisrael. Huwezi kujianzia tu na kuzitumia hizo hovyo hovyo tu kwa watu wote na kwa wakati wote na zaidi ya yote, kwa hakika huwezi kuzitumia hizo leo kwa wakristo waliokwisha tubu toka mioyoni mwao na wakaupata wokovu katika Yesu Kristo.

Hebu sasa hapa mwishoni niseme kwamba, kwa sababu yeye Mungu ni muumbaji wa wanadamu wote, kwa hakika anaweza akazungumza nao na kuwa hukumu kama vile tunavyoona katika matukio ya Agano la Kale. Lakini hata hivyo, alizungumza nao na kuwahukumu sio tu kutokana na Agano ambalo alilifanya na Waisrael,

Missing
but when iniquity increased to such an extent among a people or nation, then God found it necessary to judge it and bring its influence to an end on earth. We have examples such as, Sodom, Nineveh and Babylon. But there are no examples of these kinds of dealings with nations in the New Testament. Of course the accounts of the book of the Revelation are an exception but these relate to the final judgements of God on the world. Obviously, as God and Lord of all, who had created us to know Him, (Rom.1:18-21), God could both judge and pardon the peoples of this earth according to His own righteousness and mercy and according to the dispensation of the time.

bali pale uovu kati ya watu au taifa GAP haihitaji laana kwa kuihusisha na shetani kabisa;

**Laana ya Shetani**

Let us now consider what the Bible has to say about the devil and his work in this matter of curses.

Firstly, it is clear that the Bible doesn't mention curses in relationship to the devil at all. haimwonyeshi shetani binafsi akiimwaga laana kwa yeyote yule.

Biblia pia haitumii tamko hili "Laana ya shetani." Pengine unaweza kupenda kufikiri tukio la Ayubu ni tofauti na hilo, lakini kwa lile tukio la Ayubu, tunaona kuwa kile kilichomtokea hakikuwa ni laana ya mababu zake ambayo ilimjia juu yake. Hapana, haikuwa hivyo; bali hapo ili kuwa Mungu mwenyewe akiruhusu au hata akimtumia shetani ili kumjaribu mtu wake. Kuendelea kuileta imani yake ili iwe kama dhahabu. Mungu aliwaruhusu watu wake waweze kujaribiwa katika jangwa kwa kusudi hilo Kumb: 8 2,3. Pia Yesu aliongozwa

kwa Roho wa Mungu nyikani ***ili kujaribiwa na shetani***, na tunasoma kuwa Yesu alikwenda nyikani akiwa ***amejaa Roho*** Mtakatifu. Lakini maandiko yanasema kwamba, "…alipomaliza kila jaribu, Ibilisi akamwacha…Yesu akarudi ***kwa nguvu za Roho***." Luka 4:13,14. Yale majaribu yaliweza tu kumwimarisha na hii ndivyo maana ya majaribu kwetu sisi - ili kwamba tupate kukua katika kumjua na neema ya Bwana na katika imani kama vile Ayubu alivyosema pale mwishoni mwa majaribu yake "Nimekuwa nikisikia habari zako kwa kusikia kwa masikio, bali sasa jicho langu linakuona". Ayubu alikuwa katika ufahamu wa kumjua Mungu ndani ya majaribu hayo magumu; tazama pia kuwa katika habari hiyo, hata shetani mwenyewe anaomba kibali cha Mungu kabla hajamgusa Ayubu au mali zake anazozimiliki. Katika hayo yote ni Mungu ndiye aliye katika usimamizi na kusudi lake ni kumbariki Ayubu pia kwa vitu vingi kuliko vile alivyokuwa navyo hapo mwanzoni, sio tu kwa vitu vya nje, bali pia katika kuujenga ule uhusiano wake na Mungu.

***Tatizo lililopo kwa Ayubu na pengine hutupata sisi sote ni kwamba hatuelewi kwa nini tunaumia wakati fulani.*** Kunaweza kukatokea wakati wa shida au matatizo, au tunaweza tukaumia, lakini hapo tunakuwa hatujui sababu za kuingia katika hayo; na hatuwezi hata kuzitazama sababu zile za kiroho ambazo zinakuwa zinaleta mateso. ***Hicho ndicho kipimo cha imani ambacho kina thamani kubwa zaidi kwa Mungu kuliko hata dhahabu,*** 1 Pet1: 5-9 – yaani, ***kuteseka pasipo kujua sababu zake kwa nini*** na kisha kumtegemea na kumpenda Mungu katikati ya hayo yote, huko ndiko kumwabudu Mungu na ambako kunaleta baraka zisizo na ukomo. Iwapo tutauruhusu uvumilivu ufanye kazi yake njema ndani yetu kama vile asemavyo Yakobo, (Yak1: 2-4). Sisi sote tunapitia katika majaribu ya aina mbalimbali ambayo ndiyo sehemu ya Mungu kwa ajili yetu. Ikiwa Ayubu angeujua sababu ile ya mateso yake - yaani, Mungu alikuwa upande wake Ayubu na kwamba alikuwa anamruhusu shetani ili kupima unyoofu wa Ayubu; na wala mateso kwa Ayubu hayakuhusiana na chochote kile cha aina ya adhabu kwa ajili ya dhambi - *kwa hakika asingeweza kuteseka kwa mawazo yasiyo ya lazima kuhusu Mungu pamoja na mateso yake yeye mwenyewe.* Lakini hakuna aliyejua hali ya nyuma ya kiroho kwa mateso hayo ya Ayubu, na hivyo ndivyo inavyokuwa kwa majaribu kwetu sisi sote.

Kama vile hapo ilivyokuwa, sio tu kwa ajili ya Ayubu isipokuwa na kwa marafiki zake pia ambao hapo kwanza, wao walifikiri wanaelewa ipasavyo juu ya kile kilichokuwa kinasababisha mateso kwa Ayubu. Marafiki zake walimjia wakiwa wamejaa elimu yao juu ya theologia, ***mara moja tu wakamwambia kuwa, anaumwa kwa sababu ya dhambi! Halikadhalika hawa walimu na wahubiri wa kisasa wanaofundisha na kuhubiri juu ya "laana".*** Wao wanafikiri kuwa wanayo macho ya kuona ndani ya mwendo wa nyuma wa kiroho ili kujua kwa nini watu wanateseka juu ya mambo fulani fulani. Na kama wao wangekuwepo nyakati hizo pale pamoja na Ayubu, ***bila shaka yoyote ile wangeweza kutwisha mzigo na kuuletea mateso moyo na akili za Ayubu huku wakimtumbukizia mawazo kuwa hiyo, ni laana ya mababu zake ndizo zinazomsababishia kuteseka huko kote.*** Tukitazama katika Kumb.28 wangeweza kujishawishi wao wenyewe na pia wangeweza kumshawishi Ayubu kuwa hapo palikuwa na ushahidi wa kutosha kuwa alikuwa chini ya laana - kule kuangamia kwa fedha zake, hiyo ilikuwa ni dalili ya wazi ya laana (kwa mawazo yao)! Kumb.28: 18,32,41. Na utawezaje basi sasa kutotia shaka kuwa yuko chini ya laana, wakati mtu huyo anateseka kwa magonjwa yale yale yaliyoelezwa katika sura ile ya Kumb.28. mstari 22,35? Kama waandishi hawa na wahubiri hawa wa kisasa wangekuwa pale mbele za Ayubu na hasa kama wangekuwa nacho kitabu cha Kumbukumbu la torati mikononi mwao ndipo, na kama wafanyavyo siku hizi za leo, hakuna shaka yoyote kuwa hayo ndiyo yangekuwa ni mabishano yao mbele za Ayubu. Kwa kufanya hivyo watu hao kwa hakika wangekuwa wamefanya makosa makubwa yasiyo na kifani!

***Hapo, ushauri wao ungekuwa umeongeza tu mateso zaidi kwa Ayubu***; kwa kumwachia mawazo tu ya kwamba ni laana ndiyo iliyokuwa inamshikilia juu yake na hata penginepo wangetumia miaka mingi ya kutafuta kugundua kwa kupitia "maombi" na "neno la maarifa". Ni mababu wapi wangepaswa kulaumiwa hapo? Yote hayo ni bure tu, kwa kuwa hayo hayakuwa ndiyo sababu ya mateso yake wangeweza kujaribu kumloga Ayubu kwa huo udanganyifu wao, Gal.3:1. ***Na kwa hiyo hawa walimu wa kisasa pamoja na washauri wenye kutaabisha (waongo) wanastahili kukemewa na Mungu, kwa sababu wamemwakilisha Mungu vibaya na kwa hiyo wamemtenda dhambi Mungu, ni vile vile kama wale rafiki zake Ayubu 42:7-8***. Ni kweli kuwa hawa walimu wa kisasa wanamwakilisha vibaya Mungu, wanamwekea mifano isiyolingana na tabia yake Mungu mwenyewe - wala hailingani pia na mafunuo ya kweli ya Biblia, wanachokifanya ni kuwapoteza na kuwaloga watu wa Mungu na kuwatumbukiza ndani ya mateso makali pamoja na vifungo. Wanamtenda dhambi Yesu na mwili wake pia! Kuhusiana na lile suala la Ayubu pamoja na ***Kumb.8: 2,3; Rumi 5:3-5; Yak.1:2-4 na 1Pet1: 5-9, inatuonyesha jinsi ilivyo ni muhimu kwetu kutofikiria mara moja kwamba tatizo lolote au ugumu ni matokeo ya dhambi au laana; au shetani tu alipata nafasi katika maisha yetu***. Hapa tunakaribia kwenye ukweli wenye muhimu ulio katika maandiko na kuhusiana na kujishughulisha kwa Mungu kwa ajili ya watakatifu wake. Matatizo yanatujia, na wakati mwingine tunateseka lakini Mungu anayaruhusu mambo hayo kwa wakati wake ili kututhitisha, kutuimarishia Imani zetu katika yeye, ili kwamba tupate kukua katika neema yake na ile kweli ya ufahamu wa Mungu. ***Na***

***kinachofanyika katika hayo mafundisho yao ni kuwachanganya watu na kuzitia giza akili za watu wengi kuhusiana na Mungu na namna anavyotushughulikia, kwa kuwa hii inawaongoza watu ili waione laana kuwa ndiyo chanzo cha kila tatizo wanalolipata.***

Tafadhali usinielewe vibaya hapa sisemi kwamba kila kitu kinachomtokea mtu basi kimetumwa na Mungu, kwa mfano - dhambi sio mapenzi ya Mungu, na kamwe yeye Mungu hatafanya chochote kile kwetu ambacho kitatupelekea kutenda dhambi, Yak1:13. Yale majaribu (mitihani) yanayoruhusiwa na Mungu yanakusudiwa kwetu ili kutuingiza ndani zaidi katika kumfahamu Mungu na katika neema yake pamoja na upendo wake! Wala kamwe hayakusudiwi kutuangusha. Iwapo tunayo mawazo mabaya au hisia mbaya dhidi ya watu wengine kama vile, uchungu na kutosamehe; hii ni kwa sababu ya ulafi wetu, tabia za kimwili au dhambi - tunayakataa au kutoyatii yale ambayo Mungu amekwisha yafundisha wazi ndani ya neno lake. Na kama ndoa inavunjika, haivunjiki kwa sababu hayo ni mapenzi ya Mungu au eti ni kwa sababu huyo Mungu ametuma laana juu yetu kwa ajili ya dhambi za mababu zetu, bali ni kwa sababu mmoja wa wanandoa hao yeye binafsi ni mtu wa mwilini tu na zaidi ya hayo ni mtu wa tabia zenye kujipendeza. Jawabu kamili la wanandoa hao hapo *ni kuzitubia dhambi zao za kujipendeza na wala sio kuanza kuangalia laana* na kuiona kuwa ndiyo chanzo cha ubinafsi wako, kama vile hayo mafundisho yao ya kisasa yanavyotutaka sisi tuamini hivyo.

Kama tutarejea kwenye somo letu halisi, nilisema kuwa maandiko hayatumii tamko hili - “laana ya shetani”. Shetani mwenyewe haonyeshwi kuwa ni mfano wa kumlaani yeyote yule. Hata hivyo kile tunachoweza kukiona ndani ya Biblia ni kwamba, kwa hakika wapo ambao wanapenda kuwashawishi watu wengine na hata kufanikiwa kuwawekea laana juu yao na ili kufanya hivyo watu hao wanazitumia nguvu za ushirikina, wanajiingiza katika mambo ambayo yamekatazwa na Mungu. Wanatumia milki ya kimapepo na ndipo baadaye wanakuwa ni mawakala na wajumbe wa shetani katika ile, Mtd13:6-12. Mtume Paulo anawasili huko Pafo, kulikuwa na mtabiri wa uwongo ajulikanaye kwa jina la Bar-Yesu, ambaye anayapinga mahubiri ya Mtume Paulo, na ambaye pia anajaribu kumzuia makamu wa Pafo ili asiweze kuamini… Mtume Paulo anamkemea mtu huyo anamwita “ewe mwana wa shetani”. Kwa lugha hiyo, Mtume Paulo anaonyesha kuwa mtu huyu ni chombo cha shetani kwenye hali hiyo.

Katika Mtd 8:9 tunazisoma pia habari za Simon mchawi ambaye aliutumia ulozi wake ili kuwaloga watu wa kule Samaria; kwa hiyo ipo mifano ya watu ambao walitumia nguvu za ulozi na kuwashawishi watu na kujifanya ni watu maarufu. Na hizo nguvu za uaguzi walizokuwa wakizitumia huwafanya kuwa ni mawakala halisi wa shetani. Lakini, ukiangalia kwa makini sehemu hiyo, utaona kuwa wale watu waliokuwa wanashawishiwa ni wale wasioamini! Hata hivyo ndani ya Biblia upo mfano mmoja, na kwa kweli ni mfano mmoja tu wa mtu fulani aliyejaribu kutumia nguvu za uaguzi ili kuwawekea laana watu wa Mungu. Hilo pia ni jambo ambalo nalo linahitaji maelezo marefu. Kwa hiyo tunapaswa kuangalia kwa makini sana juu ya jambo hili ili kuweza kuona Biblia inafundishaje juu ya jambo hili la kipekee.

**Balaam na Hesabu Sura ya 22 – 24**

Hapa tunakutana na mtu maarufu kwa matumizi yake ya nguvu za uaguzi; ambazo anazitumia ili kuwaloga watu. Hakuna mtu aliyeweza kulinganishwa naye katika mkoa wake wote na alikuwa akilipwa fedha nyingi sana ili kutekeleza hiyo kazi yake, na hicho ndicho tunachokikuta katika habari hiyo.
Baalaki yule mfalme wa Moabi anawatuma watu kwa Balaam wakiwa wamechukua fedha za malipo ili aweze kuwalaani Israel. Kama Balaam angekuwa ni nabii wa kweli angeweza kukitambua kile ambacho Mungu amewatendea Waisrael na kwamba angeona kuwa hao Waisrael walikuwa ni watu wake maalum na hivyo wala isingempasa yeye kushiriki katika jambo hilo. Lakini sasa, inapasa iwe wazi kwetu kwamba - Balaam alikuwa ni mtu mbaya ambaye alizipenda sana fedha. Yeye aliweza hata kufanya mawasiliano na ule ulimwengu wa kiroho ijapokuwa yeye hakuwa ni mtu wa kiroho! Alitumia uwezo wake kwa kujipatia faida yake yeye binafsi, na hapo maandiko yanaweka mkazo maalum kuwa kama mfano wa mtu asiye na haki, (Yoshua 13:12, 2Pet2:15; Uf.2:14). Kwamba yeye ni mtu mjinga kabisa na anaonyeshwa na Mungu kwa kuufungua mdomo wa punda ili kumkemea Balaam, kwamba yeye anayapinga mapenzi ya Mungu. Hilo linaonyeshwa kwake kwa ukweli kwamba Mungu amemtuma malaika ili kumwua. Lakini pale mwisho, Mungu anamtumia mtu huyu kwa makusudi yake ili kuonyesha ulimwengu pamoja na wale wenye uwezo wa uaguzi kwamba watu wa Mungu ni watu maalum, ni watu wake mwenyewe amewakomboa kutoka katika nyumba ya vifungo kwa damu ya Mwanakondoo. Mungu angeitukuza neema yake kwa Israel na upendeleo wake wa ki-mungu na ulinzi juu yao!

***Sasa, kilitokea nini pale Balaam alipotaka kuwalaani Waisrael? Hawezi kufanya hivyo***! Hakuna nguvu zozote zile za kiuaguzi ambazo angeweza kujaliwa kuzikusanya pamoja ndani yake na kwa kupitia kuwepo kwake ambazo zingefanikiwa kuwagusa watu wa Mungu; siyo tu kwamba alishindwa kabisa, bali Mungu

aliigeuza ile laana kuwa ni baraka. Hes 23:16-20. Na Balaam mwenyewe analitangaza neno la Mungu pale kwenye ule mstari wa 23 ambao kwa hakika unashangaza kwa ajabu kubwa na unatujenga kwa hali ya juu.

***“Hakika hapana uchawi juu ya Yakobo, wala hapana uganga juu ya Israel.”*** *Je, hiyo haikushangazi mpendwa wangu? Na ukumbuke kuwa hivyo ndivyo alivyosema Mungu kuhusu watu wake. Na hivyo ndivyo alivyofanya kwa ajili ya watu wake katika Agano la Kale, kabla Yesu hajafa pale Kalvari. Je, si zaidi sana kwamba hii ni kweli zaidi wakati huu wa Agano Jipya?*

Ambalo limenunuliwa kwa ajili yetu kwa damu ya Kristo! Kuna mfano huo mmoja tu ndani ya Biblia yote ambapo tunaona wazi mtu anayejaribu kuwalaani watu wa Mungu. Na Mungu mwenyewe anautumia mfano huo ili kutuonyesha wazi kuwa jambo hilo halikuweza kufanikiwa kufanya kazi na anaitumia ili kutufundisha kwamba; “hapana uchawi juu ya Yakobo wala hapana uganga juu ya Israel”.

Kama nilivyokwisha kusema kwamba Mungu aliwakomboa Waisrael kutoka kule Misri kwa damu ya Mwana Kondoo. Amewanunua. Walikuwa ni watu wake, na kama walikosea angeweza kuwahukumu kama atakavyoona yafaa. Hakuna mtu yeyote aliyekuwa na haki ya kumwibia Mungu ile hukumu ya watu wake mwenyewe! Na huo ndio ukweli halisi usio na ukomo kwao hao ambao sasa wamekombolewa kwa damu ya Yesu. Hakuna mtu yeyote yule awaye, mke au mume bila kujali uwezo wake wa kishetani alionao mtu huyo atakayeweza kuwagusa au kumdhuru mtu aliye ndani ya Yesu kwa kutumia nguvu hizo za giza alizonazo mtu huyo. Iwapo wewe ni mtu wa Mungu katika Kristo, basi hawana uwezo wala mamlaka juu yako.

Baadaye Balaam alimshauri Balak ili kuwaruhusu wanawake zao wajichanganye na Waisrael kwa nia ya kuwaondosha toka kwa Bwana na kuwageuzia kwa masanamu, (Hes. 25:1-3; 31:16). Hata hivyo hiyo haikuwa ni laana. Hizo zilikuwa ni mbinu za shetani za kuwageuzia mbali na Mungu wao wana wa Israeli ili wamkatae Mungu kwa kuwajaribu kwa miili yao. Lakini hebu angalia hapo pote kuwa pamoja na hayo yote ***ilikuwa ni Mungu mwenyewe aliyewahukumu watu wake***, ***na yeye ndiye aliyeamua hukumu hiyo iwe ni ya namna gani***. Hivyo naye aliwahukumu kwa lile walilolichagua wao wenyewe kulifanya na kisha kutenda dhambi; Na pamoja na hayo yote, bado Balaam hakuingia na laana baada ya tukio hilo la sanamu walilolifanya waisrael. Na muda mfupi tu baada ya hapo Balaam aliuawa na Waisrael.

*Kwa hiyo hayo yote yanaunga mkono juu ya yale niliyokuwa nikisema katika makala hii, kama vile si shetani wala si mtu yeyote yule awaye awezaye kuweka mkono wa laana juu ya mtu yule aliyekombolewa na damu ya Mwana Kondoo, na akazaliwa kwa Roho wa Mungu. Hayo yote yameonyeshwa wazi na kufundishwa ndani ya maandiko ya neno la Mungu.*

Hebu tazama kuwa, hata katika muda huo, ***haikuwa*** kama kwamba hao Waisrael walikuwa ni watu wanaojiheshimu kwa tabia za utakatifu zinazompendeza Mungu. Utaona kuwa katika Hes.21 wamemlalamikia Mungu, naye akatuma nyoka wabaya katikati yao; na katika Hes.25 Waisrael walitenda dhambi tena kama tulivyokwisha kuona. Kwa hiyo hata katikati ya kuanguka dhambini, bado Mungu aliendelea kuwalinda watu wake kutokana na laana; kwa sababu ijapokuwa walikuwa siyo watiifu wakati Fulani, bado ni watu ***wake***. Na kwa hiyo yeye ndiye anayepaswa kuwahukumu; na kama shetani alikuwa na sehemu yake katika hilo basi imekuwa hivyo tu kwa sababu Mungu mwenyewe amemruhusu kufanya hivyo, ili kutimiza kusudi lake Mungu mwenyewe. Bila shaka, hapa ***sisemi*** kuwa wewe utakuwa salama utakapokuwa umetenda dhambi! Lakini kama tunavyoona hapa, na hasa kama ilivyo ndani ya Biblia yote ni kwamba Mungu ndiye muhukumu wa watu wake na ni yeye ndiye apimaye jinsi gani yafaa kuwahukumu watu wake. Kwa hiyo hapa tunayo habari ya kipekee kuhusiana na jambo hili la laana na jinsi ambavyo nguvu za uganga na ulozi zisivyokuwa na uwezo wa kuwagusa au kuwadhuru watu wa Mungu. Kwa vyovyote vile jambo hili haliungani vizuri na mafundisho yale ya hao, walimu wa kisasa pamoja na mafundisho yao kuhusu laana.

Haya basi, sasa hawa walimu wa kisasa wanasemaje kuhusu sura hii? mwandishi mmoja maarufu sana, anayeandika sana habari zihusuzo “Laana” yeye anasema jambo fulani kama ifuatavyo, “Unaona, hata Mungu mwenyewe alitambua uwezo wa Balaam kulaani vibaya sana, kwa sababu ilikuwa lazima Mungu atumie nguvu za pekee kuweza kuingilia kumsimamisha. Kwa hiyo hata sisi wakristo tunapaswa kutambua uwezo wa watu wengine pia kulaani vibaya - ikiwa hatutakuwa waangalifu tunaweza kulaaniwa!” Hivyo ndivyo asemavyo huyo mwandishi wao. Kwa hiyo wewe unadhani mwandishi kama huyo anapata ujumbe gani ndani ya sura hiyo? Kwa kweli anapata kitu kilicho tofauti na cha kinyume kabisa ya yale ambayo sura hiyo inadhamiria kutufundisha au kutuonyesha. Kwa sababu Mungu hakuwaonya Waisrael kabla kwamba, “Haya Baalam anawajia” au hata labda kuwaonya kabla kuwa, walipaswa kuwa waangalifu juu ya hatari ya laana ya watu waovu. ***Hakuna sehemu yoyote ile ndani ya Agano la Kale au Agano Jipya ambapo Mungu anawafundisha watu wake kuwa laana ya watu waovu au ya mtu mwingine yoyote inaweza***

***ikawadhuru***. Mungu aliwaambia kuwa, Yeye atawahukumu iwapo hawatakuwa watiifu kwake. Wakati huo, hata Waisrael wenyewe hawakuwa na taarifa yoyote ile kuwa Balaam anajaribu kujitahidi kuja kwao ili kuwaalani. Kwa hiyo basi, kwa nini sasa sisi tuwe katika woga wa kuogopa laana ya watu?
Ukweli mwingine mkubwa ambao waandishi hawa wanaukataa ni kwamba - Mungu kwa niaba yetu amekwisha kuyaingilia hayo kwa nguvu za kipekee kabisa pale Kalvari. Hilo wanalikataa kwa nguvu zao zote! Hakuna laana ya watu waovu wala ya wachawi wala ya waganga kwa njia yoyote ile iwayo, ambayo inaweza kuwaumiza watu wa Mungu. Jina lake lisifiwe! Jambo hili lilikuwa ni la ukweli nyakati zile za Agano la Kale, basi ni la ukweli zaidi nyakati hizi za Agano Jipya. Lakini wao hao waandishi wa hapo hiyo inaonyesha kuwa eti sura hiyo inaonyesha kuwa watu waovu wanaweza wakatulaani iwapo sisi wenyewe hatukuwa waangalifu! Lakini pamoja na maoni yao hayo yote, bado sasa ***Yesu mwenyewe anasema kuwa, ikiwa mtu yeyote atawalaani, mbarikini!*** Yesu Kristo hakutoa uwezo wowote ule kwa ajili ya laana ya binadamu. Yeye hakuwahi kutuonya juu ya laana itokanayo na uwezo wa mtu kwamba inaweza ikatudhuru. Je unaweza sasa ukaona mwenyewe kuwa mafundisho yao hayo hayalingani kabisa na neno la Mungu? Kwa hiyo hapa tunayo sura ya habari yenye kututia moyo vilivyo kuhusiana na wokovu wetu kama watu wa Mungu na kuhusu malezi yake anayotutendea pamoja na ulinzi kwa ajili yetu. Badala yake sasa, hawa waandishi pamoja na wahubiri niliowaelezea hapo juu, wao wanaitumia habari hiyo ili kuwaongoza watu wengine ili waingie mashaka, hofu pamoja na kuingiza ushirikina ndani ya mioyo ya watu wa Mungu!

Tunao pia mfano wa mtu mmoja akiwalaani mmoja wa watu wa Mungu. Goliati alimlaani Daudi, kwa miungu yake; lakini tena hapo hapo hakupata mafanikio yoyote yale (1Sam 17:43), na ndani ya dakika chache tu huyo Goliati alichinjwa na Daudi.

Hapa Uingereza yapo makanisa yanayopata matatizo mbalimbali, na kwa sababu makanisa hayo yapo jirani na sehemu ambazo wachawi hukutana, baadhi ya wakristo wanashangaa iwapo kama matatizo ya makanisa hayo husababishwa na uchawi wao; au watu wanaojishughulisha na mambo ya uaguzi wakiziweka laana katika kanisa! Huo ni udanganyifu. Matatizo yanayoliandama kanisa leo, husababishwa na tabia za mwilini za wakristo waliomo kanisani humo. Iwapo wewe ni wa Mungu, huwezi kulalamikia tabia zako za kimwili juu ya shetani au juu ya laana itokanayo na uovu wa watu! Kwa udanganyifu huo tunaweza tu kumjaribu Mungu!

***Hakuna sehemu yoyote ile katika vijiji vyao, ambapo mitume wanakutwa wakishauri kuwa, tatizo lolote lile la kanisa linatokana na au hata linaweza kuwa linatokana na laana! Mara zote wao wanaelekeza kuwa ni tabia za kimwili za wakristo wenyewe kuwa ndizo chanzo cha matatizo yoyote yale; kwa mfano 1Kor. 3:3.***

*Na kama shetani anapewa fursa ya kudanganya au kuwashawishi, hii ni kwa sababu wakristo wao wenyewe wamempa Ibilisi fursa hiyo ya kuwadanganya hivyo*, *kupitia mlango wa tabia, zao wao wenyewe za kimwili*. 2Kor 11:3 inaelezea juu ya jambo hili kwa ufasaha zaidi. Mtume Paulo hapo hawaambii Wakorintho kuwa Ibilisi anashambulia mwenendo wao wa ukaribu na Bwana, na kwa hiyo wanapaswa kukemea vishawishi hivyo. Hapana! Yeye hafanyi hivyo; isipokuwa anawaambia kuwa hiyo yote inatokana na tabia zao za kimwili – wanayahukumu mambo kwa nje, 2Kor.10:7, kwamba wanampatia shetani fursa ya kuwadanganya 2Kor.11:4,13,15,19,20! Walipenda kuona uwezo na ishara zikitendeka pia walipenda kuona watu wale ambao wanajiinua wenyewe, hivyo baadhi yao watu wale hakupenda kuendelea kumsikiliza Mtume Paulo akihubiri –kwa sababu yeye alikuwa ni muungwana sana na mvumilivu 2Kor.10:1. Na hata baadhi yao hawakuweza kumtambua kuwa alikuwa ni Mtume, 2Kor.10:10; 11:5-7,16,13; 12:11,12. Na kwa sababu ya hizo tabia zao za kimwili, Wakorintho walikuwa tayari kuwapokea watu ambao walikuwa ni wadanganyifu na walimu wa uongo. Katika hali hiyo yote Mtume Paulo hawaagizi watu kumkemea na kumfunga shetani isipokuwa anaiagiza mioyo yao kwa kuitumia kweli ili kusudi waweze kuziachilia mbali tabia zao hizo za kimwili. Mafundisho mengi ya tofauti ya kisasa hupenda kutuweka tufanye “matengenezo ya kijinga” kushughulikia yale yaliyopita au hata kwa nguvu zinginezo zisizojulikana! Wanayaazima mawazo hayo kutoka kwa ulimwengu, kwa sababu ni kutokana na mawazo hayo hayo, ambayo yamepata ushawishi mkubwa sana katika jamii ya huko magharibi, na hata wakristo wengine wanajichukulia tu mawazo hayo na wanayatumia katika kuchafua Injili. Pale msalabani Yesu Kristo alikwisha yashughulikia mambo yetu yote yaliyopita pamoja na vishawishi vyake ikiwa ni pamoja na nguvu zote za shetani; nasi tumekwisha angalia katika sura zinazofanana zituonyeshazo hilo. Yeye Yesu, amekwisha kufanya kila kitu kwa ajili ya wokovu wetu ili kwamba tusipate kumlaumu mtu yeyote yule, kwa ajili ya tabia zetu sisi wenyewe za kimwili. Ikiwa tu watoto wa Mungu, basi ndipo jawabu letu ni toba ya ubinafsi wetu pamoja na dhambi. Ikiwa kama vishawishi vingine vimeingia katika maisha yetu kwa sababu ya dhambi zetu wenyewe na kutokutii, ndipo basi chanzo cha mizizi ya kila jambo bado ni ubinafsi wetu pamoja na dhambi na hiyo ndiyo tunayopaswa kuitubia. Ndipo hapo hivyo vishawishi vinginevyo navyo vitashughulikiwa pia.
Hapa tena naongelea kuhusu wale ambao tayari ni watoto wa Bwana. Lakini wale watu ambao hawajaamini ambao wanaweza kumrudia Bwana katika toba, hao wanaweza kwa hakika kuhitaji ukombozi huo kutokana

na nguvu za shetani pamoja na vifungo vyake. Na yapo mamlaka katika Jina la Yesu ili kuwaachia watu huru pamoja na kuwatunza katika uhuru huo. Hii haina maana kwamba kutenda dhambi sio jambo la hatari sana. Lakini sasa kile tunachokiona hapa ni kwamba, ijapokuwa Waisrael walikuwa si watiifu, Mungu hakuweza kuzikubali haki za Balaam ili kuwalaani. Ni Mungu pekee ndiye awezaye kuamua hukumu ya watu wake naye anafanya hivyo kufuatia mtiririko wa damu ile iliyomwagika pamoja na lile Agano walilolifanya naye.

Hebu nirudie kusema tena kuwa ikiwa hii ilikuwa ni kweli wakati ule wa Agano la Kale, basi si zaidi sana itakuwa ni kweli ya jinsi gani wakati huu wa Agano Jipya! Ninalieleza jambo hili kwa sababu waandishi hawa wa kisasa wanataka kutuambia kuwa mara tu mtu anapokuwa si mtiifu au anapokuwa ametenda dhambi kama mkristo, basi shetani anaweza kukuwekea laana. Sasa ni wazi kuwa hatupendi kumpatia yeyote yule sababu yoyote ile, ili asiweze kumtii Mungu, au kuwafanya wafikirie kuwa si jambo la hatari pale anapofanya dhambi.
Kama nilivyokwisha sema, ni jambo la hatari sana na pia kuna madhara yenye hatari sana, pale mtu anapotenda dhambi. Yatupasa tuwe ni watu watakatifu tunaoendeleza haki, upole na upendo. Na Agano Jipya linafundisha kwamba, kila mtu atavuna kile alichopanda. ***Lakini sasa badala ya kunukuu na kuyatumia maonyo na mausia yaliyoandikwa ndani ya Agano Jipya ambayo kwa hakika mengi yake yana mkazo wa kutosha, (Rumi 8:13; 1 Kor4:5; 2Kor.5:10,11; Gal.6:7,8; 1Tim.6:9,10; 2Tim.4:1; Hes.2:3; 10:26-31), wao sasa wanatupilia mbali lugha na mafundisho ya Agano Jipya na kinyume chake, wanatafuta kutujaza akilini mwetu kwa mawazo kwamba eti tutalaaniwa dakika yoyote ile iwapo hatutakuwa waangalifu!*** Huo ni uongo! Na matokeo yake ni kwamba wanaijaza mioyo ya watu kwa tabia za ushirikina na mawazo ya woga na hofu.

Kwa mara nyingine tena fikra za aina hii zinahusika tu na mila na desturi za kiuchawi wa vijijini, kuliko ambavyo ingeweza kutupatia afya na mausia na maonyo ya uhakika ya kibiblia. Je Mtume Paulo au Petro au Yohana wanatuonya namna hiyo? "Wapenzi ikiwa tutatenda dhambi, ndipo shetani anaweza kukuwekea laana; au pengine yawezekana ukavuna moja ya zile laana zilizoandikwa katika kumbukumbu ya torati." Je, haya ni mafundisho au lugha yao? Hapana! Tumekwisha kuelezea mbele kabisa maonyo yote yenye hatari yaliyomo katika Agano Jipya; lakini pia Agano Jipya hilo hilo linao uthibitisho na raha. Yohana mtakatifu anasema; "Wapenzi nawaandikieni ninyi mambo haya ili msitende dhambi, lakini ikiwa yeyote yule atatenda dhambi tunaye mwombezi kwa Baba Yesu Kristo mwenye haki." Agano Jipya linasisitiza pamoja na kutangaza utoshelevu wa wokovu wa Kristo usio na ukomo na ukichanganya na msamaha wa dhambi unaoendelea pale tunapozitubia. ***Walimu hao wanatukuza laana na sheria zaidi kuliko toleo la Kristo.*** Ikiwa utasoma Agano Jipya, utagundua kuwa Agano Jipya lililoanzishwa na Mungu kupitia Kristo, halichanganyi au kuendeleza matumizi ya laana ya Agano la Kale. Tafadhali ujisomee mwenyewe utaona kuwa si Yesu Kristo wala mitume wake wanaotumia lugha hii mahala popote pale na hawatoi maonyo ya laana kabisa! Halipo tamko lolote lile lililofanywa la muundo wa laana kwa dhambi. Ikiwa tutatenda dhambi tunaye mwombezi pamoja na Baba. Na Yesu anasema, "Wabarikini wanao walaani!"

Bila shaka katika haki yake Mungu na hekima yake anaweza akaingilia kwa hukumu ya muda katika mazingira, hasa kama kuna dhambi nyingi au kuna kupinga kwa dhahiri kinyume naye, pale kunapofanywa na hasa pale inapokuwa jambo hilo lina madhara au linashawishi watu wengine, (Mtd. 5:1-11; 1Kor.11:30; Uf. 2:20-23). Lakini hayo yote ni huruma za hukumu zake ndani ya mazingira maalum na wala sio matokeo ya mfumo wa laana iliyofunuliwa au kuelezwa katika Agano Jipya au la Kale. Kifo cha Bwana Yesu Kristo kimebadilisha mambo, ukichanganya na jinsi ambavyo Mungu mwenyewe anavyojishughulisha nasi hapa duniani.

Katika Agano Jipya kuna mikazo mingi ya uvumilivu wa Mungu na ustahimilivu wake ndani ya siku hizi za neema, ambazo zinapaswa kuwaongoza watu ili wafikie ile toba. Hilo ni jema zaidi kuliko kujiingiza katika hukumu. Watu wamepewa muda na wanategemewa kulifikia tangazo la Mungu la upendo na wokovu lililodhihirishwa pale Kalvari, (Rumi 2:4; 2Pet.3:9; Yak.5:6) - "Tulipokuwa tungali wenye dhambi, Yesu akatufia". Lakini pia ni uwazi usio na ukomo kwamba kwa dhambi zote pamoja na kutokutii ambako watu wanadumisha kufanya na hawataki kutubu, bado hukumu yao watu hao haijasinzia kabisa - inawangojea - 2Pet 2:3. Hata kama Mungu anaingiza hukumu yake ya muda (hukumu ile tunayoipata tukiwa hapa duniani) ndani ya maisha yetu, au la; lakini sote tutasimama mbele ya Kiti chake cha hukumu siku ile, ili kila mtu apokee hukumu sawa sawa na matendo yake aliyoyafanya. Huo ndio mkazo na msisitizo unaotolewa na Agano Jipya, ukituonya madhara yapatikanayo kutokana na tabia za aina hiyo katika siku ile ya hukumu. Hata kama Mungu ataiingiza hukumu yake ndani ya maisha yetu kabla ya siku ile kutufikia; bado hilo nalo ni jambo lihusulo busara zake, rehema na haki yake mwenyewe Mungu. Lakini dhambi bado itapokea madhara yenye uharibifu mkubwa ndani ya maisha yetu iwapo tutachagua kutenda dhambi badala ya kuzitubia; kwa yoyote ile unavyoweza kutokea.

Pengine moja ya mambo ya kukumbukwa kwetu kwa kusema kibinadamu, ni jinsi ile ambavyo Mungu mara nyingi anavyoonekana kutokuingiza hukumu pale ambapo mtu kwa makusudi anaendelea kutenda dhambi pamoja na kuwadhuru wengine. Katika Yakobo upo mstari unaotufundisha sana (Yak.5: 6) katika jinsi ambavyo Mungu hawapingi watu mara nyingi watu wanaotenda uovu. Hawa watu wasio na haki wanafanya dhambi na kuwadhuru wengine bila kupata mateso au matatizo; hapo haionyeshi kuwa Mungu akiwazuia mbali ya kule kuwaadhibu tu. Kwa hakika hilo ndilo jambo mojawapo ambalo linawafadhaisha watu wengine katika Biblia kama vile mfalme Daudi. Kwa nini basi iwe hivyo? Kwamba Mungu asiingilie na kuleta hukumu juu ya watu wasio na haki (na hata juu ya baadhi ya wakristo) ambao mara zote wao wanaendelea kutenda dhambi au hata wakitukana watu wengine au wanakuwa ni watu wanaokwaza wengine? Hilo ni aina ya swali ambalo mfalme Daudi pia alikuwa akijiuliza yeye mwenyewe pale katika **Zab.73:1-7**. Daudi anashindana na tatizo hilo mpaka wakati ule anapopaingia mahala patakatifu pa Mungu, ambapo ndipo Mungu anamfungua ili aweze kuelewa mwisho wao. Katika ule mstari wa 17, kwa maneno mengine anaona kwamba, “Hawana usalama watu hao na wala hataweza kuikwepa hukumu”. Nami ninaamini, na huo ndio msimamo au mwelekeo wa Agano Jipya na hasa kwa muda huu wa sasa kwa sababu ya Kalvari.

Uvumilivu wa Mungu unawasubiri watu wamwitikie kwa kile alichowafanyia pale Kalvari (msalabani) na anawapa ile fursa ya kutubu, (Rumi 2:4; 2Pet 3:9; Yak.5:6). Mungu pia hufanya kwa uthabiti juu ya lile alilolitangaza, 2Kor.5:19, kama vile “Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na yeye mwenyewe asiwahesabie dhambi zao”. Rumi 5:6-10 na Mtd 17:30-31. Mistari hiyo hapo juu inazidi kukazia zaidi juu ya jambo hilo hilo. Muda huu Mungu anapanua neema yake na rehema zake na huku akizizuia hukumu zake ili watu wamjie wakatubu. Huu ndio mkazo mkuu wa Agano Jipya, Mungu akafa kwa ajili ya wenye dhambi wakati wakiwa wangali ni maadui zake, asiwahesabie dhambi zao bali akiwasihi watubu kwa sababu kila mmoja atafika mbele zake siku ile ya hukumu.

Nimeweza tu kugusia juu ya mambo haya, na mengi zaidi yangeweza kusemwa na kuelezwa, lakini ninaamini kuwa hivi imetosha kwa ajili ya kuonyesha sio tu jinsi gani hawa walimu walivyokosea na walivyo kinyume kabisa na Biblia.

## UMASKINI / UFUKARA

Ningependa kulitaja hapa jambo lingine ambalo nalo limekwisha sababisha mchanganyiko mkubwa wa huzuni pamoja na vifungo ndani ya mioyo na akili za watu wa Mungu. Hilo ni somo la ufukara; kuishi maisha ya hali ya uduni kama vile ilivyo kwa wakulima wadogo wenye kujitafutia riziki wanavyoishi - katika sehemu nyingi za Afrika. Kwa kawaida watu hao wanapaswa kufanya kazi kwa bidii sana ili kupata chakula cha kutosha, pamoja na mavazi yao kwa familia zao. Mara zote huwawia vigumu sana angalau kupata elimu ya sekondari, hii ina maana kuwa watoto wao nao wanaendelea kuishi kwa kulima kama wazazi wao walivyokuwa wakifanya. Kama itatokea kwao mvua ni nyingi msimu huo au pengine inyeshe chache, basi hapo huo kunaharibika na hivyo maisha humwia vigumu sana. Nayaelezea haya - ndiyo mazingira ya ujumla ambayo ndiyo yanaendelea kuwepo katika vijiji vingi sana mbali na sio katika maeneo yenye majanga maalumu ambako misaada mikubwa ya kuwaponya inahitajika.

Walimu, wahubiri, semina na vitabu vingi vimekwisha kuingia Afrika na kuwafundisha watu humo vijijini mwao kwamba eti “hali yao ya ufukara unaowaandama inatokana na laana au roho fulani ya umaskini. Ninapenda hapa nikuulize tena mpendwa msomaji, Je, mambo kama hayo yanaonekana sehemu gani ndani ya Agano Jipya? ***Je unaweza kweli ukaupata hata mstari mmoja ambao angalau unajaribu kutaja tu mbali ya kufundisha mambo hayo***? Je, umewahi kuona mitume pamoja na Yesu wakishauri mambo hayo kwa namna hiyo? Ni wapi ambapo wanaitambua hali ya ufukara kuwa ndiyo chanzo cha matokeo ya laana au roho ya umaskini? ***Basi sasa, hebu niseme wazi kabisa kutoka ndani ya moyo wangu kuwa mambo kama hayo hayafundishwi na wala hayapo kabisa ndani ya Agano Jipya.*** Huo ni ulaghai wa kikatili kabisa kwa binadamu na ni tatizo la ushirikina.

Tunawatendea dhambi ndugu zetu na kuwatumbukiza ndani ya vifungo na kukata tamaa pale tunapowapatia mafundisho ya jinsi hii yasiyotokana na fikra za kimaandiko ya neno la Mungu. Tunaweka nira ya mizigo mizito ndani ya mioyo na akili zao. Tunakuja huku tunawafundisha watu mambo haya kisha tunajiondokea,

tukiwaacha wao katika hali mbaya zaidi kuliko ile tuliyowakuta nayo pale tulipowajia pale tulipobeba haya mafundisho yetu, vitabu vyetu, na semina zetu kwa ajili yao. Kwa sababu hakuna hata moja kati ya mafundisho hayo ya uongo, vitabu hivyo vya uongo wala semina hizo za uongo ambazo zimefanikiwa kubadilisha mazingira ya watu hao au hata hatua tu ya maisha yao. Ikiwa mhubiri anakuja kwako na kuuamini ujinga huu, kwa nini basi haombi na kukemea hiyo “laana” au hiyo “roho ya ufukara” kwa jina la Yesu ambamo katika jina hilo tunao uwezo dhidi ya uwezo wote wa adui na pia juu ya hiyo laana? Kwa nini basi hawawafundishi watu wa Mungu kuondokana na laana hiyo au roho hiyo ya ufukara, ikiwa hilo ni tendo tu la makosa na mawazo yasiyo na nguvu zozote?

Haya basi imani pasipo matendo imekufa (Yak. 2:20), ikiwa mafundisho hayo yao ni ya Mungu, kwa hiyo basi usiwaelezee tu watu kuwa wayaamini pasipo kuwaonyesha uwezo wake. Jambo hili linahitajika kuwa zaidi ya maneno matupu, linahitajika kuwemo katika udhihirisho wa roho na uweza (1Kor.2:4; 4:19,20), vinginevyo utafanana na mtu yule ambaye Yakobo anamwelezea katika waraka wake (Yakobo 2:15,16), ambaye anasema kuwa, “Ndiyo - mkaote moto na kushiba”, lakini asiwape mahitaji ya mwili yafaa nini? Anawaacha vile vile kama alivyowakuta! ***Na hata hivyo hawa walimu wanakuja na kisha wanajiondokea zao na kuwaacha watu wa Mungu wakiwa hawana mabadiliko yoyote yale - mbali ya kwamba wamewasababishia watu wa Mungu wajisikie kusumbuliwa zaidi juu ya laana au juu ya aina fulani ya maroho mabaya na hivyo kuwaweka katika eneo la huzuni!*** Mafundisho hayo hayajafanikiwa kubadilisha chochote kile katika maeneo yale ambayo nimewahi kutembelea katika nchi ya Tanzania. Kwa kweli yameshindwa kubadilisha maisha ya watu na kamwe, hayawezi hata kama tutayapatia muda mrefu kuwepo katika jamii. Mafundisho hayo yameshindwa kufanya hivyo, vitabu hivyo vimeshindwa kuleta mabadiliko wala semina hazikuweza chochote. Kwa nini wameshindwa? Kwa sababu elimu itolewayo na walimu hao katika semina zao, vitabu vyao na mahubiri yao vinapingana na neno la Mungu, pia inapingana na mpango wa Mungu kwa watu wake ndani ya muda huu wa Agano Jipya. Mbali ya kuwa elimu hiyo wanayoitoa husababisha kuchanganya akili za watu na kuwatumbukiza katika vifungo kwa kuyafuatilia mawazo haya yenye kasoro na madhaifu.

Wapendwa, mafundisho hayo ni ya uongo, Agano Jipya halifundishi hivyo, wala Biblia kwa ujumla wake haifundishi hivyo. Katika Mtd tunasoma habari za wajane fukara. Kanisa lilikuwa likifanya kazi ya kukusanya fedha na kuzisambaza kwa watu fukara. Hilo lilikuwa ni tendo la kawaida kabisa ndani ya kanisa la Agano Jipya (Mtd.11:29; 2Kor.24: 17; Rumi 15:25,26; 1Kor.16:1-3; Gal.2:10; 1Yoh.3:17). ***Lakini sasa pamoja na hayo yote hakuna mahala popote pale ambapo tunakuta mitume wakisema kwamba, maisha ya kiufukara yanasababishwa na laana au roho chafu.*** Kulikuwepo na watu mafukara ndani ya nyakati za Agano Jipya, kama vile walivyo leo pia; kulikuwepo pia mafukara waliokithiri nyakati za Agano la Kale kama ilivyo leo pia.

Wote tunakumbuka mama yule aliyeshindwa, na kusubiria afe yeye na watoto wake kwa sababu ya ufukara wake, kisha anamlalamikia mtu wa Mungu naye anampa mafuta atumie kisha yanayosalia akauze akalipe wadeni wanao ndani. Hakuna lolote lile lililobadilika kufuatia hali hiyo. Kwa hiyo basi kwa nini watu wanadhani kwamba wanaweza kulibadili neno la Mungu pamoja na mafundisho yake? Mtume Petro pale katika Mtd.6; wala Mtume Paulo katika 2Kor.8, kadhalika Yohana katika nyaraka zake, kamwe hasemi kuwa, “Aha, aha, kuna umaskini uliokithiri! Inawezekana basi kuwa hii yote imesababishwa na laana fulani pamoja na maroho ya ufukara! Hebu basi sasa tuombe na kuzivunja nguvu zake na kuwa wamefunguliwa na kupata mafanikio mema! (Na kisha ndipo kanisa halitakuwa na mzigo tena wa kutoa kwa ajili yao!). Hilo lingekuwa ni jambo la upumbavu kwao kufanya hivyo, na kwa kweli ni upumbavu mtupu kuwaona watu wa magharibi wakija Afrika na kufanya mambo ya jinsi hiyo leo!

Katika Agano Jipya inaonyesha wazi kwamba hali ya ufukara itaendelea kuwepo, hivyo kwa ujumla wake inapokelewa kuwa sio kitu chochote kisichokuwa ni cha kawaida, isipokuwa hiyo ni sehemu ya maisha katika jamii. Maisha yako hivyo wakati mwingine na katika maeneo fulani na unapaswa kupambana nayo kama vile unavyopambana na mazingira ya kawaida ya maisha na roho chafu ya ufukara au laana. Kama vile walivyofanya katika Agano Jipya. Wala ufukara haumjui mtu eti kwa sababu yeye amependa awe hivyo? Hapana. Wala si kwa sababu mtu fulani alisema itapasa kuwa hivyo. Hapana. Isipokuwa Yesu alionyesha kuwa maisha kati ya watu katika jamii yapo hivyo kwamba kutaendelea kuwa na watu fukara - soma Yohana 2:8. Na hata Yesu mwenyewe alikuwa na wanafunzi wakibeba mfuko ambao ulikuwa na fedha kwa ajili ya kuwagawia watu masikini. Soma tena Yohana 12:6; 13:29! Hivyo ndivyo walivyofanya Yesu pamoja na mitume wake; walikusanya fedha kwa ajili ya watu masikini! Yesu mwenyewe hakuweza kuzunguka huko na huko ili eti akakemee roho za ufukara au kuivunja laana ya ufukara! Yesu aliyajua mambo yote na angeweza kuyatambua mambo yote na alikuwa na uwezo wote. Mbali ya ukweli huo wote, bila shaka yoyote ile yeye hakutambua roho au laana ya ufukara na wala hakuomba kwa ajili ya mambo ya jinsi hiyo, wala mitume hawakuomba kwa ajili ya hilo pia - vipi sasa kuhusu wewe?

Katika Mtd.6, kulikuwa na wajane, waume zao walikuwa wamekufa. Waume hufa pia huko Uingereza, na nafikiri kuwa wanafariki hata Tanzania pia. Hii haishangazi. Ni sehemu ya maisha, huwa inatokea wala hiyo siyo laana au roho chafu kwa kusema kwa ujumla. Haipo maana yoyote ya kukemea kitu chochote kile hapo. Hilo halitawasaidia wajane wale! Kama ilivyo katika Mtd 6, ndivyo ilivyo Tanzania na nchi nyinginezo pia, ikiwa mume wa mwanamke akifa, mwanamke huyo ambaye aweza pia kuwa na watoto, anaweza kuachwa pasipo namna yoyote ile ya kujipatia fedha za kutosha ili kumwezesha yeye na watoto wake kuishi vizuri. Anaweza kuwa ameachwa akiwa fukara, hayo ni madhara ya kawaida ya maisha katika hali nyinginezo.

***Na hapa ndipo mahala ambapo upendo na upole wa Kristo unapaswa ujionyeshe wenyewe kupitia watu Mungu kwao hao walio katika uhitaji***. Hivi ndivyo tunavyopaswa kujifunza na kufanya, 1Yoh.3: 17. Wakati nabii Agabo alipotangaza kuwa kutakuwepo na ukame katika mji mzima, mitume hawakuitangaza kwamba hii ni aina ya laana inayotokana na viazazi vilivyopita au maroho ya uovu ambayo yangepaswa kukemewa! Sivyo kabisa. Kwa kadiri tunavyoweza kuona jambo hili wala halikuwajia akilini mwao ili kuwazia juu yake. Walifanya nini sasa? ***Waliamua kutuma fedha kwa wale wasiojiweza kule Yudea. Na hayo ndiyo tunayoyaona yakifanyika katika Agano Jipya lote***. Mitume hawakuwaachilia watu masikini waendelee kuwa masikini kana kwamba hilo lilikuwa ni janga lao. Siyo hivyo kabisa. Sisi sote ni wana wa Mungu kupitia Yesu Kristo, hatuamini juu ya aina fulani ya majanga yasiyo ya ki-mungu au kuwaacha watu katika hali yao ya taabu. Tunapaswa kuonyesha ule upendo wa Yesu Kristo pale ndugu zetu wanapoteseka na sio kufunga mioyo yetu kwa matatizo yao. Ikiwa Mungu amekuendeleza wewe kama kanisa, Je, unatumia kiasi gani basi kwa ajili ya majengo ya kanisa lako na kiasi gani unakitumia katika kuwaendeleza ndugu zako, ambao wanateseka kwa wakati fulani? ***Karibu fedha zote zilizokuwa zinakusanywa na kanisa wakati wa Agano Jipya, ilikuwa zinakusudiwa kuwapatia ndugu walio masikini.***

Hebu ujifunze kutoka katika Matendo ya Mitume na nyaraka nyinginezo zilizomo katika Agano Jipya, ndipo utagundua kuwa hivyo ndivyo ilivyokuwa! Pale mwanzoni kabisa mwa kitabu cha Matendo ya Mitume tunasoma kuwa, kanisa lilipokea kiwango kikubwa cha vitu pamoja na pesa, na walizigawa hizo, “kufuatana na hitaji la kila mtu” Mtd 2:45. Zipo pia kumbukumbu nyingine ambazo zinatuonyesha wazi kuwa wale waliodumu katika kuhudumia neno la Mungu walipokea msaada wa fedha nyakati nyingine. Yapo baadhi ya mausia yanayowahimiza watakatifu kufanya hivyo; lakini kutoa huko walikofanya kulielekea kuwa katika mfumo wa tabia ya hiari zaidi (1Kor.9:1-5; 1Tim.5:17,18). Lakini sasa, kukusanya fukara, kunaonyesha kuwa kulikuwa kunategemewa au kuhitajika kuwa ni sehemu ya maisha ya kanisa na huduma zaidi. (Rumi 15:25-27, 1Kor. 16:1-3).

***Je, tumepoteza mwelekeo wetu kidogo? Je, fikra zetu za kiroho au mafundisho zimeifanya mioyo yetu iwe migumu kwa ajili ya mahitaji ya ndugu zetu ambao kwa wakati fulani wanakuwa hawana mavazi ya kutosha au kupungukiwa na chakula?***

Nisingependa mtu yeyote yule anielewe vibaya. Hapa sisemi kwamba mtu fulani yeye binafsi kila mara lazima kuwa ni fukara, wala pia sisemi kuwa mambo hayawezi kubadilika kwa mtu, sipendekezi juu ya maisha ya mtu mmoja mmoja, isipokuwa mimi naongelea kuhusu sababu au asili ya ufukara katika maisha ya vijijini, na jinsi ambavyo sisi kama inavyojitokeza na vile ambavyo inawasilishwa kwetu.

Kama ikitokea kuwa mmoja bado ananielewa tofauti, hebu basi niongeze kuwa, ikiwa wewe ni Mkristo, basi neno la Mungu na Roho wa Mungu wote pamoja wataweza kukufundisha ili usiwe mzembe bali uwe mwenye bidii katika kazi na kuwa mnyofu na mwaniminifu. Na kama hakuna kazi nyingine basi utaweza kutafuta au hata kubuni fursa ya kukupatia halali - ukizikabidhi njia zako kwa Mungu na kuyaweka matumaini yako kwake ili kwamba na wewe uwe na kitu cha kuweza kuwapatia watu wengine. Na kwa watu wengine ambao kabla hawajaokolewa hawakuwa hivi kuboresha katika hali ya namna hiyo, mambo haya sasa ndani yao yanaweza kuwaongezea maisha yao sana. Lakini pale inapotokea hali kuwa ni ngumu, bila kujali chochote kile, wale wanaoyaweka matumaini yao kwa Mungu na kuutafuta Ufalme wa Mungu kwanza watazijua baraka za Mungu na wema wake na neema kuhakikisha wanavuka hata nyakati hizi ngumu. Na ninafahamu kuwa wapo watu wengi ambao wanaweza kushuhudia jambo hili.

Ni kweli kabisa kwamba Mungu aliwafanya masikini wa ulimwengu huu wawe ni matajiri wa Imani! Hata kama tunayo maendeleo mengi au kidogo sana; mara zote Mungu anatutaka tuyaweke matumaini yetu kwake na kumtukuza yeye ili kwamba ulimwengu upate kuona kuwa tupo tofauti nao na kwamba Kristo kwetu ni bora kuliko kitu chochote kile. Na pale ambapo watu wa Mungu watakuwa wameweza kuyafanya yale yote wanayoweza kuyafanya lakini bado pamoja na hayo wanakuwa wakiendelea kuteseka kwa kukosa mahitaji makuu na (muhimu) hapo sasa ndipo kanisa linapaswa kuwa na huruma na kutuma msaada.

Nimebarikiwa sana kusafiri katika vijiji hivyo na kuwakuta ndugu wakiwa na nguo chache sana, hawana chakula cha kutosha pamoja na vitu vingine vichache sana, wakifanya kazi kwa bidii sana ili kupata hayo waliyonayo. Na wakati mwingine wakishuhudia kwa kuona hata hayo waliyo nayo yakiteketezwa kutokana na hali mbaya ya hewa ya eneo hilo, lakini hata hivyo watu hao bado ni watu wa shukrani mioyoni mwao mbele za Bwana na hata wanaweza kumsifu na kumwabudu Mungu katikati ya dhiki nyingi walizonazo. Ni ushuhuda wa ajabu jinsi gani kwa Bwana!

Tafadhali usinielewe vibaya, mimi huwa siji tu na kuangalia; bali huwa natoa kile ninachoweza kulingana na uwezo wangu ili kuwasaidia ndugu zangu. Lakini ninachoweza kusema hapa ni kwamba mafundisho hayo ya kisasa ni ya kikatili, yanahamasisha matarajio miongoni mwa watu wa Mungu ili waone kwamba vitu vinaweza tu kubadilika kihadithi wataweza kuivunja laana au kuikemea ile roho mbaya ya umasikini. Lakini kwa ukweli hayapo mabadiliko yoyote ya kimchezo kutoka kwa aina hii ya maombi na badala yake ndugu zetu wanaachwa katika hali ya kujisikia vibaya juu ya laana fulani ya roho ya uovu ambayo wao hujiona kuwa hawawezi kujinasua kwayo. Ninafahamu kuwa vipo vitabu vinavyosema mambo hayo, nami nawaambieni kabla kwamba mambo hayo wayasemayo siyo ya kweli na wala hayafundishwi hivyo ndani ya Agano Jipya.

Wapendwa wasomaji, napenda kusema tena na ninawatieni moyo kuwa usiyapokee tu haya maneno yangu, isipokuwa uyachunguze maandiko ili kuona kama ni hivyo katika neno la Mungu.

**Magome, Ilula na Iringa**

Hebu nieleze kile ninachokisemea kwa kufananisha na sehemu zinginezo ambazo nazijua. Katika milima ya Udzungwa kuna kijiji kiitwacho Magome; ili kukifikia kijiji hicho unahitajika upate gari la abiria (basi) kutoka mji wa Iringa ambako litachukua muda wa masaa manne yenye mavumbi; kisha baada ya hapo bado utahitajika utembee mwenyewe kwa miguu zaidi ya masaa mawili ili kufikia Magome. Katika kijiji hicho hakuna viwanda, hakuna biashara yoyote ya uhakika na hakuna maduka mbali ya vile vijibanda (vijigenge) vidogo vidogo. Wengi wa wanakijiji wa huko ni wakulima wadogo wadogo. Sasa hebu jaribu kufikiria, iwapo mtu atazaliwa katika kijiji hicho cha Magome ni dhahiri kwamba wazazi wake ni wakulima, kwa hiyo yamkini anaweza kupata uwezo wa kwenda shule ya msingi ijapokuwa hiyo nayo ni gharama kwao.

Lakini kwa ujumla haupo uwezekano wowote wa mtoto kufikia shule ya sekondari: Kwanza haipo shule ya sekondari hata moja hapo kijijini Magome - na shule iliyopo karibu na kijiji hicho, ipo mbali sana na ile iliyopo jirani hapo ni shule ya binafsi inagharaama zaidi. Kwa hali hiyo watoto hawawezi kupata elimu yoyote ya sekondari na wala kwa ujumla wake hawana fursa ya kupata kusomea ujuzi wa ufundi kama vile useremala au umakanika kwa sababu mafunzo ya aina hiyo pia yana gharama kwa hali yoyote ile. Kwa hiyo watoto wanapomaliza shule ya msingi, mara moja huendelea kuwasaidia wazazi wao kwenye mashamba yao kisha hatimaye na wao hugeuka kuwa ni wakulima wadogo wadogo wakiandamwa na kazi ngumu pamoja na maisha ya ufukara ambayo hurithishwa na hali hiyo.

Sasa, kipo kijiji kingine ambacho ni kikubwa kando kando ya njia kuu kuelekea mji mkuu wa mkoa huo wa Iringa, kijiji hicho kinaitwa Ilula. Na hapo kwenye kijiji hicho kuna biashara nyingi kama vile maduka, wafanyabiashara mbali mbali halikadhalika na wakulima, hapo ipo pia shule ya sekondari; sasa, iwapo utakuwa wewe umezaliwa katika kijiji hicho, basi bila shaka familia yako yaweza ikawa katika hali nzuri ya nafasi nzuri, au kwa kule kuwepo kwa shule ya sekondari hapo; ipo fursa kubwa ya wewe kuingia shuleni hapo iwapo wazazi wako ni watu wenye maendeleo, au ni watu waliojitunzia akiba kwa madhumuni hayo. Zaidi ya hayo yote ipo fursa pia ya wewe kupata kazi mahala kama hapo; kwenye vile viduka vya wenyeji au biashara au hata kuchagua biashara kwa ile elimu unayoipata au fedha unazojiwekea akiba zinaweza kukuwezesha hata kusafiri kufika mjini Iringa ili kuendeleza matarajio yako. Ninawajua watu ambao wameweza kufanya vile vile kama hivi ninavyoeleza.

Lakini pamoja na hayo yote huwa inakuwa ni jambo la tofauti kabisa iwapo wewe utakuwa umezaliwa katika mji mkubwa wa Iringa. Kwa sababu hapo utazikuta zipo shughuli za biashara mbalimbali pamoja na viwanda kadhalika na maduka mengi yasiyoweza kuhesabika pamoja na biashara na wauzaji. Ikiwa wewe sasa, utakuwa umezaliwa katika mji, hapo, ndipo upo uwezekano kuwa familia yako itakuwa ni yenye nafasi ya kutosha. Kutakuwepo pia na fursa kubwa ya kupata haki ya elimu nzuri kukufikia karibu kabisa na mlangoni pako, bila kuzitaja fursa zozote zinazopatikana hapo pia. Bado mahali kama hapo kutakuwepo na kutafuta kazi au kujifunza mambo ya kibiashara, ingawaje si rahisi kwa kila mmoja kuwa hivyo, lakini kuna uhakika wa fursa ya aina hiyo kuwepo pale ili kukuendeleza. Unaweza kuishi na kazi inayokulipa vizuri na yenye kukuendeleza vizuri.

Sasa tutasemaje? Je, tuseme kwamba ipo laana kubwa kule katika kijiji cha Magome, na laana kidogo katika kijiji cha Ilula, kisha kwamba hakuna laana kabisa katika mji wa Iringa? Na hapo kisha kuna nini tena? Kwamba mji mkuu wa biashara wa Dar es salaam utakuwa umebarikiwa na Mungu kwa hakika? Kwa vyovyote vile, kuwa na mawazo kama hayo ni ukamilifu wa udanganyifu! Lakini sasa hivyo ndivyo watu wengi wanavyofikiri. Wao wanafikiri kwamba maisha ya taabu na ile hali ya kufanya kazi inasababishwa na laana za mikoa na za uenyeji zinazowajia watu kutoka kwa mababu zao! Kwa kweli hivyo ndivyo tulivyokuwa tukifikiri pale zamani kabla ya kuokolewa kwetu na pale tulipokuwa tukiishi katika hofu na desturi za kiuchawi.

Nimewahi kufika katika vijiji hivyo vyote nilivyovitaja hapo juu, nami ninaweza kukuambia wazi kuwa hali iliyopo huko haitokani na aina fulani ya laana hata kwamba iweze kusababisha tofauti hizo za kimaisha. Na pia sio kweli kuwa mtu awapo katika mji mkubwa ndivyo hubarikiwa zaidi kuliko kule vijijini. ***Kunawezekana kukawa na uchoyo, uovu na ulafi katika miji mikubwa kuliko ilivyo vijijini, sasa kwa nini basi miji hiyo haiteswi zaidi kwa laana kuliko vijijini?*** Sababu inayopelekea kuwepo kwa tofauti ni ***zile fursa walizo nazo*** watu au wanazozikosa katika kupata kazi ya mshahara au kupata elimu. Katika kijiji ambacho kiko mbali sana kutoka barabarani, (barabara kuu) au mji - halipo hitaji au lengo kubwa au fursa kubwa ya kuanza kwa biashara. Maisha ya watu huko yanabakia kuwa ni ya kienyeji sana na madhara yake hapo kunakuwa na nafasi au fursa chache sana huko kwa ajili ya mtu kujiendeleza au hata kupata kazi ya mshahara. ***Hayo yote ni madhara ya kawaida yatokanayo na hali ya kawaida***! Na kwa serikali ambayo haina fedha (siyo tajiri) inajikuta kuwa ni shida au vigumu sana kugharimia kwa ajili ya kuwa na shule au vyuo kwenye maeneo ya vijijini kule ndani kabisa; halikadhalika wafanyabiashara nao hawaoni sababu ya kupeleka biashara zao huko vijijini ndani kabisa ambako hata wakazi wake huwa ni wachache pia, mambo hayo yote ni mambo ya kawaida kuyafikiria. Na kwa hiyo, kutokana na fursa nyingi zilizopo katika miji, watu wanaweza wakajifanyia vizuri zaidi huko kwa kujitafutia riziki zao.

Badala yake sasa, hawa walimu wa kisasa wanawazamisha watu katika mawazo ya njia za kiushirikina ambazo huwafanya wawe vipofu kwa mambo yaliyo wazi kabisa. Kwa kweli mafundisho ya walimu hao yanafanana na ulozi, Gal.3: 1, ambayo huyaondoa macho ya watu mbali kabisa na Yesu ili wasiangalie kile ambacho alikifanya kwa ajili yao, na yanawazamisha ndani ya udanganyifu mtupu. Nimewahi kuhubiri na kufundisha katika maeneo ya vijiji vyote nilivyovitaja hapo juu. *Hebu niseme jambo langu binafsi*; na kwa usemi wa kiujumla imekuwa ni rahisi kuhubiri kule ambako hali ya maisha ni ngumu, kuliko katika miji. Siwezi kuelewa vizuri iwapo hiyo inatokana na ukosekanaji wa mambo mengine, kwamba labda watu wa vijijini wanayo njaa zaidi na nia ya hamu ya kuyasikiliza maneno ya Mungu na kumfahamu Yeye, katika vijiji kuna uhakikisho huo kwa kanisa la Bwana na kwa neno lake ambalo huwezi kulipata kwa kipimo kile kile huko mijini.

Hapa, ninaongelea mambo ***ya kiujumla sana***; kama vile ninavyofahamu kwamba kunaweza kukawa na tatizo katika kanisa la vijijini lilelo la namna ile ile kama ilivyo kwa kanisa la mjini. Lakini kile ambacho naweza kusema kwa uhakika ni kuwa wakristo waliopo mijini na miji mikuu kwa vyovyote vile hawabarikiwi zaidi kuliko wale wanaoishi katika hali ya ufukara katika vijiji. Kila mmoja anayeliweka pendo lake kwa Bwana huwa anabarikiwa bila kujali mahali popote pale alipo! Lakini kama tunaweza kuliongelea hilo, kwa ujumla inaonyesha kuwa watu wale walioko vijijini wamebarikiwa zaidi kuliko wale walioko mjini ambao wanahusisha mwendo wa maisha yao pamoja na Bwana ambayo kwa ujumla ndilo jambo la muhimu sana. Kile kinachowabariki watu wa mijini yawezekana ikawa ni kule kuwa na vitu vya pekee pamoja na kuwa na kazi zenye kuwaendeleza na zenye kuheshimiwa ambazo ndizo tunazoziita kuwa ni “baraka” ambazo nazo bado zikawa ni mtego pia kwa watu wa Mungu na hata zikawasababishia mioyo yao kupoa mbele za Bwana. Kisha “baraka” yako hutokea kuwa ndiyo anguko lako. Tafadhali unielewe, sisemi kuwa kupata elimu nzuri au kazi nzuri ni vibaya. Hapana. Isipokuwa tafadhali naomba tusichanganye ile maana halisi ya kubarikiwa kikweli. Iwapo utajisomea mwenyewe pale kwenye Ufunuo 2:9 na 3:17 mistari hiyo inaweza kusaidia sana kufafanua kile ninachojaribu kukisema mahala hapa.

Hatimaye hebu niseme kwamba, kunaweza kutokea kuwepo na baadhi ya watu katika baadhi ya vijiji ambao huyapinga mabadiliko ambayo yanaweza yakaleta faida katika kijiji kile. Lakini hiyo siyo sawa na kuwepo kwa laana katika kijiji, huu ni upinzani wa watu na pengine wanaweza wakawa wanashawishiwa na matendo maovu, isipokuwa hakuna lolote lile katika Agano Jipya linalotufundisha sisi ili tudumu kuomba kwa ajili ya laana katika kijiji. Lakini mtu anaweza kuomba kwa ajili ya watu au kwa ajili ya kazi ya Mungu ipate kuendelea mahala popote pale unapopaona wewe mwenyewe. Yesu Kristo pamoja na mitume wote kwa pamoja walikutana na upinzani kutoka kwa watu katika miji, lakini hata hiyo haikuhesabiwa kuwa ni laana iliyopo katika miji inayopaswa kuvunjwa. Upinzani kwenye kazi ya Mungu haukuja kutokana na laana. Ilitokana na ugumu na kutokuamini kwa mioyo yao Mt.13:58; Mtd 13:45,46; 17:32-34; 19:23-41. Bila shaka nguvu za giza na Shetani wanapinga kazi ya Mungu kupitia ugumu wa mioyo ya watu lakini kama tulivyoona, ndiyo watu wanaompa Shetani nafasi hii. Katika Mtd sura zote mbili ile ya 17 na 19 tunakutana na watu

ambao wanaishi sana katika dhambi na mambo ya kuabudu masanamu, lakini bado mitume hawatubu kwa ajili ya dhambi hiyo ambayo wameikuta huko wala hawaendi huko na huko ili kwenda kuvunja baadhi ya laana katika miji itokanayo na kuabudu masanamu huku kama kwamba hiyo ndiyo inayozima kazi ya Mungu; wala pia hawaonekani kuwahimiza watu wengine au hata kuwafundisha kufanya hivyo. Pia mitume hawakutaji au kufundisha kitu cho chote kwao watu wa mataifa juu ya laana inayotajwa katika kitabu cha Mwanzo (kwa mfano, Mwanzo 9:24) au katika Agano la Kale kwa ujumla. Walihubiri Yesu Kristo tu! Mungu asifiwe!